# Nipashe

Alhamisi Novemba 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581139

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13


SUPA JACKPOT

TZS. 1,053,232,366

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




RIPOTI MAALUM

**Mabadiliko tabianchi yalivyoathiri huduma ya maji na chakula**

UKURASA 4

# GIZA NENE

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**MWALIMU AUAWA BAADA YA KUDAIWA KUWA MWIZI**

ALIYEKUWA Mwalimu wa Shule ya Msingi Livingstone, Erick Mbilinyi, mkazi wa mtaa wa Mgendela katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ameuawa na wananchi wenye...

UKURASA WA 7

**JITIHADA ZA RAIS SAMIA MSIMBAZI ZAZAA MATUNDA**

JITIHADA za Rais Samia Suluhu Hassan, tangu akiwa Makamu wa Rais kuhusu uendelezaji bonde la Mto Msimbazi kwa kuwasaidia wananchi waondokane na...

UKURASA WA 8

**KIGOGO CUF ATIMKIA CCM**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimepata pigo, baada ya Mwenyekiti wa chama hicho Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Jamal Salehe, kutimkia Chama Cha Mapinduzi (CCM)...

• **TANESCO** yakiri hali ngumu, megawati 414 zakosekana kisa ukame, yatoa majawabu kukabili... *Endelea ukurasa 2*



Wafugaji wa Kata ya Paranga, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, wakinywesha maji mifugo huku wananchi wakiwa wamepanga foleni kusubiri kuchota maji hayo, mapema wiki hii. **PICHA: GWAMAKA ALIPIPI**

## Samia ashtushwa kasi ya matukio ukatili kijinsia

UKURASA 2



## Ripoti ajali ya ndege yaacha maswali, Majaliwa hayumo

UK.3



**MICHEZO** NABI AFUNGUKA YANGA SC NI MOTO UK.32

**KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati akimsikiliza Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, aliyekuwa akielezea maendeleo ya ujenzi wa hospitali hiyo, mjini Babati, mkoani humo jana. **PICHA: IKULU**

# Giza nene makali mgawo umeme

**Na Mauld Mmbaga**

NI GIZA nene. Ndivyo uhalisia ulivyo kuotokana na kuendelea kwa makali ya mgawo wa umeme unaotokana na hali ya ukame nchini na kusababisha baadhi ya mabwawa ya kuzalisha nishati hiyo kufanya kazi kwa kiwango kidogo.

Baada ya wananchi katika maeneo mbalimbali kulalamikia makali ya mgawo wa nishati hiyo huku wengine wakisema zinaweza kupita hata siku mbili wakakosa huduma huyo, jana Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) liliitisha mkutano wa waandishi wa habari na kuweka bayana hali halisi.

Katika mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam, shirika hilo lilisema umeme ambao hauzalishwi kutokana na ukame na matengenezo mengine, ni megawati 414 hadi jana asubuhi, hivyo kuathiri upatikanaji wa nishati hiyo.

Aidha, TANESCO ilisema megawati 300 hadi 350 zimepungua katika uzalishaji kwa siku za hivi karibuni kutokana na vyanzo kukauka kwa sababu ya ukame.

Akizungumza jana katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema kutokana na tatizo hilo, jitihada zinafanyika kutafuta vyanzo mbadala ili wananchi waendelee kupata nishati hiyo.

Chande alisema ukame umesababisha kupungua kwa kina cha maji katika Bwawa la Kihansi ambalo lilikuwa likizalisha megawati 180 lakini zimeshuka hadi 17 na zikipanda hazizidi 30 huku magawati 163 hazizalishwi.

Kwa mujibu wa Chande, chanzo kingine ni kituo cha Pangani ambacho awali kilikuwa kinazalisha megawati 68 lakini kwa sasa kinazalisha megawati 10 na kufanya upungufu wa 58.

Pia alisema bwawa la Mtera uzalishaji umepungua kutoka magawati 180 hadi 175 huku Nyumba ya Mungu lililokuwa likizalisha megawati nane, kwa sasa linazalisha megawati tatu.

Mkurugenzi huyo alivitaja vituo vilivyoko kwenye matengenezo kuwa ni Kidatu kilichokuwa kinazalisha magawati 200 na sasa ni 150 na kufanya upungufu wa 50 na Ubungo III iliyokuwa inazalisha megawati 112 na sasa kinazalisha 32 huku Kinyerezi II iliyokuwa inazalisha megawati 248 sasa inazalisha megawati 195.

"Hivi karibuni tumekuwa na matatizo makubwa ya upungufu wa umeme ambao umesababisha shirika kushindwa kuhudumia wateja wetu vile tunavyotaka. Katika kipindi hiki kigumu tunahakikisha tunatoa taarifa sahihi kwa wateja wetu za hali ya umeme inavyoendelea," alisema.

"Kutokana na upungufu wa umeme uliopo, hatua za kushughulikia mfumo zisipochukuliwa, mfumo utaanguka. Ili mfumo usipate hitilafu inabidi maeneo mengine yasipate umeme na ratiba zinazotolewa na kwa kiasi kikubwa zinafuatwa," aliongeza.

**HATUA ZA MUDA MFUPI**

Chande alisema juhudi za muda mfupi zinazofanyika katika kukabiliana na tatizo hilo ni kuelekeza nguvu kwenye vituo vya gesi na kuharakisha matengenezo kinga na marekebisho yanayofanyika kwenye vituo.

Alisema kituo cha kwanza ambacho wanakishughulikia ni Ubungo III ambako kuna mashine zinazofanyiwa matengenezo kinga na nyingine marekebisho za megawati 40, na kwamba leo zinatarajiwa kurudishwa kwenye mfumo baada ya matengenezo kukamilika.

"Matengenezo ya megawati 20 yanatarajiwa kukamilika mwezi huu ambazo zitarudishwa kwenye mfumo na jumla zitakuwa 60. Ikifika Desemba tutapata megawati 20 na kufanya jumla ya megawati 80 kurudishwa kwenye mfumo na sehemu zinazokosa umeme zitazidi kupungua.

"Juhudi nyingine tunafanya matengenezo katika kituo cha Kidatu ambacho kina mashine ya megawati 50, na tunatarajia wiki ijayo kitarudi kwenye uzalishaji, na kufanikisha megawati 130 kurudi kwenye mfumo," alisema.

Pia alisema jitihada zingine ni upanuzi wa Kinyerezi I, na kwamba wanategemea mpaka mwisho wa mwezi huu, chote kitaweza kuwa kimeingia kwenye mfumo na kwa sasa wako kwenye majaribio yatakayowezesha kupatikana megawati 90.

Kuhusu muda wa kati, alisema Kituo cha Kinyerezi I kina megawati 180, hivyo wanatarajia Januari na Februari, mwakani, megawati zingine 90 zitaingia kwenye mfumo.

**MUDA MREFU**

Pia alisema jitihada za muda mrefu wanazozifanya ambazo ni za zaidi ya miezi 12 mpaka 18, matumaini yao ni kukamilika kwa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, akieleza kuwa litakapokamilika adha ya kukatika kwa umeme itakuwa imekwisha.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA MAELEZO YA MASLAHI KWA RANGI YA KUREKEBISHA MIPAKO**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0011**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ugavi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia mafuta ghafi kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni yenye wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa rangi ya Kurekebishia Mipako (Coating Repair Paint).**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuko wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Makadirio ya lita 12000 za rangi kutumika,
- Dhamana (warranty) ya ugavi itatolewa kwa rangi,
- Kwa miundo ya HDG, tutahitaji rangi yenye zinki (I-pack inorganic zinc-rich paint) kama vile mipako ya ZINGA (ZINGA Coating) au sawa na ISO 1461,
- Kwa miundo ya Chuma kama vile Piles na Trusses, tutahitaji glassflake reiforced epoxy na phenolic epoxy primer na topcoat,
- Usafiri kutoka kiwandani hadi bandari ya Tanga,

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Makampuni yanayoonyesha nia yao yanaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha vifuatavyo:

- Wafanyakazi walioidhinishwa kufanya kazi za Uthibitishaji Ubora / Udhibiti Ubora (QA/QC)
- Kipindi cha dhamana (Warranty Period) wa miezi 24 na miaka 5 juu ya kasoro za siri (latent defects) baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi husika inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma sawa za ugavi unaohitajika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa,
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya, Mazingira Usalama eneo la Kazi na vyeti vya Ubora vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawia.
- Alama ya Ubora ya CE na vyeti vyote vya ubora wa vifaa.
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Hati zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **8 Desemba 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji, yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17162002


# Samia ashtushwa ongezeko ukatili kijinsia

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza kusikitishwa na kasi ya matukio ya ukatili wa kijinsia nchini, huku akitaka hatua za jumla kuchukuliwa hasa kwa mkoa wa Manyara ambao taarifa zake zilimshtua.

Kutokana na kasi hiyo, ametaka wote wanaohusika na utoaji haki kuhakikisha wanashughulikia upatikanaji wa haki za watoto na wanawake wanaofanyiwa ukatili huo.

Akihutubia mamia ya wananchi wa Babati kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Kwaraa, mjini hapa, Rais Samia alisema takwimu za mwaka jana zilizoko mezani kwake zinaonyesha kuwa katika mkoa wa Manyara kulikuwa na matukio 3,641 waliyofanyiwa wanawake na watoto.

Pia alisema matukio hayo yanaonyesha kesi 792 ni mashambulio ya kimwili na 708 ni za kingono kwa watoto.

"Kufanya ukatili wa aina hii siyo sifa. Watu wa Manyara tuhakikishe tunabadilika kitabia," aliagiza Rais Samia.

Rais Samia aliagiza wataalamu wa maendeleo ya jamii na mahakimu kuhakikisha wanashughulikia upatikanaji wa haki kwa watoto na wanawake, ambao wanafanyiwa unyama huo.

Kuhusu ukame, Rais Samia aliagiza kufanyika tathimini ya kina ya athari za uharibifu wa mazingira katika Ziwa Babati, Basutu na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, ili kubaini ukubwa wa tatizo hilo.

Alisema tathimini hiyo ifanywe haraka na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na maofisa mazingira wa halmashauri za mkoa wa Manyara.

"Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, nawaagiza waje kufanya tathmini ili kuona maeneo yanayoharibiwa. Kazi hiyo ifanywe kwa kushirikiana na maofisa mazingira wa halmashauri za wilaya zenye tatizo la uharibifu wa mazingira kwenye maziwa," aliagiza.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha kufanya uharibifu wa mazingira katika maziwa hayo, akiagiza kuanzishwa kampeni maalum ya upandaji miti kuzunguka maziwa hayo, ili kuepusha kuendelea kwa mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa Rais Samia, uharibifu huo wa mazingira unaofanywa na wananchi kutokana na shughuli za kiuchumi, umeanza kuleta athari za moja kwa moja za kuwapo kwa kipindi kirefu cha ukame, kilichosababisha pia kupoteza mifugo mingi mwaka jana.

"Twendeni tutunze mazingira yetu ili tuepuke mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha njaa, ukosefu wa maji na umeme na kuathiri viumbehai. Serikali itajenga mabwawa ya maji, ila naomba ushirikiano wa wananchi yatakapoanza kujengwa mchangie fedha mradi huo ili utekelezwe kwa mafanikio," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ripoti ajali ya ndege yaacha maswali

**Na Romana Mallya**

TAARIFA ya awali ya ripoti ya ajali ya ndege ya Kampuni ya Precision Air, iliyoanguka katika Ziwa Victoria, mkoani Kagera, imeacha maswali huku ikiacha kumtaja kijana mvuvi, Jackson Majaliwa, aliyeonekana shujaa kwa kuokoa watu.

Ripoti hiyo imeonyesha vikosi vya uokoaji vilichelewa kufika katika eneo la tukio bila kumtaja Majaliwa na kazi aliyoifanya hata kuonekana ndiye alikuwa kinara wa suala hilo.

Kutokana na ripoti hiyo iliyotolewa juzi na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ikiwa ni baada ya siku 14 tangu kutokea kwa ajali hiyo, Novemba 6, mwaka huu, katika mitandao ya kijamii, wananchi wamekosoa kwa kutomtaja Shujaa Majaliwa, licha ya kwamba serikali ilimtambua na kumzawadia ikiwamo kumpeleka kwenye chuo cha mafunzo ya uokoaji.

Katika ajali hiyo, Majaliwa alijizolea umaarufu wa kuitwa shujaa, baada ya kitendo chake cha kuokoa baadhi ya manusura wa ajali hiyo na ndipo serikali ilipomzawadia kwenda kusoma mafunzo ya uokozi na kumpa ajira ya kudumu serikalini.

Novemba 7, mwaka huu, wakati wa kuaga miili ya marehemu 19, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alimtangaza Majaliwa kama shujaa na kumzawadia Sh. milioni moja ambayo alikabidhiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Ajali hiyo ilitokea wakati ndege hiyo ikitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Bukoba, ikianguka katika Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya watu 19 na manusura 24.

Ndani ya ripoti hiyo, kuna taarifa kwamba mhudumu wa ndege kwa kushirikiana na abiria ndio walifungua mlango na kuwezesha kuokolewa kwa watu 24. Ripoti hiyo ilisema hadi saa 2:20 asubuhi hali ya hewa Bukoba ilikuwa shwari lakini ilipofika saa 2:25 ilikuta mvua kubwa na radi.

Ilisema ndege hiyo iliendelea kuzunguka kwa dakika 20 kusubiri kuwe shwari na wakati ikianza kutua barabara ya kutua ndege ilikuwa inaonekana.

Ripoti hiyo pia ilisema lengo halikuwa kutua kwenye maji kwa kuwa abiria hawakuambiwa wavue viatu au wavae makoti ya kujiokoa na matairi ya ndege yalifunguka kuashiria ndege ilikuwa tayari kutua uwanjani.

Ilieleza kuwa kilichotokea kilikuwa ghafla, rubani hakuwa amejiandaa nacho na kwamba uokoaji ungefanyika kwa wakati watu wengi zaidi wangeokolewa. Pia ilisema marubani walishindwa kufungua mlango wa chumba chao na ule wa dharura juu ya ndege kutokana na msukumo mkubwa wa maji.

"Wavuvi walifika eneo la tukio takribani dakika tano na waliwachukua manusura kwenye mitumbwi. Boti ya kitengo cha polisi cha majini ilifika saa saba mchana eneo la tukio kwa sababu haikuwa Bandari ya Bukoba ilikuwa inafanya oparesheni zingine.

"Baada ya kufika walikuwa na changamoto ya ukosefu wa oksijeni na mafuta ya kutosha, lakini kabla ya kufika mvuvi mmoja tayari alianza kutoa maiti zilizokuwa ndani ya ndege," ilisema.

Kwa mujibu manusura wa ajali hiyo, ripoti inasema ndege hiyo ilishuka salama, lakini kabla haijakanyaga ardhi ndipo ilibadili uelekeo kwenda upande wa Ziwa Victoria.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa, mhudumu mmoja wa ndege hiyo pamoja na abiria mwingine ndio walihusika kufungua mlango na kwamba baada ya kufunguka, abiria huyo alisimama kuzuia mlango kujifunga ili abiria wengine watoke na kuingia kwenye mitumbwi ya wavuvi.

Ilibainisha kuwa Uwanja wa Ndege wa Bukoba, hauna mnara wa kuongozea ndege na kwamba mawasiliano yote hufanyika kwa kutumia mnara uliopo Mkoa wa Mwanza.

Pia ilisema rubani alijua anatua kwenye njia ya ndege na si kwenye maji na kwamba kuna uwezekano ndege ilisukumwa na upepo kwenda ziwani wakati akijaribu kutua. Aidha, taarifa hiyo ilisema uchunguzi wa kubaini chanzo halisi cha ajali hii bado unaendelea.

## WADAU WAFUNGUKA

Kutokana na ripoti hiyo, wadau mbalimbali wamefunguka huku Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, katika ukurasa wake wa Twitter jana akiandika: "Nimeona taarifa rasmi ya serikali kuhusu ajali ya ndege ya Precision Air iliyotokea Bukoba na kuua watu 19.

"Tuliyeambiwa ni shujaa aliyeokoa si aliyeokoa watu, mhudumu wa ndege na abiria mmoja ambaye hajatajwa kabisa ndiye aliyefungua mlango na kushikilia mlango watu watoke.

"Kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa huduma za uokoaji kwa taarifa kuchelewa kutolewa kwa dakika 15 nzima, meli ya uokoaji kufika eneo la tukio ikiwa imechelewa sana na haikuwa na mafuta wala oksijeni na hivyo kutazama watu wakikata roho."

Mwalimu Philbert Macheyeki Jr, kwa upande wake aliandika kuwa yapo maswali magumu katika ripoti hiyo ambayo yanapaswa kutolewa ufafanuzi.

"Tunamtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ajitokeze na kutoa ufafanuzi wa kina, kuliomba radhi Taifa kwa uzembe na zaidi aone umuhimu wa yeye kuwajibika katika hili," Mwalimu Macheyeki Jr aliandika katika Twitter.


Novemba 14, mwaka huu, Baraza la Mawaziri liliagiza wataalamu wa ndani kushirikiana na wa wataalamu kutoka nje ya nchi kufanya uchunguzi. Baada ya ajali hiyo serikali ilitangaza hatua tatu za kufuatwa kwenye uchunguzi ambazo ni timu ya uchunguzi kufanya uchunguzi na kutoa maelezo yake ndani ya siku 14.



RIPOTI MAALUM

# Mabadiliko ya tabianchi yalivyoathiri upatikanaji huduma ya maji, chakula

- Kisima cha msikiti chaokoa wananchi na mifugo
- Wakulima wakimbia mashamba, wahamia dukani



Wafugaji wa kata ya Paranga, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, wakinywesha maji mifugo huku wananchi wakiwa wamepanga foleni wakisubiri kuchota maji hayo, mapema wiki hii. **PICHA: GWAMAKA ALIPI**

**Na Gwamaka Alipipi, aliyekuwa CHEMBA**

NI mwendo wa takribani dakika 10 kwa kutumia usafiri wa pikipiki kutoka mjini Chemba kukifikia Kijiji cha Paranga kilichoko Kata ya Paranga, Halmashauri ya Chemba mkoani Dodoma.

Kwa muda wote wa safari hiyo fupi kutoka mjini, kinachoshuhudiwa ni nyasi zilizokauka, miti iliyopukutisha majani na ardhi iliyopasuka huku kukiwa na kadhia nyingine ya watoto wanaoswaga punda, wanaovuta mikokoteni iliyosheheni madumu ya maji.

Nipashe inapozungumza na wenyeji, mara moja inabaini kwamba kinachojiri dhidi yao ni matokeo ya athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, shida zilizoyakumba maeneo mengi nchini.

Katika udadisi wake kuhusu undani wa madhila hayo kwa wananchi, Nipashe pia inashuhudia mkusanyiko wa wananchi walioweka foleni ya kuchota maji, huku mifugo nayo ikinyeshwa maji hayo hayo yanayotolewa na msikiti unaoitwa Masjidi Nuru Paranga.

Ikirejewa mipango na mikakati ya kitaifa, kinachoshuhudiwa Chemba kinakinzana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025, inayoelekeza serikali kuhakikisha inapunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Pia ni hali iliyo kinyume cha Sera ya Maji inayotumika kwa sasa nchini, ikiitaka serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi ndani ya mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

**"Sasa nimeamia dukani, kilimo kimekataa kabisa, hakuna mvua wala maji ya kumwagilia mazao. Mwaka mwaka jana sijapata hata debe la mahindi, yote yamepotelea shambani, nilipanda ekari mbili lakini yamepotelea shambani," anasema Walfa, mama wa watoto sita.**

Logo Tuji, mfugaji kutoka Kijiji cha Paranga mwenye mifugo zaidi ya 80 aliyekutwa eneo hilo la kisima cha msikiti akiwa na mifugo yake, anasema: "Hali ni mbaya sana. Isingekuwa msikiti huu, sijui tungenywesha nini mifugo yetu. Kama unavyotuona hapa, tunaweka foleni kupata huduma, jua linawaka sana, hakuna mvua."

Shakira Ramadhani, mama wa watoto wanne na mkazi wa Kata ya Paranga, ambaye alikutwa na Nipashe kisimani huko, akisubiri mifugo imalize kunywa ndipo achote maji, anasema analazimika kuweka foleni na mifugo kwa sababu hakuna sehemu nyingine anayoweza kupata maji kwa ajili ya matumizi ya familia yake.

"Ukitaka kuyafuata maji inakupasa uamke alfajiri sana, utembee umbali wa kilometa 10. Ukirudi unachoka sana na majukumu mengine ya familia yanakusubiri, hivyo kuepukana na adha hiyo tunalazimika kuweka foleni na mifugo," anasema Shakira.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Kuruthumu Skana anasema uhaba wa mvua umemwathiri kiuchumi kwa kuwa ameshindwa kuzalisha chakula kwa ajili ya familia yake.

Anasema hali hiyo imemlazimu ajishughulishe na upondaji wa kokoto, mwenyewe akizipa jina la 'karasha'. Pia anasema amelazimika kufanya vibarua sehemu mbalimbali ili kupata fedha kwa ajili ya kulisha familia katika kipindi hiki cha ukame.

"Mimi ni mkulima wa mahindi na alizeti, mwaka huu sijaambulia chochote. Nilipanda Januari mwishoni lakini mazao yameishia katikati. Maji nayo hakuna, ukiagiza dumu la lita 20 gharama yake ni Sh. 250. Ni gharama kubwa sana huku kwetu maana maisha yetu kama unavyoona ya kuungaunga," Kuruthumu analalama.

Mkazi mwingine Maria Loyababu anaendelea kusimulia kinachowasibu kipindi hiki, akitamka: "Upatikanaji wa chakula na maji ni wa tabu sana mwaka huu, jua linawaka sana, ukame umeongezeka, huwa ninalima ekari moja ya mahindi lakini yamekauka.

"Nina watoto saba. Ninaomba serikali itupatie msaada wa chakula au kutuuzia kwa bei nafuu zaidi ili hata sisi tuliomo kwenye TASAF (Mpango wa Maendeleo) tumudu kukinunua".

Mkuu wa kaya hiyo, Damian Kolo anasema ugumu wa kupata maji na chakula unamkwamisha kufanya shughuli zingine za maendeleo.

"Kwa sasa tunatumia muda mwingi kusaka maji badala ya kujikita kwenye shughuli zingine za maendeleo. Tunafikia hatua ya kutooga hata kwa siku mbili hadi tatu maana upatikanaji wa maji ni mgumu," anafafanua.

Mmoja wa wakulima wa kijiji hicho, Walfa Salum anasema amelazimika kuachana na kilimo na kufungua duka la bidhaa za matumizi ya nyumbani baada ya kulima msimu uliopita na kuambulia patupu kwenye mavuno.

"Sasa nimeamia dukani, kilimo kimekataa kabisa, hakuna mvua wala maji ya kumwagilia mazao. Mwaka mwaka jana sijapata hata debe la mahindi, yote yamepotelea shambani, nilipanda ekari mbili lakini yamepotelea shambani," anasema Walfa, mama wa watoto sita.

Moshi Ali, mkulima wa mpunga, anasema ukame wa mwaka huu umesababisha kutopata hata debe la mpunga.

"Uhaba wa mvua ni tatizo, maji ya RUWASA (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini) nayo ni tatizo, njaa inatunyemelea. Wakulima hatujavuna kitu msimu uliopita, mwaka huu kama unavyoona jua linawaka, mvua tulitarajia inyeshe kuanzia mwanzoni mwa Novemba lakini hadi leo (Novemba 12, mwaka huu) hakuna kitu, uzalishaji wa chakula umepungua," anasema.

Diwani wa Makorongo, Petro Mollel anakiri kuwapo tatizo la uhaba wa maji na chakula katika eneo lake la utawala lililosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Anaiomba serikali kufanya alichokiita kuiangalia kwa jicho la tatu hali hiyo kwa kuwa wananchi wengi katika kata yake wameshindwa kuvuna mazao kutokana na uhaba wa mvua.

Anataja hatua anazoona zinatakiwa kuchukuliwa na serikali kipindi hiki ni pamoja kuwapelekea maji wananchi kutoka vyanzo vingine vya maji na kuwapatia chakula cha bei nafuu, hatua ambazo serikali imezichukua katika maeneo mengi yaliyoathiriwa na ukame, zikiwamo Halmashauri za Longido na Monduli mkoani Arusha.

*ITAENDELEA KESHO

TANGAZO

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITIES

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line with its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the positions mentioned below:-

## 1. POSITION: DIRECTOR OF TECHNICAL SERVICES – (1 POST)

### 1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have a Degree in Aeronautics / Degree in relevant engineering field from a recognized institution or its equivalent
- Must have Aircraft Maintenance Engineer's license/approval with appropriate airframe, power plant or avionics ratings;
- Must have at least ten (10) years of working experience of which two (2) years must be in a Managerial position: and
- Must have at least three years' experience in maintaining the same category and class of aircraft used by the AOC holder including one year in the capacity of returning aircraft to service.

### 1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Advises the Managing Director and CEO on all matters related to Technical Services activities to contribute in reaching of the vision and realizing the mission of the Company.
- Provide leadership and coordination of Technical Services sections to ensure legal, safe and efficient operation.
- Responsible for development, implementation, and evaluation of strategies to achieve technical services' corporate objectives
- Development and enforcement of company policies and for ensuring compliance with all laws, rules, and regulations governing technical services activities.
- Oversee the planning and optimum use of resources under technical services section.
- Ensure that the highest possible standards of Technical proficiency are maintained
- Oversees and implements ATCL's strategic plan in relation to Technical Services directorate objectives;
- Ensure optimal, efficient and effective management and utilization of human resource under Technical Services directorate
- Oversee the planning and optimum use of resources under the Technical Services directorate
- Ensure implementation of an effective quality and determine standards operating practices to comply with relevant legislations and regulations which are related to the AOC and other necessary authorities
- Liaise with other departments within the airline to ensure the airline global objectives and targets are met.
- Oversee health and Safety Matters
- Conducts Performance Review and Appraisal of subordinates and gives feedback respectively.
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

## 2. POSITION: ADMINISTRATIVE MANAGER – (1 POST)

### 2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have a Master Degree in one of the following fields: Public Administration, Human Resources Management, Human Resources Planning and Management, Sociology, Industrial Relations, Business Administration/Commerce majoring in Human Resources Management or related qualification from recognized institutions
- Must have a Bachelor Degree in Public Administration, Human Resources Management, Human Resources Planning and Management, Sociology, Industrial Relations, Business Administration/Commerce majoring in Human Resources Management or related qualification from recognized institutions
- Must have at least eight (8) years of working experience in relevant field and must be in Senior Officer position
- The candidate must have successfully passed Qualifying Law Examinations for Administrative Officers.

### 2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Advises the Director of Human Resources and administration on administrative matters in ATCL.
- Manages the general upkeep of services to include maintenance of office equipment, water and sewerage, office environment cleanness, buildings, Vehicles and grounds including other outsourced services
- Leads the compliance of OSHA guidelines ensuring all locations are compliant with zero tolerance on non-compliance
- Develops, implements and reviews internal administrative procedures specifically with the guiding SOP to enhance administration controls
- Provides requisite link with the PMU for all departmental administrative procurement, ensuring all works and services are planned and executed as per APP and Departmental business plan.
- Manages ATCL security and out sourced security services to ensure ATCL property is well protected
- Conducts Performance Review and Appraisal of subordinates and gives feedback
- Supervises and ensures efficient system of central registry is operational to speed up correspondences between various department and with external parties.
- Manages proper allocation of physical assets such office equipment and furniture and keep current record of users to enable management to plan internal usage efficiently.
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

## 3. POSITION: ACCOUNTANT II (1 POST)

### 3.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

Must have Bachelor Degree or Advanced Diploma in one of the following fields; Accountancy, Finance, Business Administration/Commerce majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from recognized Institutions plus either of CPA (T), ACCA, ACA, CIMA or equivalent professional qualification recognized by the NBAA.

### 3.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Collect cash and cheques and pay authorized petty cash.
- Reconcile cash balance
- Prepare revenue and expenditure reports.
- Prepare accounts documentation
- Dispatch voucher lists to Head of sections.
- Make batching of payment vouchers as per Cashbook
- Maintain Petty Cashbook and Register
- Carrying out regular bank reconciliation.
- Record financial transactions in the accounting system.
- Performs any other official duties as may be assigned by the supervisor

## 4. POSITION: RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT II (2 POSTS)

### 4.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

Must have Certificate in one of the following fields: Records Management, Records and Archives Management, Corporate Information Management, or equivalent qualification from recognized institutions.

### 4.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Assist in receiving all incoming mail/documents.
- Record all incoming mail /documents.
- Post or dispatch outgoing mail/documents.
- Handle all files movements and records.
- Perform any other official duties as provided by the supervisor.

## 5. TERMS AND CONDITIONS:

Five (5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 6. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following;

i. A curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA);
iii. Two recent passport size photographs ;
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicants from Public Service should route their applications through their employers;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note:** Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.

## 7. CLOSING DATES:

Applications should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM**
**Issued on: 24th November, 2022**

17182702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka wanaume kuripoti ukatili wanaofanyiwa

**WAZIRI** wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, juzi alisema kutokana na kuwapo kwa matukio ya wanaume kufanyiwa vitendo vya ukatili na wenza wao, serikali imeanzisha mfumo utakaowawezesha kutoa taarifa pindi wanapofanyikwa unyama huo.

Hatua hiyo inatokana na wanaume hao kutokutoa taarifa, hivyo kuamua kukaa nayo moyoni na matokeo yake, matukio ya uhalifu yakiwamo mauaji ya wenzi kuongezeka siku hadi siku. Kutokana na kukithiri kwa hilo, serikali imeweka mfumo saidizi ngazi zote zikiwamo madawati ya jinsia, ili wanaume wawe huru kujitokeza badala ya kuendelea kufanya matukio makubwa ndani ya jamii.

Waziri alibainisha kuwa wanaume wengi hawapendi kutoa taarifa wanapofanyiwa ukatili wanaishia kuvumilia na kwamba wapo wanaotendewa ukatili mkubwa lakini wanaamua kunyamaza. Sambamba na kutoa taarifa, aliwashauri wanaume kutengeneza mitandao yao ili wawe na sauti moja kama wanawake wanavyofanya na sauti zao zinakuwa kubwa.

Dk. Gwajima alisema kuna chama cha kutetea haki za wanaume dhidi ya matendo wanayofanyiwa na wenzi wao lakini hakitumiki ipasavyo kutokana na waanzilishi kupigwa vita na wenzao.

Hata hivyo, baadhi ya wanaume wamejitokeza hadharani na kueleza madhila wanayokutana nayo na kuomba jamii iwasaidie huku wengine wakiishia kuvumilia na wengine kulipiza kwa kufanya matukio ya hatari ambayo yamegharimu maisha ya wake zao.

Kwa sasa matukio ya mauaji ya wapenzi au wanandoa yameongezeka ikiwa ni wastani wa tukio moja hadi mawili kila siku na mengi ni mwanaume kaamua kumuua, kumjeruhi mwenza huku sababu kubwa ikielezwa ni wivu wakimapenzi.

Wakati wanaume wakiwa hivyo, wanawake wamekuwa wepesi kusema na wengine kukimbilia vyombo vya sheria ili kupata haki zao. Hulka ya wanaume kujifanya watu wa kumeza (kunyamaza) na kuvumilia, huku wakiogopa kudharauliwa wakiripoti matukio hayo, ndiyo imezidisha kasi ya mauaji katika jamii.


Wengine huhofia kuonekana wamezidiwa nguvu na wake zao au wametawaliwa kwa kiasi ambacho hawawezi kuamua maisha yao ya kila siku, hivyo kukumbana na kebehi kuwa huenda hawana uwezo wa kipato.

Hakuna ubishi kwamba tangu enzi na enzi mwanamume amejengwa kwamba anapaswa kuwa jasiri, lakini kuendelea kuendekeza kasumba hiyo, ndivyo ambavyo matukio ya ukatili yameendelea kutamalaki katika jamii. Kwa wanaume walioshindwa kuvumilia, wamezikimbia familia hatua ambayo pia imesababisha mateso kwa watoto kwa kulelewa na mzazi mmoja au kujiingiza katika makundi ya uovu.

Pamoja na hayo, kutokana na mabadiliko ya kimfumo duniani, jamii inapaswa kubadilika na kupendana na kwa kufanya hivyo, kutakuwa na amani huku wanawake na wanaume wakiishi kwa amani.

Hata hivyo, kama alivyosema Waziri, wakati umefika sasa kwa wanaume kupaza sauti zao juu ya mambo wanayofanyiwa na wake zao hasa ukatili kwa kupigwa na hata kupata ulemavu wa kudumu. Kwa kufanya hivyo, watapunguza ukatili unaoendelea katika jamii pamoja na matatizo ya kiafya kama vile msongo wa mawazo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Onyo hili lilete matokeo chanya matumizi sahihi ya antibaiotiki

Na Sabato Kasika

**ANTIBAIOTIKI** ni dawa zitajwa kusababisha usugu katika mwili wa mtumiaji na hata wakati zinaweza kumletea madhara makubwa, ikiwamo kupoteza maisha iwapo atatumia bila maelekezo ya madaktari.

Kutokana na hali hiyo, serikali imekuwa ikitoa tahadhari mara kwa mara kwa kuitaka jamii kuacha mtindo wa matumizi holela ya antibiotiki, ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

Tahadhari hiyo inatolewa kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya watu wamekuwa na kawaida ya kukimbilia katika maduka ya dawa na kununua na kuanza kutumia wanapojisikia vibaya.

Utaratibu huo unakwenda kinyume, kwa kuwa inaelekezwa kuwa mtu anapojisikia kuumwa, aende kwa wataalamu wa afya apate ushauri utakaomwezesha kupata dawa sahihi za kumtibu.

Lakini bahati mbaya, miongoni mwa dawa ambazo watu wamekuwa wakinunua bila ushauri wa wataalamu wa afya ni antibaiotiki ambazo, jamii imekuwa ikishauri kutozitumia bila kupata ushauri wa madaktari.

Inaelezwa kwamba, sababu kubwa ya bakteria kuwa sugu kwenye antibiotiki, ni matumizi makubwa kupita kiasi au matumizi yasiyo sahihi, kwamba mengi kwa dawa hizo si ya lazima.

Ninadhaani kuwapo kwa dawa hizo kwenye maduka mengi, isiwe sababu ya watu kuamua kwenda kuzinunua tu bila kupata ushauri wa kitaalamu unaowawezesha kupata vipimo sahihi kabla ya kununua na kumeza au kunywa.

Kwa kuwa inashauriwa kwamba matumizi ya antibaiotiki ni kwa ajili ya maambukizi ya bakteria tu na kwamba mtu asiitumie kwa changamoto zinazosababishwa na virusi kama mafua, koo kuwasha au kikohozi.

Hivyo, ni muhimu kuzingatia hilo na kuepuka pia matumizi ya dozi tofauti, kuvusha dozi au kutumia kwa muda mrefu zaidi, kwa kuwa kitendo hicho kinasababisha usugu wa dawa, hata kama mtu atajisikia vizuri baada ya siku chache, asiache kumeza dawa ulizopatiwa.

Bahati mbaya imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya watu kufanya hivyo, huku wengine wakaitumia dozi ya dawa walizoandikiwa wengine au dawa zilizobaki hapo awali, kwani pia ni kujisababishia usugu.

Kwa kuwa matumizi holela ya antibiotiki, yanaifanya serikali kutoa maelekezo kila mara kwa kuwataka Watanzania kuwa makini, badala ya kujisikia kuumwa na kwenda kununua dawa, ni vyema kila mmoja kuchukua hatua.

Ni juzi tu serikali imetahadharisha matumizi mabaya ya dawa za antibaiotiki ambazo zinasababisha usugu wa vimelea dhidi ya dawa, ikionya hatari ya kutokea madhara makubwa hasa kifo kwa watumiaji.

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu, anasema jijini Dar es Salaam kuwa takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 92 ya antibiotiki zinatumika nchini zimesababisha usugu kwa asilimia 59.8.

Si mara ya kwanza kwa serikali kutoa onyo kwa Watanzania kuhusu matumizi holela na dawa hizo, kwani mwaka 2018, ilionya, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuchukua hatua zitakazomfanya awe salama dhidi ya antibiotiki.

Mwaka huo wakati akizindua Mwongozo wa Matibabu nchini na orodha ya taifa ya matumizi ya sawa muhimu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akatahadharisha kuhusu matumizi ya antibiotiki.

Kwamba, antibiotiki zitatumika katika ngazi ya hospitali za rufani za kanda, hospitali ya taifa na hospitali maalum, lakini zinauzwa latika maduka ya dawa, huku watu wakinunua na kutumia bila ushauri wa madaktari.

Kitendo cha baadhi ya watu kutumia bila ushauri wa madaktari, maana yake ni kujitafutia madhara kikiwamo kifo kama ambavyo wizara ya afya inatahadharisha umma wa Watanzania.

HABARI KITAIFA

# Jitihada za Rais Samia Msimbazi zazaa matunda

**Na Mwandishi Wetu**

JITIHADA za Rais Samia Suluhu Hassan, tangu akiwa Makamu wa Rais kuhusu uendelezaji bonde la Mto Msimbazi kwa kuwasaidia wananchi waondokane na adha ya mafuriko na hasara ya kupoteza maisha na mali, zimezaa matunda.

Juzi, Benki ya Dunia (WB), ilitangaza kutoa mkopo wa bei nafuu wa Sh. trilioni 1.24 kwa ajili ya mradi wa uendelezaji wa bonde la Msimbazi na kusambaza umeme vijiji, na mkataba wa makubaliano ulisainiwa Novemba 21, mwaka huu.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza baada kutia saini makubaliano hayo, alisema fedha hizo zitasaidia nchi kupiga hatua kubwa kiuchumi na kwamba Dola za Marekani milioni 200 zitatumika kuboresha eneo la Jangwani kwa kujenga daraja na kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam.

Alisema kwa maagizo ya Rais Samia, wamefanya majadiliano ya haraka na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kusaini mikataba na kutekeleza miradi ya maendeleo. Alisema mradi huo unatarajiwa kutoa suluhisho ya muda mrefu la mafuriko yanayotokea kila mara mvua inaponyesha eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam.

"Mradi huu ni jitihada za muda mrefu za Rais Samia tokea mnamo mwaka 2017 wakati bado ni Makamu wa Rais," alisema.

Januari, 2018, Samia akiwa Makamu wa Rais, aliitisha mkutano wa kutafuta suluhisho la mafuriko ya mara kwa mara yanayolikumba Jiji la Dar es Salaam, na kiliundwa kikosi kazi kuratibu jitihada za serikali na kutoa mwongozo wiki siku zijazo kwa eneo hilo.

Mchakato huu uliojulikana kama 'Msimbazi Basin Charattee' ulianza kwa kupitia hatua mbalimbali na kuratibiwa ofisi ya Rais chini ya Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Ripoti ya WB inasema maboresho ya eneo hilo imeeleza mradi huo utahusisha hekari 57, makazi 14,500, maeneo ya bishara yatakayotumiwa na sekta binafsi, serikali na wadau wa maendeleo kwa kuligeuza eneo hilo kutoka kuwa la mafuriko hadi lenye thamani ya kuboresha uchumi wa watu.

Aidha, ripoti hiyo ilibainisha kuwa kulingana na makadirio ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kiuchumi ndani ya Bonde la Msimbazi, mtaji wa kuendeleza eneo hilo utarejeshwa kwa miaka 12.

Ripoti hiyo inayotambulika kama 'Msimbazi Opportunity', ililenga kutoa mrejesho wa maelekezo ya Makamu wa Rais mwaka 2017.

Mradi huo ulitengenezwa na wadau mbalimbali wa mradi wa Msimbazi kwa kipindi hicho, Januari mpaka Agosti 2018, na kwamba maendeleo ya mpango wa mradi ni matokeo ya jitihada ya timu ya zaidi ya watu 200 kutoka taasisi 59 pamoja na jamii kutoka vitengo vyote vya kazi.

Taarifa ya TAMISEMI ilisema hatua za awali za mradi huu wa Msimbazi, wadau walioshirikishwa ni kutoka ngazi za juu kabisa za serikali mpaka ngazi za chini za jamii, kuanzia asasi za kijamii mpaka sekta binafsi.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Rogatus Mativila, alisema wamepata zaidi ya Sh. bilioni 145 kupitia mradi huo, kwa ajili ya kujenga daraja la juu kuzuia mafuriko na wataanza baada kupatikana kwa mkandarasi kuanzia mwezi wa nne 2023.

Alisema TANROADS itajenga daraja hilo kwa miaka miwili hadi mitatu lenye urefu wa mita 390 na litanyanyuka juu kwa mita sita na kusaidia kutofikiwa tena na mafuriko ya maji.

Pia watajenga kingo za Mto Msimbazi za kilomita 1.8 kwenda juu na Kilomita 1.8 kushuka chini kwa kuchimba mchanga ambao pia utasaidia katika shughuli za ujenzi.

Walioshiriki mpango wa Bonde la Msimbazi ni Mkoa wa Dar es Salaam, Baraza la Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Ubungo, DART, DAWASA, DAWASCO, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Ujenzi, Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Ofisi ya Waziri Mkuu - Kitengo cha Maafa, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

## Mwalimu auawa akidhaniwa mwizi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ALIYEKUWA Mwalimu wa Shule ya Msingi Livingstone, Erick Mbilinyi, mkazi wa mtaa wa Mgendela katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ameuawa na wananchi wenye hasira kali kwa madai ni mwizi.

Tukio hilo lilitokea Novemba 20, mwaka huu majira ya saa 10:00 jioni katika eneo la Shule ya Msingi Selestini iliyoko mtaa wa Joshoni, baada ya wananchi hao kumwita mwizi. Inadaiwa kuwa alikutwa na umauti baada ya kuingia katika moja ya nyumba mjini hapa

Baadhi ya waombolezaji, walisema wakati wa mazishi ya mwalimu huyo katika makaburi yaliyopo katika mtaa wa Maheve, majirani wa karibu na Mbilinyi, akiwamo Mwalimu Robustus Mtala, walisema wamehuzunishwa na kitendo cha kujichukulia sheria mkononi kilichofanywa na baadhi ya wananchi bila kujiridhisha zaidi kwa kuwa hakuwa na tabia za ajabu.

Ofisa Tarafa wa Njombe Mjini, Lillian Nyemele, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alionya wananchi kujichukulia sheria mkononi.

"Tulipokea taarifa hizi zenye huzuni Jumapili usiku. Tukio hili lisijirudie tena kwa kuwa inasikitisha mno mwalimu kuuawa bila hatia. Polisi kata wamekuwa wakitoa elimu kupitia mikutano yetu nini cha kufanya juu ya mtu unayemtilia mashaka. Hiyo hapana, niwaombe sana tuwe watulivu kwa kipindi hiki tunachokipitia," alisema Nyemele.

Inadaiwa kuwa marehemu huyo alikuwa na tatizo la akili hali ambayo ilikuwa ikimtokea mara kwa mara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi unaendelea.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mama G Inv. Filling Station, S.L.P 188, Kiteto. | Kijiji cha Kimana, Kata ya Partimbo, Kiteto, Manyara. | Benjamin Eliakim Mrema (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Elon and sons Limited, S.L.P 509, Babati – Manyara | Kiwanja Na. 19, Kitalu "EE", Babati, Manyara. | Msama Kosani Msama (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 3. | Olasiti Investment Co. Ltd, S.L.P 10275, Simanjiro – Manyara. | Kijiji cha Naberera, Kata ya Terati, Simanjiro , Manyara | Innocent Simon Moshi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | Emmanuel Munisi Angasa T/A Ebanow Investment – Msitu wa Tembo Petrol station, S.L.P 5102, Manyara. | Kijiji cha Msitu wa Tembo, Simanjiro, Manyara | Emmanuel Angasa Munisi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Sabri Ahmed Said, S.L.P 90499, Dar es Salaam. | Kijiji cha Muungano, Kata ya Msanja, Kilindi, Tanga. | Sabri Ahmed Said (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Adolph Misael Lyakundi, S.L.P 39, Songe – Kilindi, | Kiwanja Na. 16, Kitalu "A" , Eneo la Songe Mjini, Kilindi, Tanga | Adolph Misael Lyakundi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Star Oil Tanzania Limited – Kwasadala Petrol station, S.L.P 5005, Hai – Kilimanjaro. | Kiwanja Na. 1, Eneo la kwa sadala, Hai, Kilimanjaro. | Murtaza Ali-Hussein Fazal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 8. | Ally Abdallah Talib, S.L.P 438, Arusha. | Kiwanja namba 131, Kitalu "A", Eneo la Engare - Olmotonyi, Arumeru, Arusha | Ally Abdallah Talib (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 9. | Tabora Amazon Service Station, S.L.P 155, Tabora. | Kiwanja No. 89, Kitalu "DD', Mtaa wa Lumumba, Tabora | Hanif Bhaloo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 10. | Amazon Service Station, S.L.P 155, Tabora. | Kiwanja No. "Agip Service Station", Kitalu "DD", Mtaa wa Lumumba, Tabora | Hanif Bhaloo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 11. | Malekia Filling Station S.L.P. 198, Morogoro. | Kijiji cha Kichangani, Eneo la Komnyiga, Mvomero, Morogoro. | Erondy Elikana Malekia ( Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 12. | Refuelling Solution (T) Limited - Ifakara Branch, S.L.P. 5421, Morogoro. | Kiwanja Na. B Kitalu "D", Eneo la Ifakara, Kilombero, Morogoro. | Mohsin Bharwani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 13. | Puma Visiga Services Station, S.L.P. 9043, Pwani. | Kiwanja Na.54/3, Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Dominic Dhanah (Mzimbabwe) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 14. | Ashura Athumani Ditopile T/A King Fahad -Mwasonga Filling Station, S.L.P 6613, Dar es Salaam | Kiwanja Na. P15501, Eneo la Mwasonga, Kigamboni, Dar es Salaam. | Ashura Athuman Ditopile (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Rupeez Oil, S.L.P. 84, Dar Es Slaam. | Eneo la Kimara Stop Over, Ubungo, Dar es Salaam. | Elias Henry Rupia (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | Refuelling Solution (T) Limited - Dodoma Branch, S.L.P. 5421, Morogoro. | Kiwanja Na. 37 Kitalu "B", Eneo la Kisasa - Ilazo, Dodoma mjini. | Mohsin Bharwani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Tilu Amos Nsimba, S. L. P. 1006, Katoro - Geita | Kiwanja Na.180, Kitalu "A", Eneo la Bugayambalehe "A", Wilaya ya Geita, Mkoa wa Mwanza | Tilu Amos Nsimba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Fuel Master (T) Limited, S.L.P. 305, Kigoma | Eneo la Kitonga, Manispaa ya Kigoma-Ujiji, Mkoa wa Kigoma | Bera Andrew Karumba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | NGS Petroleum Limited, S.L.P. 20, Bariadi | Kiwanja Na.110, Kitalu "G", Eneo la Bariadi Mjini, Wilaya ya Bariadi, Mkoa wa Simiyu | Njalu Daudi Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Mount Meru Petroleum Limited, S.L.P. 7094, Arusha. | Kijiji cha Nyamuswa, Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Silasi Mayunga Masalu T/A Vatcan Investment, S.L.P. 170, Bukombe. | Kiwanja Na.1, Kitalu "D", Eneo la Bwanga, Wilaya ya Chato, Mkoa wa Geita | Silasi Mayunga Masalu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Som Petroleum (T) Limited, S.L.P. 45053, Dar es Salaam | Kiwanja Na.15, Kitalu "B", Eneo la Mutukula Trading Centre, Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera | Abdallah Hassan Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Remigius Patrick Nshange, S.L.P. 881, Bukoba | Kijiji cha Katoro, Kata ya Katoro Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mkoa wa Kagera | Remigius Patrick Nshange (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Julius Marko Wambura, S.L.P. 403, Tarime | Kiwanja Na.1736, Kitalu "A", Eneo la Kewanja, Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara | Julius Marko Wambura (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Ochele Service Station, S.L.P. 250, Rorya | Kiwanja Na.2&4, Kitalu "A", Eneo la Kanyama, Wilaya ya Magu, Mkoa wa Mwanza | Charles Ochele Obutu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Petroafrica (T) Limited, S.L.P. 4878, Dar es salaam | Kiwanja Na.75, Kitalu "B", Eneo la Kahama Mjini, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga | Yasin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Mexons Energy Limited-New Maendeleo Service Station, S.L.P 506, Njombe | Kiwanja Na.7 na 8, Kitalu "E", Eneo la Njombe Mjini, Wilaya ya Njombe Mjini, Mkoa wa Njombe | Mexon Jephta Sanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

17163301

# Shaka: Kasi ya Samia imewatoa pangoni

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, imewatoa nyoka pangoni kuja kuota jua la maendeleo.

Amesema kipaji cha uongozi cha Rais Samia ni chachu ya maendeleo endelevu, huku ubunifu wake ukileta ari mpya ya kusukuma maendeleo ya nchi.

Shaka alisema hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini hapo, ukiwa sehemu za shughuli za Rais Samia akikamilisha siku ya pili ya ziara yake mkoani Manyara.

"Mheshimiwa Rais (Samia) na Watanzania msishangae kwa mambo makubwa yanayofanyika nyoka aliyeko pangoni atakuja juu, atakuja juu kutafuta jua ili akauke na kupata matumaini. Mambo makubwa anayoyafanya Rais Samia ameua ndoto, ameua matumaini ya watu. Ndiyo imekwisha hiyo tena, tuombe uhai na uzima, tunaye (Rais Samia) kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, umoja wetu na mshikamano wetu habari 2030 penye uhai," alisema.

Shaka alisema Rais Samia ni kioo kinachoakisi utu na thamani ya Watanzania, huku kipaji chake cha siasa na uongozi imekuwa chachu ya maendeleo na kwamba ubunifu wa Rais Samia umeleta ari mpya ya kusukuma maendeleo katika nchi, hivyo Watanzania waendelee kumuunga mkono.

"Ndugu zangu mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, Rais Samia umeleta mageuzi makubwa katika nchi hii. Hatukuwa na mazoea kukaa kwenye mikutano hii... jamani nini mnachokitaka," alisema huku akibainisha kuwa chama kinaridhishwa na kazi nzuri inayotekelezwa na Rais Samia katika kuwatumikia wananchi.

"Kwa Chama ni faraja na matumaini makubwa kwamba kumbe Rais wetu mambo yake si mabaya, mambo yake ni mazuri sana,"

Hata hivyo, Shaka alisisitiza kuheshimiwa na kuenziwa kwa utamaduni wa kupongeza pale kiongozi anapofanya vizuri na kukosoa kwa heshima na staha pale mambo yanapokuwa hayakwenda sawa.

"Tukajikumbusha utamaduni wa Waafrika, pia tukajikumbushe utamaduni wa Watanzania tangu enzi za uhai wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, utamaduni wetu Watanzania ukifanya vizuri unapongezwa, unapewa shukurani na unatiwa moyo ili ufanye vizuri zaidi, lakini utamaduni wetu pale ambapo hufanyi vizuri au mambo hayaendi vizuri Watanzania tumekuwa na utaratibu mzuri wa kukosoana kwa staha na heshima," alisema.

# Kigogo CUF atimkia CCM

**Na Boniface Gideon,** TANGA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimepata pigo, baada ya Mwenyekiti wa chama hicho Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Jamal Salehe, kutimkia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Amesema amechukua uamuzi huo kutokana na kuvutiwa na ushawishi wa kisiasa alio nao Mwenyekiti mpya wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajab Abdallah.

Jamali alitangaza kujiuzulu wadhifa huo juzi jijini hapa na kuomba kujiunga na CCM, wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa ngazi ya mkoa ambao ulimchagua Rajab, ambaye ni mkulima wa nazi wa wilaya ya Pangani.

Akitangaza uamuzi wake wa kujivua haki zote kama mwanachama wa CUF na kisha kujiuzulu, Jamal alisema: "Nilimwahidi ndugu yangu Rajabu kwamba endapo atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, basi mimi nitahamia CCM. Leo (juzi) nimeamua nitimize dhamira yangu na kuanza kumuunga mkono. Naomba mnipokee ndugu zangu kwa sababu nimekuja kuongeza nguvu."

Akiwa CUF, aligombea ubunge katika Jimbo la Pangani wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2020 na kuangushwa na mbunge wa sasa, Jumaa Aweso, ambaye pia ni Waziri wa Maji.

Kiongozi huyo wa CUF, inaelezwa kwamba alikuwa mwanasiasa wa upinzani mwenye ushawishi mkubwa ndani na nje ya CUF. Ameiongoza CUF kwa miaka 15 akiwa Mwenyekiti wa Wilaya ya Pangani.

Wakati Jamal akiwa ametangaza kujiuzulu nafasi hiyo, mpaka sasa hakuna taarifa yoyote ya Chama Cha Wananchi (CUF), iliyotolewa kuzungumzia uamuzi wa aliyekuwa Mwenyekiti wao kuondoka.

Jamal, anakuwa kiongozi wa pili mwenye ushawishi ndani ya CUF, kujiuzulu na kuondoka baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CUF wa Wilaya ya Tanga, Rashid Jumbe, kukihama na kutimkia Chama Kikuu cha Upinzani nchini, CHADEMA.

Katika uchaguzi wa CCM, ngazi ya Mkoa wa Tanga, Rajab aliwabwaga washindani wake na kuwa mwenyekiti mpya wa CCM mkoani hapa baada ya kupata kura 1,340, akifuatiwa na Derrick Kazoba aliyepata kura 29 na Mathias Mkingwa aliyeambulia kura tisa.


KNAUF

## PUBLIC TENDER NOTICE

## TENDER NO: MKURANGA II 3652 CONSTRUCTION SERVICE IN DESIGN AND BUILD (EXTENSION) OF EXISTING PLASTERBOARD PRODUCTION LINE.

Knauf international is one of the world's leading manufacturers of modern insulation materials, drylining systems, plasters, thermal insulation composite systems, paints, floor screed, floor systems, construction equipment, tools, and other accessories. Knauf has more than 300 production facilities, with sales organizations in over 90 countries, 40,000 employees worldwide.

**Knauf Gypsum Tanzania Limited** being a part of Knauf international produces German quality drywall products using locally sourced materials. **Knauf Tanzania** is going to extend its plasterboard production line, located at Kisemvule, Mkuranga, Tanzania, from the manufacturing capacity of **15 million square to 40.5 million square.**

**The Company do hereby** invite competitive, reliable, well performing, experienced and eligible **Local Contractors** to tender for the construction service in **Design and Build** of its plasterboard production line based on the description and pre – qualification criteria provided in the table below.

**Description and pre – qualification criteria**

| No | Reference number | Description of work | Pre-qualification criteria |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkuranga II 3652 | • Extension of current plant building' <br>• New raw material stock area <br>• New parking area including internal roads. <br>• New social building | Civil and Building works Contractor Class 1 |

If your company meets the pre – qualification criteria you may obtain information from the Procurement & Logistics department at Knauf HQ offices, **Plot 17 Block 186030 14110 • Off Kinondoni Road • Mwindu Lane street, Dar es salaam** from 10:00AM to 16:00PM weekdays only.

A complete set of Tender Documents in English which include tender rules, terms and conditions will be available for physical collection at a fee of Tshs. 100,000/=. Funds must be deposited to the below bank details; (ensure your company details are clearly indicated on the deposit slip when collecting the tender documents for record and reference)

| BANK DETAILS | |
|---|---|
| Bank Name: | CRDB Bank Tanzania Ltd |
| Account Name: | **KNAUF GYPSUM TANZANIA LTD** |
| Account Number | **0150440243800** |
| Branch | Oysterbay Branch |

Submission deadline is **14th December 2022,** Late tenders, partial submission will not be considered.

**ENQUIRIES: Magretha.VanDerMerwe@knauf.com**

**NB: This tender advert does not entail any commitment on the part of Knauf to any applicant. Knauf reserves the right to accept or reject any or all applications without incurring any obligation to inform the applicant (s) of the grounds.**

2171630 01

## Wanafunzi sayansi wapewa mbinu mpya

**Na Devota Mwachang'a**

KATIKA kuhamasisha na kuwaandaa wanafunzi wapende masomo ya sayansi, Kampuni ya Baobab Shalom imezindua Jarida la Sayansi ili kuwawezesha watoto kuwa na uwezo wa kuchunguza, kukusanya taarifa na kuzikabili changamoto za dunia zilizoko nje ya shule.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo wa jarida hilo liitwalo "OYLA Africa Magazine" jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa OYLA Africa, Godfrey Lugalambi, alisema litamwandaa mtoto na mzazi nje ya maisha ya shule kuongeza ujuzi katika kukusanya taarifa na kutafiti majibu sahihi, hivyo kufanya uamuzi binafsi pevu na wenye uhuru.

"Hili ni jarida bora kabisa na la kwanza la kisayansi kwa Tanzania na Afrika yote. Ni chapisho la kila mwezi maalum kwa wanafunzi na wazazi na limesheheni uchambuzi wa kisayansi, hisabati, fizikia na TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)," alisema.

"Tukiwa ulimwengu wa digitali tumeamua makusudi kulichapisha jarida hili kwa njia ya karatasi, hivyo kumrahisishia msomaji asilazimike kutumia intaneti au vifaa vya aina nyingine kupata taarifa," aliongeza.

Naye Mkurugenzi OYLA Africa, Yevgemiy Semikov, alisema jarida hili linaweza kusomwa na familia nzima, kuazimwa na marafiki na kutolewa kama zawadi kwa maktaba za shule.

"Jitihada zetu zinalenga kumwongezea mtoto maarifa na pia kuhakikisha inafikia walengwa wote si shule tu za mjini lakini hata za vijijini.

"Tunatoa wito kwa wadau kuunga mkono jitihada hizo ikiwamo kupata nakala ya jarida na kuendelea kushirikiana katika kuhakikisha linaboreshwa kwa ajili ya kuandaa kizazi kilicho bora kinachoweza kupambana na mazingira yanayowazunguka," alisema.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid, alisema elimu ni gharama na serikali inaposema inatoa elimu bure haimaanishi kuwa ni bure bali inagharamia vitabu, mishahara, hivyo wazazi wachangie kununua vitabu kwa ajili ya watoto wao watakavyosoma wakiwa shuleni na nje ya mazingira ya shule.

Mwakilishi wa Shule ya Sekondari Tusiime, Jenipher Kaizilege, alisema jarida hilo limeandaliwa vyema na limerahisisha vitu vingi na kuweka katika njia ya picha na michoro, hivyo kumvutia mwanafunzi kusoma na kuelewa kwa haraka, nadharia imepeleka kwenye vitendo.

# Mashirika yajengewa uwezo huduma za bima

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya mashirika 100 ya bima yamepatiwa mafunzo ili kuimarisha upatikanaji wa huduma kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mafunzo hayo ya siku nne yalianza juzi jijini Dar es Salaam na yaliendeshwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema benki hiyo imeanza mpango mkakati wa kuhakikisha matumizi kamili ya teknolojia na mifumo ya kidijitali yanaendelea kuwa sehemu muhimu katika utoaji wa huduma za benki hiyo.

"Ili kuhakikisha benki inatoa huduma bora za bima, tumeanza mpango mkakati utakaohakikisha matumizi ya teknolojia na mifumo ya kibenki ya kidijitali inaendelea kuwa sehemu muhimu ya utoaji wa huduma zetu za benki ili kuongeza upatikanaji wa huduma hii nchini nzima.

"Hivi sasa, Tanzania ina kiwango cha chini zaidi cha upatikanaji wa bima katika Afrika Mashariki, ambayo iko chini ya asilimia moja huku mtandao mpana zaidi wa mawakala wa bima ukienea karibu mikoa yote nchini," alisema.

Aidha, alisema NBC iko katika nafasi nzuri ya kutoa huduma za bima ili kuwafikia watu wengi zaidi iwe kwa wateja au wasio wateja.

Pia alisisitiza kuwa mawakala hao sasa watatumia mfumo maalum uliotengenezwa na benki na washirika wake ili kurahisisha utoaji wa huduma ya bima ya benki hiyo.

"Huduma zetu za bima au mauzo yetu ya bima kupitia nyinyi mawakala yatafanyika kupitia mfumo maalum uliotengenezwa na benki na washirika wake ili kuhakikisha huduma inakuwa rahisi kwenu kama wauzaji wa bima lakini inakuwa rafiki kwa watumiaji wa bima au wananchi kwa ujumla," alisema.

Naye Kamishna wa Bima nchini, Dk. Baghayo Saqware, aliipongeza NBC na Jubilee Alliance kwa kutekeleza wito wa serikali wa kupanua wigo wa huduma na bidhaa za bima nchini. Dk. Saqware alisema Mei, mwaka huu, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa mwongozo unaoelekeza makampuni na watoa huduma za bima kusajili maofisa mauzo wa bima nchini.

"Kilichofanywa na Benki ya NBC na Jubilee Alliance ni kusajili maofisa mauzo wa bima nchini ambao watasambaa kuuza bima Tanzania nzima, nawapongeza kwa hatua yao," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya bima kwa mawakala yaliyotolewa na benki hiyo, pamoja na kampuni ya Jubilee Allianz General Insurance Tanzania kupitia Chuo cha Bima na Hifadhi ya Taifa (ACSID), jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mvomero yanogewa mradi hifadhi misitu

**Na Christina Haule, MOROGORO**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mvomero mkoani hapo imesema kuna umuhimu wa kupatikana fursa nyingine ya kutumia mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) ili kusimamia, kuhifadhi na kupanda miti na kuimarisha misitu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Philipina Philipo, alisema hayo jana ofisini kwake kuwa japokuwa mradi huo unafikia mwishoni katikati ya mwezi ujao, upatikanaji wa fursa ya kuendelea kwa mradi huo utasaidia kupatikana wadau wa kuendelea kutoa elimu ya usimamizi wa misitu.

Dk. Philipo alisema katika kupambana na uharibifu wa misitu, serikali imetoa maelekezo kwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka jambo ambalo wanaweza kulifanya kwa kushirikiana na wadau kwa kuimarisha utunzaji wa mazingira.

Alisema kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira, wananchi wanaweza kupata maji na hewa nzuri na mazingira yakiharibiwa maisha yatakuwa si mazuri tofauti na inavyofikiriwa. Alisema viumbe pia vitaathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo aliupongeza mradi huo kwa kuwezesha masuala mbalimbali kwenye vijiji ikiwamo kuboresha huduma za mbalimbali za kijamii zikiwamo afya, maji na miundombinu mbalimbali ikiwamo ya elimu.

Naye Ofisa Misitu Wilaya ya Mvomero, Edward Kimweri, alisema tayari vijiji viwili vimeshaingizwa kwenye mchakato wa kutekeleza mradi wa CoForEST kupitia bajeti ya mwaka 2022/23 kwa kutengewa Sh. milioni 15.

Kimweri alisema awali mradi huo ulitekelezwa kwenye vijiji vya Msongozi, Misongeni Maharaka, Kihondo, Kipera, Ndole, Magunga, Msolokelo, Diguluma na Masinde ambavyo vimeonyesha mafanikio makubwa ikiwamo kutangaza misitu mitano kwenye gazeti la serikali ili kuwezesha kutambulika kisheria na kulindwa.

Aliitaja misitu iliyotangazwa ni Maharaka, Misengere, Kipera, Kihondo na Msongozi huku wakiwa tayari wameshaandaa sheria ndogo kama vitendea kazi katika kuhifadhi misitu.

Akizungumzia manufaa ya mradi, Mkuu wa Idara ya Maliasili na Mazingira wa Wilaya, Mary Kayowa, alisema suala la uhifadhi limeonekana kuwa juu sambamba na elimu katika vijiji vyenye mradi tofauti na maeneo ambayo hayana mradi.

"Yaani waliopata mradi wamekuwa watu ambao wanaguswa kunapotokea changamoto, iwe ya mradi mwingine au shughuli inatekelezwa na kuwa na viashiria vya kuharibu katika vijiji vyao, wanakuwa wepesi kutoa taarifa ili kulinda maeneo yao na maeneo mazima ya mradi huo," alisema Kayowa.

Mmoja wa wakataji mkaa kwa njia endelevu kutoka Kijiji cha Msolokelo, Jumanne Omari, aliahidi kuendeza mradi wa CoForEST licha ya kuisha mwezi ujao kwa sababu ya kuisaidia jamii ikiwamo kutoa ajira kwa vijana baada ya kukubali kutenga misitu ya vijiji na kunzisha mradi mwaka 2014.



Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (katikati), akionyesha gari jipya aina ya Toyota Rush, atakalozawadiwa mshindi wa promosheni ya Tigo Tanzania ya "Ndinga la Kishua", wakati wa uzinduzi wa awamu ya tatu ya kampeni ya promosheni hiyo, jijini Dar es Salaam jana, itakayowawezesha wateja watakaofanya miamala zaidi kupitia Tigo Pesa, kupata nafasi ya kujishindia zawadi za pesa taslimu kila siku na kila wiki zenye thamani ya mamilioni. Kushoto ni mhamasishaji wa kampeni hiyo, Hamisa Mobeto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkataba watiwa saini kuboresha pamba

**Na Thobias Mwanakatwe,**

MWANZA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), zimetia saini mkataba wa ushirikiano ya kiutendaji katika mradi wa kuzalisha na kuongeza tija kwenye mnyororo wa thamani wa pamba na mazao mengine ya chakula lishe.

Mradi huo wa mwaka mmoja unaojulikana kama 'Beyond Cotton,' unafadhiliwa na serikali ya Brazil kwa Dola za Kimarekani 629,000 na kutekelezwa na taasisi hizo, unatarajiwa kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wa pamba takribani 9,000 kutoka wilaya za Magu, Kwimba na Misungwi mkoani hapo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alipongeza serikali za Brazil na Tanzania kupitia Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono na mtazamo chanya katika kuhakikisha pamba na mazao mengine ya chakula yanaendelezwa na kuongezewa tija kwa manufaa ya wakulima na ukuaji wa uchumi.

Mkamilo alisema kwa namna serikali zote mbili zilivyojipanga, chini ya utekelezaji wa wadau mbalimbali, watahakikisha matokeo ya utekelezaji wa mradi huo yanakwenda kuleta ustawi na ongezeko la ubora na uzalishaji kwenye zao la pamba na kilimo mseto.

"Hafla hii ni fursa ya kipekee katika kuendeleza na kuongeza uzalishaji wa mnyororo wa thamani kwa wakulima wa ukanda wa pamba, lakini kuwajengea uwezo zaidi maofisa ugani wa zao hilo," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alisema ndani ya mfumo wa Ushirikiano wa Kusini-Kusini, mradi wa 'Beyond Cotton' unalenga zaidi kubadilishana maarifa kati ya Tanzania na Brazil katika mustakabali chanya unaolenga kuongeza tija katika kilimo cha pamba na mazao mengine ya chakula, pamoja na kuimarisha mnyororo wa thamani, ikiwamo kuwaunganisha wakulima na masoko ya ndani na nje.

"Ni matumaini yetu kuwa mradi huu utabadilisha maisha ya wakulima wadogo, sisi WFP nchini Tanzania na Kituo cha Ubora cha WFP dhidi ya njaa nchini Brazili-tunathamini ushirikiano thabiti wa TARI na TCB ulioanza tangu mwaka 2019 na tunatazamia kuendeleza vilivyo ushirikiano huu," alisema Gibson.

"Naishukuru Serikali ya Brazil kupitia Shirika la Ushirikiano la Brazil kwa kufadhili mpango huu na kwa kuwachukulia wakulima wadogo wa Tanzania kama wadau watarajiwa katika sekta ya pamba. Pia ningependa kushukuru Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Campina Grande na Taasisi ya Pamba ya Brazili kwa kusaidia mradi huu.

Mwakilishi wa TCB, ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Usimamizi wa Bodi hiyo, James Shimbe, alisema ustawi, tija na ongezeko chanya la uzalishaji wa pamba nchini linategemea zaidi utafiti, hivyo katika kutekeleza azma ya mradi huo, TCB, TARI na WFP wamejipanga kuhakikisha wanashirikiana kwa karibu na halmashauri zote zitakazofikiwa ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Naye Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa TARI, Prof. Joseph Ndunguru, alisema pamoja na mambo mengine, mradi huo unakwenda kufanya utafiti na majaribio ya mbegu, kutoa mafunzo ya kilimo cha pamba na mazao lishe mengine, ikiwamo viazi, mahindi na maharagwe lishe.

Kwa mujibu wa Ndunguru, mradi huo utaongeza thamani kwenye uchakataji wa pamba kwa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) tisa ndani ya wilaya za Kwimba, Magu na Misungwi na baadaye matokeo tarajiwa yatasambazwa nje ya wilaya hizo na kwingineko nchini kwa lengo la kueneza teknolojia ya mradi huo.

Mkurugenzi wa TARI-Ukiriguru, ambaye pia ni mratibu wa zao la Pamba nchini, Dk. Paul Saidia, aliainisha baadhi ya mambo yatakayotazamwa zaidi katika utafiti kulingana na mkataba huo kuwa ni pamoja na kuongeza thamani kwa kuwa na mbegu bora za pamba, kuongeza usalama wa chakula na namna ya kupambana na magugu.

# Utashi kisera, kisiasa waelezwa chachu katika usimamizi misitu

**Na Christina Haule,** DODOMA

UTASHI wa kisera na kisiasa umeelezwa kuwa ni jambo la msingi kwa viongozi kuamua kuwashirikisha wananchi katika utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu (USMJ) ili kuona tija ya uhifadhi na kunusuru uharibifu wa misitu.

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania, Clara Melchior, alisema hayo jana kwenye mkutano wa wadau wa misitu na serikali katika kuangalia namna ya kuwekeza kifedha katika usimamizi wa misitu kilichofanyika jijini hapo.

Alisema mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) unaotekelezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano Uswisi (SDC) ni muhimu ukapewa nguvu zaidi kisera na kisheria kupitia wanasiasa na viongozi.

Kwa kufanya hivyo, alisema mradi huo utaendelea kuzaa matunda kwa wanavijiji kuwa na moyo wa kusimamia misitu baada ya kuona faida ya utunzaji.

Melchior alisema kupitia utafiti walioufanya kupitia wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wamebaini bado kuna mahitaji ya kuendelea na hatua ya tatu ya mradi huo ambao unamalizika mwezi ujao baada ya kutambua kuwa kuna umuhimu wa kupanua wigo wa ushirikishaji wanavijiji kusimamia rasilimali za misitu ya vijiji (USMJ).

Alisema upanuzi wa wigo huo unapaswa kwenda sambamba na kuwajengea uwezo wadau wakubwa wa misitu wakiwamo serikali kuu na za vijiji ambao ndio wenye nguvu kisera na kisheria pamoja na asasi za kiraia ili waone utaratibu mzima wa mradi unavyotekelezwa na kubaini maana ya mradi na kuuendeleza hata pale mradi utakapofikia mwisho.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Deusdedit Boyo, alisema serikali ina mpango wa kusimamia halmashauri zote nchini kutenga fedha katika bajeti za kila mwaka kwa ajli ya kuangalia misitu sambamba na kutumika katika usimamizi na uhifadhi wa misitu.

Boyo alisema utengaji fedha hizo, unapaswa kwenda sambamba na kuzijengea uwezo halmashauri kwa sababu kuna baadhi ya watu hawafahamu umuhimu wa misitu katika mazingira ya kawaida na kuingia kukata kuni na kufanya shughuli zingine za uharibifu wa misitu.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na misitu hekta milioni 48.1 yakiwamo maeneo makubwa yanayoanguka katika ardhi za vijiji yakiwa na hekta milioni 22 na kati ya hekta hizo ni chache ambazo zimeshakidhi kuingia katika mpango wa usimamizi shirikishi.

Kwa mujibu wa Bayo, serikali kupitia wizara hiyo, iko katika mkakati wa kuhakikisha misitu mingi inahifadhiwa kwa sababu inapokuwa haijahifadhiwa kisheria inaweza kuharibiwa.

Alisema tayari wameshatekeleza mkakati wa Sera ya Taifa ya Misitu ambao ndio dira ya kuendeleza misitu katika kipindi cha miaka 10 ijayo kuanzia mwaka 2021 hadi 2031. Pia alisema wametengeneza mpango kazi wa usimamizi shirikishi wa misitu hasa katika vijiji kwa lengo la misitu mingi kuwa katika hifadhi za vijiji na kuhifadhiwa kisheria.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TFCG, Charles Meshack, alisema mradi wa CoForEST una uwezo wa kulinda na kuhifadhi mazingira na kwamba suala la kutoweka kwa misitu nchini linasababishwa na watu wanaofanya shughuli za mbalimbali kwenye ardhi ikiwamo kilimo, mkaa na ulishaji mifugo.



# Watoto 80,000 kupewa dawa za minyoo tumbo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha, imesema wakati wowote kuanzia sasa itaanza kutoa dawa za kinga tiba, dhidi ya minyoo tumbo kwa watoto 80,000 wakiwamo wanafunzi shule zote za msingi.

Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Arumeru, Dk. Petro Mboya, alisema jana kuwa maandalizi ya kutoa dawa hizo yamekamilika, ikiwamo kutoa elimu kwa walimu wa afya shuleni na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wanaokwenda kugawa dawa hizo.

"Walengwa wa dawa hizi ni watoto wenye umri wa miaka mitano mpaka miaka 14. Dawa zinatolewa kwa watoto wa umri huo ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, walioko kwenye mfumo wa shule na wasiokuwa kwenye mfumo wa elimu," alisema Dk. Mboya.

Aidha, alisema kuwa Mpango Jumuishi wa Taifa, umelenga kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ukiwa na dira ya kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi usiyodhoofishwa na madhara ya magonjwa hayo.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Halmashauri ya Arusha, Ramadhani Kulewa, alisema halmashauri hiyo inatarajia kutoa kinga tiba hiyo kupitia vituo 211, kwenye shule za msingi 155, vituo vya afya 56, huku wahudumu 433 wakigawa dawa hiyo, walimu 310 na wahudumu wa afya 112.

Kulewa alisema ili kufikia lengo, licha ya kuwapo kwa vituo maalumu vya kutolea huduma, pia watatumia mfumo wa ugawaji dawa katika jamii kwa kupita nyumba kwa nyumba, ugawaji wa dawa kwa makundi maalumu, pamoja na kwenye mikusanyiko ya watu kama nyumba za ibada, sokoni, vituo vya mabasi na maeneo yote ya biashara.

"Tutahakikisha tunatoa chanjo hii kwa uhakika kwa wahusika kwa lengo la mpango huu ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi usiyodhoofishwa na madhara ya magonjwa hayo," alisema.

Kati ya watoto hao waliolengwa kupatiwa dawa hizo za kinga tiba dhidi ya minyoo tumbo, watoto 76,000, ni wale waliosajiliwa shuleni na watoto 4,000 ni ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo rasmi wa elimu.

# Serikali yasema mahindi ya NFRA si msaada

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI imesema mahindi ya chakula yanayotolewa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) kwa wananchi kwa ajili ya kukabiliana na makali ya njaa na mfumuko wa bei sokoni, si msaada bali ni chakula kinachopaswa kuuza kwa bei nafuu.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, David Lekei, alitoa ufafanuzi huo baada ya baadhi ya wananchi walayani hapo kuomba bei ya Sh. 880 kwa kilo moja ya mahindi ipunguzwe zaidi ili wananchi wengi wenye shida ya chakula wamudu kuyanunua.

"Tufikishieni salaam kwa wananchi wote kwamba haya mahindi si msaada, yanauzwa kwa bei nafuu ili watu wenye uhitaji waweze kumudu kuyanunua. Suala la kupunguza bei na wengine kudhani ni msaada si sawa. Wilaya ya Hai, tumepokea tani 100 za mahindi na tani zingine 200 zitakuja baada ya Mbunge Saashisha Mafuwe kuomba kuongezewa mahindi.

"Kilogramu moja ya mahindi, inauzwa kwa bei shilingi 880 tofauti na sokoni ambako kilogramu moja ni Sh. 1,200 hadi 1,300. Hapo ukitazama maana yake ni kwamba mahindi kilogramu 100 yanayotolewa na NFRA ni sawa na Sh. 88,000 na mahindi yanayouzwa na wafanyabiashara sokoni ni Sh. 150, 000," alisema.

Kwa mujibu wa Lekei, ili kuhakikisha kila mwananchi mwenye uhitaji anapata huduma hiyo, tayari Halmashauri ya Wilaya ya Hai, imetangaza kwa viongozi wa kata zote, vijiji na vitongoji kuandikisha wananchi wenye uhitaji na kupeleka majina ili kupata mahindi hayo.

Kwa sasa, uwezo wa NFRA kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula kwa miezi mitatu, ni zaidi ya tani 500,000 kulinganisha na tani 150,000 iliyokuwa inahitajika miaka ya 1992 wakala ulipoanzishwa.

Kabla ya Lekei kutoa ufafanuzi huo, wananchi hao mbali na kuomba kupunguzwa bei ya mahindi, pia waliomba kusogezwa karibu vituo vya ugawaji wa mahindi kwa kuwa wanatumia gharama kubwa kuyafuata.

Baadhi ya wakazi hao, Ibrahim Munisi, Mkazi wa Kata ya Bondeni na Zakayo Mosha wa Kata ya Muungano, kwa nyakati tofauti, waliwasilisha ombi hilo kwa serikali wakieleza kuwa wananchi wenye hali ngumu zaidi kiuchumi wanashindwa kumudu bei hiyo na kukosa chakula hicho.

Aidha, Faudhia Abdallah, Mkazi wa Kata ya Masama Kusini, aliiomba serikali kuchunguza hali ya kipato cha wananchi wake, kabla ya kupanga bei ya mahindi na kuyapeleka kwa wananchi, kwa kuwa serikali ina nia njema ya kuwasaidia watu wenye mahitaji ya chakula.



Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdalla, akizungumza baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo, katika mkutano mkuu wa CCM Mkoa jijini Tanga juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Mfanyabiashara wa nazi aibuka kidedea uchaguzi m'kiti CCM mkoa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKULIMA wa nazi wa Wilaya ya Pangani, Rajabu Abdallah, ameshinda uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, akichukua nafasi ya mbunge wa zamani wa Lushoto, Hendry Shekiffu.

Rajab aliwabwaga washindani wake, baada ya kupata kura 1,340, akifuatiwa na Derrick Kazoba aliyepata kura 29 na Mathias Mkingwa aliyeambulia kura tisa katika mkutano huo wa uchaguzi.

Akitangaza matokeo hayo juzi usiku, msimamizi wa uchaguzi huo, ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema uchaguzi huo ulikuwa huru na wa haki, huku akiwasihi wagombea na washindi wa nafasi zote zilizogombewa kuvunja makundi yao kabla ya kuondoka ukumbini ili wasiache majeraha ya uchaguzi na kuiumiza CCM kuelekea uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025.

Msimamizi huyo wa uchaguzi, alimtangaza mfanyabiashara wa mabasi ya abiria yaendayo mikoani ya RATCO, Mohamed Salim, kuwa mshindi wa nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kupitia Mkoa wa Tanga.

Salim aliibuka kidedea baada ya kuwashinda wagombea wenzake, Omar Sempoli na Hassan Bomboko, kwa kupata kura 774 na kutetea nafasi hiyo aliyokuwa akiishikilia.

Akizungumza na wajumbea wa mkutano huo, mwenyekiti huyo mpya alisema hakuamini kwamba angeshinda nafasi hiyo kwa kuwa wagombea wote walikuwa na nguvu kisiasa na walikuwa wakiungwa mkono na makundi mbalimbali.

"Niwaahidi wana CCM wenzangu na viongozi wenzangu kwamba nitafanya kazi yangu kwa nguvu zote kukitumikia chama pamoja na nchi kwa ujumla. Nawashukuru wajumbe wenzangu kwa kuniamini tangu awali na kunipa nafasi hii. Kikubwa kilichoko sasa ni kufanya kazi kwa maendeleo ya mkoa na taifa letu kwa kumuunga mkono Rais wetu, Samia Suluhu Hassan," alisema.

Kabla ya uchaguzi huo, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Tanga, Shekifu, alisema hana upande wala kinyongo kuhusu uchaguzi huo. Alisema katika uongozi wake alipigania na kusimamia hoja yake ya kutaka mkoa wa Tanga kugawanywa na kuwa mikoa miwili.

"Ndugu zangu mliochaguliwa endeleeni na hii hoja kwa kufuata nyayo zangu. Niwaombe kama chama mwendelee kulibeba hili kwa ukubwa wake na kulisemea ngazi za juu, kwa kuwa Tanga ni mkoa ambao una halmashauri nyingi, hivyo inaleta ugumu kwenye kutoa maamuzi ya kiutawala," alisema Shekifu.





# Jiji lapitisha azimio ujenzi kituo mabasi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, limepitisha azimio la kutaka kuanza mara moja kwa utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi, kitakachojengwa eneo la Bondeni City.

Mbali na kituo hicho cha mabasi, pia madiwani hao wamepitisha mpango wa ujenzi wa soko la kisasa la wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga na kuanza kwa mchakato wa kuuza viwanja zaidi ya 100 kwa wananchi pamoja na taasisi mbalimbali.

Azimio hilo lilipitishwa na kutangazwa jana na Meya wa Jiji hilo, Maximillian Iraqhe, baada ya kumalizika kwa kikao maalum cha Baraza hilo la Madiwani.

"Wananchi wa Mkoa wa Arusha, walikuwa wanasubiri kwa hamu kuona ujenzi wa stendi mpya ya mkoa inajengwa. Sasa nawahakikishia wananchi wa Mkoa wa Arusha, fedha zimeshapatikana kwa sasa tunaendelelea na upembuzi yakinifu na ujenzi huo utaanza rasmi mwezi Machi mwaka 2023.

"Ujenzi wa stendi hii ya kisasa, utakwenda sambamba na ujenzi wa soko la machinga katika eneo hilo la Bondeni City, ili wafanyabiashara wadogo wapate eneo maalum la biashara, linalokwenda sawa na hadhi ya Jiji letu hili la kitalii."

Kwa mujibu wa Iranqhe, fedha za ujenzi wa stendi hiyo zinatoka Benki ya Dunia (WB), kupitia Mradi wa TACTICS, na kwamba ujenzi wa soko la machinga la kisasa, Halmashauri ya Jiji hilo imeshatenga fedha kutoka kwenye mapato ya ndani, kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

Alisema stendi hiyo ya kisasa ujenzi wake ukikamilika, utakuwa chanzo kikubwa cha mapato ya Halmashauri ya Jiji la Arusha, ambako wanatarajia kukusanya zaidi ya Sh. bilioni moja kwa mwezi.

"Jiji la Arusha, tutajenga soko la machinga la kisasa katika eneo hilo la Bondeni City ambalo linakwenda sambamba na hadhi ya Jiji letu la kitalii ili watalii wanaokuja katika jiji letu waweze kutembelea soko hilo la kununua bidhaa mbalimbali,"alisema.

Kuhusu mradi wa uuzaji wa viwanja Iranqhe alisema idara ya ardhi ya halmashauri ya Jiji la Arusha, itaanza mchakato wa kuuza viwanja katika eneo hilo sambamba na aliyekuwa mwekezaji wa eneo hilo.

"Hivi karibuni tutaoa matangazo ya kuanza kuuza viwanja katika eneo la Bondeni City, vyenye ukubwa tofauti, ambapo mji utakuwa ni mji wa kitalii na utajengwa kwa utaratibu maalum ili kuongeza hadhi ya Jiji letu la Arusha," alisema.

Iranqhe, alitumia fursa hiyo kuwaalika wananchi wa Mkoa wa Arusha, kuchangamkia fursa hiyo ya kununua viwanja baada ya matangazo kutoka na hakutakuwa na upendeleo wowote katika kutoa fomu hizo.

# Zalothe achaguliwa tena uenyekiti CCM

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa zamani na aliyewahi kuwa Kamanda wa Polisi katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Shinyanga, Zelothe Stephen, amechaguliwa kwa kipindi cha pili mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha.

Zelothe alishinda kiti hicho juzi kwa kura 683 kati ya kura 970 zilizopigwa na wajumbe halali wa mkutano mkuu wa chama hicho na kuwashinda wagombea wenzake, Robert Kaseko aliyepata kura 281 na Edna Kivuyo aliyeambulia kura sita.

Juzi usiku, msimamazi wa uchaguzi huo, Loota Sanare, ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alimtangaza Zellothe kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM wa mkoa kuanzia sasa hadi mwaka 2027.

Katika mkutano huo, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Arusha, aliwataka wanachama wa chama hicho kuachana na dhana ya kukomoana kutokana na makundi ya uchaguzi yaliyojengwa wakati wa kupigania nafasi walizoomba.

"Nawashukuru sana wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM Mkoa wa Arusha, kwa kutimiza haki yao ya kidemokrasia na kufanya uamuzi wa kumchagua Zelothe. Nimeridhika kabisa kwamba uchaguzi umefanyika kwa amani na kwa utulivu na hapakuwapo kwa dosari yoyote," alisema Pinda.

Aidha, baada ya kutangazwa kuwa mshindi, Zellothe, aliwashukuru wajumbe kwa kumwamini tena na kumchagua katika nafasi hiyo awamu nyingine. Aliwaomba wanachama wa CCM, kumpa ushirikiano katika kipindi cha uongozi wake ili kusukuma gurudumu hilo. Alisema siri kubwa ya mafanikio katika chama ni ushirikiano na imani waliomwonyesha katika kipindi cha uongozi wake wa siku 1,089 alizoongoza awali na aliahidi utendaji kazi maradufu ili kujenga CCM kuwa imara kwa maslahi ya chama na wananchi.

Mgombea Robert Kaseko, aliyeshika nafasi ya pili, aliwashukuru wajumbe kwa kumpa kura 281 huku akisema amepata kura nyingi sana katika historia ya uongozi wake kwa kuwa wajumbe walionyesha kumkubali.

Hata hivyo, aliwaomba wanachama kumpa ushirikiano mwenyekiti aliyechaguliwa kwa kuwa uchaguzi umeisha na kiliko mbele ni kukijenga chama kwa maslahi yao na wananchi kwa ujumla.

"Binafsi nampongeza Zellothe kwa dhati kabisa kwa kuaminiwa na wajumbe kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa kipindi cha 2022- 2027 na ninamtakia heri katika uongozi wake, kwa muda miaka mitano mingine.

Naye Edna Kivuyo, mgombea mwanamke wa nafasi hiyo, aliwashukuru wajumbe kwa kumpa kura alizopata, zilikuwa nyingi kwa kuwa ni mwanzo wa kuanza harakati za kuwania nafasi mbalimbali za chama.




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti kwa pamoja wakivuta pazia kuzindua rasmi upanuzi wa kiwanda cha kutengeneza bia cha SBL Moshi, mkoani Kilimanjaro mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia atangazia kiama wahudumu wa afya wanaofanya kwa mazoea

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali inawamulika watumishi wa sekta ya afya wanaofanya kazi katika hospitali mbalimbali nchini, kama wanatoa huduma vizuri kwa wagonjwa wanaofikishwa kwao kupata huduma za tiba na uchunguzi.

Amesema kama wafanyakazi hao wakibainika kwamba wanawahudumia vizuri wagonjwa na wakaenda nyumbani kwao kuendelea na shughuli za kiuchumi, na wao wataonwa na serikali kwa kuboreshewa maslahi yao.

Akizungumza jana katika mji wa Babati, alikokwenda kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Rais Samia alisema wafanyakazi hao wanachopaswa kukifanya ni kuendelea kuwahudumia wagonjwa kwa moyo wa huruma. "Nimeona mradi huu unakwenda vizuri, lakini niagize sasa wafanyakazi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, muwahudumie vizuri wagonjwa ili afya zao zitengamae na waweze kuendelea na shughuli za kiuchumi.

"Mimi niwaombe hudumieni kwa dhati na kwa moyo mmoja, wagonjwa wanaokuja kutibiwa hapa Hospitali ya Mkoa. Mkiwahudumia vizuri wagonjwa wakaenda nyumbani kwao kuendelea na shughuli za kiuchumi, na nyie mtaonwa na serikali kwa kuboreshewa maslahi yenu. Si sawa! Hakuna kurudi nyuma, kazi lazima iendelee ya kuwahudumia wananchi."

Aidha, Rais Samia akiwa hospitalini hapo, alisisitiza kuwa kama watawahudumia vizuri wagonjwa, mapato yao pia yataongezeka na serikali itawaongezea kwa kuboresha stahiki zao.

Awali, akizungumza kabla ya Rais Samia, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molell, aliwahakikishia wakazi wa Mkoa wa Manyara, kwamba jengo la huduma ya damu likikamilika, wataanza kulitumia, hawatakuwa tena na haja ya kutegemea kupata huduma hiyo kutoka Benki ya Damu iliyoko katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC. Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Catherine Magali, akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo wa ujenzi, alisema kwa sasa umefikia asilimia 85. Alisisitiza kuwa kwa majengo yanayojengwa likiwamo jengo la huduma za damu, umefika asilimia 60.

Dk. Magali alisema: "Upatikanaji wa dawa katika hospitali hiyo ni asilimia 97, na hata dawa zisipopatikana wagonjwa wanatafutiwa. Tunashukuru kwa fedha za UVICO-19 na huduma za dharura, tumeanza kupata na tutaanza kutoa huduma za CT Scan Desemba mwaka huu.

"Hatuna budi kuishukuru serikali unayoiongoza Mheshimiwa Rais, kwa kuwa imetoa fedha za kujenga majengo na kuwekeza mtambo wa kuzalisha hewa ya Oxjeni, ambao umetumia gharama ya zaidi shilingi milioni 600. Hivi sasa mitambo hiyo ina uwezo wa kutengeneza mitungi ya gesi 80 kwa siku."

ama
ALHAMISI NOVEMBA 24, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




**KABRASHA LA COP27**
**Kutoka kitendawili cha tabianchi hadi penye mwelekeo wa safari kuu iliko**

Ukurasa 18



**KABRASHA LA COP27**
**Dunia inavyopambana kukabili ukame na miradi mipya 19 ya kuinusuru Afrika**

Ukurasa 16

# Hatari ya kujenga nyumba yako jirani na penye mti wa mbuyu

**Na Halfani Chusi**

NYUMBA ni makazi ya kudumu. Kwa namba, huwa hapatakiwi kukosa usalama wa kudumu kwa mmiliki, kuanzia mazingira yanayoizunguka nyumba hiyo, ikiwamo ndani na nje.

Kwa maeneo ya mjini, nyumba nyingi zimejengwa kwa kiasi kikubwa, kuzingatia mahitaji ya ubora na ufanisi. Tatizo zaidi linaonekana vijijini, ambako wakazi wengi hujenga pasipo kuzingatia tahadhari ubora na usalama stahiki.

Mkoani Iringa, ambako kuna miti ya mibuyu kwa wingi, haiendani na uhalisia namna pale wakazi wanajenga nyumba karibu na miti aina ya mibuyu ambayo kimsingi ni miti inayoishi muda mrefu, huku nyumba nazo vilevile hudumu muda mrefu zaidi ya mibuyu.

Ujenzi huo unamfanya mwenye nyumba awe katika hatari ya kupoteza maisha, kuharibika miundombinu ya nyumba hiyo, inayodondokewa na mibuyu.

Ushuhuda wa Nipashe katika vijiji vya wilayani Kilolo, mkoani Iringa, wanavijiji wengi wamejenga jirani na mibuyu, bila ya tafakari kuhusiana na uelewa wa madhara yaliyoko.

Ni muktadha unaotoa funzo, kukiwapo ushuhuda kutoka habari iliyoandaliwa na gazeti hili wastani wa zaidi ya mwezi mmoja sasa, ukiripoti watu wawili waliofariki dunia Dar es Salaam, eneo la Kinondoni Mkwajuni, baada ya kudondokewa na mbuyu uliokuwa pembeni ya nyumba hiyo.



Nyumba iliyojengwa karibu na mbuyu huko kijijini Mgowelo, mkoa wa Iringa wilayani Kilolo katika Kata ya Nyanzwa. Jirani ni pikipiki iliyoegeshwa. **PICHA: HALFAN CHUSI.**

Tukio jingine lilitokea mkoani Iringa katika kijiji cha Ruaha Mbuyuni, wilaya ya Kilolo, baada ya pikipiki kudondokewa na mbuyu na ikaharibiwa vibaya, hata mmiliki, Bezalali Pasko, aliyekuwa akijishughulisha na kilimo cha kitunguu kijijini, kupoteza usafiri wake kwa maana ya kuharibika kwa hali mbaya zaidi.

Ni madhila yanayoendelea kujitokeza dhidi ya wanaofanya uwekezaji karibu na mti wa jamii hiyo, kikuu kinachowaponza wengi ni kufuata kivuli cha mti huo bila kujua kuna mda mbuyu utakauka na kuchoka na hivyo utadondoka bila kutoa taarifa.

Kuna kila sababu ya jamii kuepuka kufanya uwekezaji karibu na miti ya aina hiyo, hata pale inapotokea ulazima wake ushauri ni wa mhusika akijitahidi kuepuka ama ukaribu nao au aukate mti huo.

Pia, kila wakati hasa nyakati za kiangazi, unapukutisha matawi ambayo yana athari. Anafafanua, pia katika kijiji cha Mgowelo kilichopo mkoani Iringa wilaya ya Kilolo, mwanafunzi alipata ulemavu kwa kuangukiwa na tawi la mbuyu, wakati akipita njiani kuelekea shuleni.

Matukio hayo kwa ukubwa wake, yanarejesha elimu ili kuwakumbusha wawekezaji kutowekeza karibu na miti ya aina hiyo, katika mazingira ya usalama zaidi.

Kama ilivyo miti mingineyo, mibuyu ina umri wa kuishi na pale inapotimu, huanza kuchakaa na kuoza na ndio safari ya kudondoka inapoanza.

Mara zote, kinachopotosha watu wengi, ni mtazamo wa kuona mti huo bado una umri mrefu wa kuishi.

**SIMULIZI YA MKASA**

Mama Mzazi wa mtoto aliyewahi kupoteza maisha kwa mkasa kudondokewa na mbuyu, Anjelina Paul, anaeleza mkasa ulivyotokea: "Nyumba yetu ilikuwa karibu na mti wa mbuyu. Siku moja tulikuwa tumeenda shambani, mwanangu alikuwa ameenda shule. Aliporudi, akawa anapika ghafla mbuyu ulianza kuyumba ukadondoka na kusababisha mwanangu kupoteza maisha.

"Tukapigiwa simu, tukarudi nyumbani mapema, lakini tulikuta raia wema wameshawatoa, lakini tayari walikuwa wameshakufa. Roho yangu iliniuma sana mwanangu alikufa kifo kibaya sana."

Mama huyo sasa anatumia nafasi hiyo, akiisihi jamii pale inapotaka kujenga au kufanya uwekezaji, lazima waangalie kwa makini eneo hilo na kutotumia miti ya mibuyu kama kivuli.

"Huwa inatoa wadudu ambao wakikudondokea katika mwili, wanawasha sana na wengine huvimba mwili mzima. Sisi huwa tunaita washawasha hawa wanapenda kukaa kwenye mibuyu," anasema.

***Wasiliana kwa simu: 255 787 879707.***

MAZINGIRA

# Wenye mji wao Mpanda walivyoteketeza vichaka 'makao makuu' magenge uhalifu

## •Makaburini, Stesheni palikuwa shida 'usiku, mchana'

**Na Neema Hussein, Mpanda**



Makaburi ya Mwangaza, katika Mtaa wa Mpadeko, mjini Mpanda katika hali mpya baada ya kusafishwa. Awali palikuwa na majani kimo zaidi ya mita mbili, wahalifu wakitumia kukaba watu na kuhifadhi nyenzo zao.

WASTANI wa mwaka mmoja uliopita, kulikuwapo makundi ya vijana waliotuhumiwa kwa uhalifu kutokana na kukosa ajira, huku kukiwapo makundi yaliyosifika kwa wizi mjini Mpanda,

Hapo kuna simulizi kutoka kwa Juvenary Deus, Mwenyekiti wa Mtaa wa Msasani, mjini Mpanda, anayetoa ushuhuda kwa Nipashe, mtaa wake ulikuwa moja ya maeneo yalikofanyika maasi 'mchana kweupe', hadi katika maeneo yenye mapori makubwa.

Ni mazingira yaliyotumika kuwa kificho cha makundi ya kihalifu na eneo mojawapo panatajwa ni makaburi ya Mwangaza, katika Mtaa wa Mpadeko. kata ya Makanyagio.

Eneo hilo kipindi cha nyuma lilikuwa tishio kwa wakazi husika, kutokana na kuzungukwa na nyasi ndefu na ikawa sababu ya kutumika kama kificho cha wahalifu na silaha zao.

Ni jambo lililochukua nafasi kubwa, hata serikali ngazi ya mkoa nayo kuingilia kati kukabili makundi hayo ya uhalifu, hali kadhalika kusafisha maficho.

Kwa mujibu wa taarifa ya kimkoa, eneo jingine lililokuwa pori jirani na stesheni ya treni, nako vijana wahalifu wakapatumia kudhuru abiria.

Baada ya serikali kugundua maeneo hayo hatari kwa maisha ya watu, ikaweka jicho hata kufikia hatua kujadili katika vikao mbalimbali na ndio mwarobaini wa uhalifu kutoka mapori ya mjini Mpanda, kufikia mwisho.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpadeko, Kata ya Makanyagio, Ivo Chambala, anaeleza kwamba wakati anaingia madarakani mwaka 2019, kulikuwapo makundi ya kihalifu, akiwa na ufafanuzi wake kuwa:

"Sasa katika vikao vyetu tulikuwa tunajua kabisa hilo eneo la makaburi ya Mwangaza ni eneo hatarishi hasa, tukiliacha likiwa chafu, kwa sababu vitendo vyote vya kihalifu vilikuwa katika hilo chaka linalowahifadhi wavuta bangi.

"Hata mali za wizi zilikuwa zikifichwa katika hayo makaburi. Kupitia vikao vya kiserikali tulivyokua tukivifanya, ikaonekana pale tufanye kila namna kwa juhudi hata kuomba msaada katika taasisi yeyote serikalini au nje ya serikali, tuweze kusaidiana kuweza kuondoa vichaka ili kuepusha masuala ya uhalifu, ikiwemo uvutaji bangi na ubakaji.

"Nakiri eneo hilo halikuwa sehemu salama, kinamama wengi wamedhalilishwa, wamebakwa pia hata watoto wadogo vilevile, hata kuporwa wameporwa sana katika eneo hilo.

"Mpaka hivi sasa tunawahimiza wananchi, pindi tutakapokuwa hatuna uwezo wa kutumia nguvu ya kusafisha eneo hilo, tutakapokuwa tumewahitaji kuwaomba msaada basi tusaidiane wote kwa pamoja.

"Sababu eneo hilo kwanza ni hatarishi, endapo tutakuwa tunaliacha bila kufanya usafi, pili ni lazima tuheshimu sababu ndio safari yetu ya mwisho, baada ya kumaliza maisha ya hapa duniani," anasema Chambala

Anakumbusha mikasa kadhaa, ikiwamo mwendesha bodaboda kutekwa na kupelekwa makaburini walikomnyang'anya vifaa vyake. Pia, kuna lingine binti naye akabakwa katika eneo hilo, hali kadhalika makaburi kufukuliwa kutafuta mali.

"Tukio jingine ambalo sio rasmi, labda kipindi ambacho tunafanya usafi tulikuja kugundua, vilevile eneo hilo lilikuwa kama maficho ya silaha za jadi mapanga,visu vilikuwa vinahifadhiwa pale usiku, baada ya watu kumaliza shughuli zao mtaani," anaeleza Chambala.



Mzee Ivo Chambala, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpadeko, Kata ya Makanyagio, shujaa mwenye mchango mkubwa kufanikisha usafishaji makaburi ya Mwangaza na kukomesha uhalifu. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

### USAFI UNAVYOFANYIKA

Chambala anasema, eneo hilo linasafishwa na wanaohusika, wakazi wote wa mitaa inayolizunguka, pia wakihusisha Manispaa ya Mpanda, kwani ni eneo la maziko ya jumla kwa jamii ya mahali hapo, hivyo wakawahusisha waumini aina zote.

"Mwitikio unakuwa bado ni mdogo, suala la machaka bado linaendelea, ila kupitia uongozi wa serikali kuna mfadhili aliyekuwa amejitolea kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na uongozi wa Kata ya Makanyagio, kupitia diwani wetu, wenyeviti na watendaji wa kata.

"Huyo mfadhili alikubali kulipa angalau gharama kidogo, ili kuweza kuwatumia wafungwa kusafisha eneo hilo na kuondoa kero na adha iliyokuwa ikitukuta," anaeleza Chambala.

"Kwa ushirikiano wa pamoja, tulikuja kungundua pia ni sehemu ya vijana wengi ambao wapo majengo na kituo chao inakuwa Shule ya Sekondari Mwangaza.

"Ndio ilikuwa kituo wanachokutana mara kwa mara, ukiwaona ni kama wamekwenda kwenye mazoezi ya mpira, kumbe wanakuwa ukingoni mwa makaburi kwa ajili ya kupanga mipango yao ya kihalifu," anasema.

"Katika vikao vyetu tulikuwa tunajua kabisa, hilo eneo la makaburi ya Mwangaza ni hatarishi, hasa tukiliacha likiwa chafu, sababu vitendo vyote vya kihalifu lilikuwa hilohilo chaka linawahifadhi wavuta bangi, hata mali za wizi zilikuwa zikifichwa katika hayo makaburi.

"Kupitia vikao vya kiserikali tulivyokuwa tukivifanya ikaonekana pale tufanye kila namna juhudi hata kwa kuomba msaada katika taasisi yoyote serikalini au nje ya serikali, tuweze kusaidiana kuweza kuondoa vichaka ili kuepusha maswala ya uhalifu ikiwemo uvutaji bangi na ubakaji.

"Kwa hiyo, mpaka hivi sasa tunawahimiza wananchi pindi tutakapokuwa hatuna uwezo wakuweza kutumia nguvu ya kusafisha eneo hilo tutakapokua tumewahitaji kuwaomba msaada basi tusaidiane wote kwa pamoja.

"Eneo hilo kwanza ni hatarishi, endapo tutakuwa tunalicha bila ya kufanya usafi, pili ni lazima tuheshimu sababu ndio safari yetu ya mwisho baada ya kumaliza maisha ya hapa duniani," anafafanua Chambala, kuhusu vichaka vya makaburini.

Anasema eneo hilo wanaohusika kufanya usafi ni wakazi wa mitaa inayolizunguka, pia katika vikao vyao wanaihusisha na Manispaa ya Mpanda, kwa sababu maziko yanayofanywa hapo ni kwa karibu wakazi wote, hivyo hata viongozi wa dini wanahimizwa kuwahusisha waumini usafi wake.

Pia, anasema kuna mwitikio mdogo na hadi sasa kupitia uongozi wa serikali kuna mfadhili aliyejitolea kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza linalotumia wafungwa pamoja na uongozi wa Kata ya Makanyagio, kupitia diwani wenyeviti na watendaji wanasafisha eneo hilo na kuondoa kero ya vichaka.

Juvenary Deus ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Msasani, anaisimulia Nipashe kuwa:"Mwaka jana, hili eneo ndio lilikuwa linaongoza kwa ukabaji, unakuta labda msafiri zile siku za treni anakuwa hana hata fedha tu ya kusema alipe aingie uwani na wazo la kuomba kwa mtu hana."

Anaendelea: "Basi anaamua kuingia kwenye kichaka ili watu wasimuone, kumbe wale mabwana ndio wanakuwa kule, basi ndio wanakabwa kwa mtindo huo."

Pia, anasimulia mbinu nyingine ya wahalifu hao wanaoazima mavazi ya askari mgambo kutisha wapita njia, eneo hilo la stesheni, akifafanua: "Wanamuonyesha hicho kitambulisho na yeye anakubali, anawafuata, akifika huko anawakuta na wengine kwenye kichaka ndio wanamkaba sasa hizo ndio zilikua mbinu zao."

***Soma zaidi kesho, ukosefu ajira Mpanda na vikundi vya kihalifu.***

AFYA

# Pata mzizi wa shida kukosa usingizi

Na Romana Mallya

TATIZO la kukosa usingizi limekuwa janga kwa walio wengi, ikichangiwa na mfumo wa maisha wa kila siku ambao unamweka mtu hatarini, kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watu, muda wa kulala unapofika mtu anashindwa kufanya hivyo na baadhi wanaeleza huchukua uamuzi hata wa kwenda baa kunywa pombe au kucheza muziki, ili tu muda usonge.

"Kuna wakati ninakosa usingizi kabisa na hali hii hunitokea mara kwa mara hasa ninapokuwa na msongo wa mawazo, ninapokuwa hivyo wakati mwingine ninatoka nyumbani na kwenda baa kupoteza muda.

"Ninaweza kukaa baa kuanzia saa tatu usiku hadi saa saba au nane usiku kisha ninarudi nyumbani," Petro Godluck, mkazi wa Mbezi Kimara, akieleza hadithi ya ukosefu wa usingizi unavyomsababishia kukesha baa.

"Baa siyo kwamba ninakwenda kukaa tu, ninakunywa bia zangu za kutosha wakati mwingine hata 10, ndipo ninarudi nyumbani, hapo sasa nitalala cha ajabu ikifika saa 12 asubuhi usingizi unakata. Na hii hunitokea hata mara tatu kwa wiki," anasimulia.

Tatizo kama hilo lipo pia kwa Christina Paulo, mkazi wa Temeke, anayeeleza mkasa wa kuachana na mwenza wake, haujamuacha salama.

Ilikuwaje? Christina anasema miezi tisa iliyopita, aliingia kwenye mgogoro na mwenza wake na kufikia hatua ya kuachana.

Anasema, kitendo hicho kimekuwa kikimuumiza kwa sababu bado anampenda mume wake na hali hiyo imekuwa ikimpa msongo wa mawazo.

Christina anafafanua kuwa, huwa anapata mawazo zaidi pindi anapoingia kitandani, kwa sababu anaishi mwenyewe na hali hiyo husababisha kukosa usingizi kwa wakati.

"Kila siku ninaamka saa 11 alfajiri kujiandaa kuwahi kazini, ninafanya kazi Posta Mpya, huwa ninatamani nilale angalau kuanzia saa tatu usiku kutokana na muda ninaoamka siku za kazi.

"Cha ajabu, nikiingia kitandani mfano saa tatu usiku, huwezi amini ninaendelea kuwa macho tu na kwa sababu nipo peke yangu, basi nitawaza milima na mabonde niliyopitia.

"Mwishowe ninaamua kuchezea simu, nitaingia mitandaoni na ninaweza kufanya hivyo hadi saa saba usiku nipo macho tu, na wakati mwingine mapigo ya moyo huenda mbio ninahisi ni kwa sababu ya kufikiria sana na kukosa usingizi," anasimulia.



Mazingira ya mtu aliyekosa usingizi rasmi, hatua anakofikia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Christina anasema hali hiyo imesababisha utendaji kazi wake katika shughuli zake za kila siku upungue, kwa sababu anapokuwa kazini, kwa kuwa mwili huwa na uchovu, hujikuta akisinzia na wakati mwingine mwajiri wake amekuwa hafurahishwi na utendaji kazi wake.

Mwanamke huyo anasema, aliwahi kuonana na mwanasaikolojia ambaye ushauri wake mkubwa ulikuwa ni kuhakikisha anapunguza mawazo na kutenga muda mrefu wa kulala, ili kutokaribisha maradhi. Pia, anasema amewahi kwenda hospitali na baada ya kumweleza daktari mateso anayoyapitia, ushauri wake haukuwa tofauti na wa mwanasaikolojia, na alimpatia dawa za usingizi ili azitumie kwa siku kadhaa ubongo upumzike.

Anasema, bado hali hiyo imekuwa ikimrudia na amekuwa akijitahidi ili iishe.

#### HATARI ILIYOPO

Ni maradhi gani hayo yanayoweza kumpata mtu asiyezingatia utaratibu wa usingizi, Mtaalamu wa Afya na Mazoezi kutoka Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza, Dk. Waziri Ndonde anasema.

Anataja maradhi mojawapo yanayochangia watu kupata magonjwa yasiyoambukiza, ni kukosa usingizi wa kutosha unapaswa kulala siyo chini ya saa saba au nane usiku.

Mtaalamu huyo anasema, kwa kawaida mtu mzima hutakiwa kulala saa hizo mfululizo, lakini walio wengi hawafanyi hivyo.

"Magonjwa yasiyoambukiza yanachangiwa na mambo matatu, kukosa usingizi wa kutosha, kutofanya mazoezi na kula vyakula bila mpangilio," alibainisha.

Kutokana na changamoto hiyo, anasema wanaendelea kuelimisha makundi mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari, ili wasaidie kuielimisha jamii isiendelee kupata maradhi hayo.

Mtaalamu huyo anasema kwa mwaka huu katika kupeleka elimu kwa jamii, wamefanya matukio mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa waandishi wa habari wa mkoani Mwanza, ili wasaidie kutoa elimu kwa wananchi kupitia kalamu zao.

Akifafanua zaidi, mtaalamu huyo anasema zipo sababu nyingi zinazochangia magonjwa hayo, lakini mfumo wa afya ulivyo unahitaji vitu vitatu.

"Unapofanya shughuli za kila siku, tishu zilizopo kwenye mwili wako zinaharibika, muda wa kulala ndiyo mwili unajikarabati, kama ni moyo ulikuwa na hitilafu utajikarabati wenyewe,"anaeleza Dk. Ndonde, akifafanua endapo mtu hapati muda wa kulala, ni rahisi kupata msongo wa mawazo.

Anasema magonjwa ya moja kwa moja ambayo mtu anapata kwa kutolala vizuri, ni moyo na mishipa ya damu, akisema takwimu za dunia zilizotolewa mwaka jana, zinataja magonjwa ya moyo na mishipa ya damu kwa mwaka yanasababisha vifo milioni 18 duniani, moja ya sababu ni kutopata usingizi wa kutosha.

Anasema, nchini Tanzania takwimu za mwaka 2012 zilizofanywa na Shirika la Afya Ulimwenguni na Wizara ya Afya, asilimia 33 ya vifo hutokana na magonjwa ya moyo na mishipa ya damu.

Kwa upande wa watoto, Dk. Ndonde anasema wasipopata usingizi wa kutosha, ukuaji wao unakuwa siyo mzuri.

"Mwana michezo asipopata usingizi wa kutosha hawezi kupona majeraha, watu wote wanaofanya kazi za nguvu wanaotembea sana, wanaoendesha baiskeli, wasipopata usingizi wa kutosha, mwili hauponi majeraha, namna unavyotembea sana au kuendesha baiskeli mwili unapata majeraha.

"Ukienda kulala yale majeraha ndiyo yanajikarabati, ushauri wetu kwa ujumla watu watimize vitu vitatu kula mlo kamili, mazoezi siyo chini ya dakika 30 kwa siku na usiku alale sio chini ya saa saba," anashauri.

Kuhusu mlo kamili, anasema katika milo mitatu iliyozoeleka, lazima iwe kamili ziwapo mboga za majani na matunda na usiku anapaswa kula saa mbili kabla ya kuingia kitandani.

"Ni vizuri mtu ale mlo wake wa usiku siyo chini ya saa mbili kabla ya kulala, siyo vizuri mtu anakula alafu anakwenda kulala, akishamaliza kula afanye shughuli mbalimbali siyo akae tu akisubiri kulala, lazima mwili wake ushughulike, pia tuepuke kula sukari nyingi na chumvi nyingi kupita kiasi," anasema.

#### UGONJWA WA KISUKARI

Mwenyekiti wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Prof. Andrew Swai anashauri watu wapunguze msongo wa mawazo ambao umekuwa ukisababisha mtu kupata maradhi ikiwamo saratani.

Dk. Swai anasisitiza watu kupata muda wa kutosha kulala, pia kupunguza msongo wa mawazo unaosababisha magonjwa kama saratani, pia wafanye mazoezi angalau kwa siku mara moja.

Anatoa mfano, wa ugonjwa kisukari, akisema miaka ya 1991 kulikuwa na asilimia moja tu ya ugonjwa huo nchini, lakini kwa sasa umeongezeka hadi kufikia asilimia tisa.

Anasema tatizo hilo linagharimu asilimia 20 ya bajeti ya serikali kwa kuwahudumia wagonjwa hao.



MAZINGIRA

## KABRASHA LA COP27

# Dunia inavyopambana kukabili ukame na miradi mipya 19 ya kuinusuru Afrika

**Na Maulid Mmbaga**

WAKATI mataifa mbalimbali yakiumiza 'ubongo' kutafuta njia mbadala ya kukabiliana na ukame, wataalamu wa masuala ya mazingira, wamechapisha orodha ya miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 120, kwa ajili ya kuzisaidia nchi maskini zinazokumbwa na mabadiliko ya tabianchi.

Wataalamu hao ni miongoni mwa wajumbe wanaoshiriki katika mkutano wa mabadiliko ya tabianchi wa Umoja wa Mataifa (COP27), uliofanyika nchini Misri ukikamilika wiki iliyopita, huku zaidi ya miradi 19 ikitangazwa kutekelezwa barani Afrika.

Mingine ni mradi wa dola bilioni tatu za Kimarekani wa kuhamisha maji baina ya Lesotho na Botswana, pamoja na mpango wa kuboresha mfumo wa maji ya umma nchini Mauritius ulio na thamani ya Dola za Marekani milioni 10.

Mjumbe wa Marekani anayehusika na mazingira, John Kerry, ametangaza kuundwa mfuko wa kukabiliana na gesi ya kabonim unaolenga kuyasaidia mataifa yanayoendelea kuharakisha kuondokana na matumizi ya nishati ya mafuta ya kuchimbwa.

Marekani imezindua mfuko huo kwa jina la ETA, kwa lengo la kufadhili miradi ya nishati mbadala na kuharakisha matumizi ya nishati safi katika nchi zinazoendelea. Chile na Nigeria, ni miongoni mwa nchi zilizooonyesha nia ya mapema kunufaika na mfuko huo.

Ripoti ya Jopo la Kisayansi linalotoa taarifa za mwendo wa joto, kiwango cha ongezeko sasa liko katika wastani nyuzi 1.09 na vita iliyoko ni kudhibiti isivuke nyuzi joto 1.5.

Ni hatua zinazoendana sasa, kwamba nchi ya Afrika Kusini, inatajwa kupokea fedha Euro milioni 600 kutoka Ufaransa na Ujerumani, ikiwa ni sehemu ya mpango wa uwekezaji kuisaidia katika kipindi cha mpito wa nishati.

Taarifa yao ya pamoja, nchi hizo tatu zimetia saini makubaliano ya fedha hizo za mkopo, kila nchi ikitoa Euro milioni 300 kila moja kuisaidia kupunguza utegemezi kwenye nishati ya makaa ya mawe.

Afrika Kusini inatajwa katika orodha ya mataifa 12 yenye uchafuzi wa hewa duniani, ikizalisha wastani wa asilimia 80 ya umeme wake kupitia makaa ya mawe.

**RIPOTI YA WMO**

Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa la Umoja wa Mataifa (WMO) katika ripoti yake, inabainisha kuwa miaka minane iliyopita ilikuwa ya joto zaidi katika historia ya rekodi, ikichochewa na ongezeko la viwango vya gesi chafuzi.

Ripoti hiyo iliyotolewa siku chache zilizopita, inaangazia utafiti wa mwaka huu wa hali ya hewa duniani, ukionyesha dalili za kuongezeka hali mbaya ya hewa, ikiwemo kuongezeka kimo maji ya bahari na dalili za kuyeyuka barafu kwenye milima barani Ulaya.

Mkuu wa WMO, Petter Taalas, anasema kadri joto linavyoongezeka, ndivyo athari zinavyozidi kuonekana katika mataifa mbalimbali duniani, ikienda kinyume na Mkataba wa Paris.

WMO inaeleza rekodi ya juu ya hewa ukaa, gesi ya methane, hewa ya nitrojeni ambazo ni kuu katika kuchafua hali ya hewa, huku upande wa pili kukiwepo maendeleo ya viwanda, ambavyo ni wazalishaji wa hewa chafu.

Inaeleza mifano ya milima ya Alps iliyopo Barani Ulaya, imeshuhudiwa kupoteza wastani wa kati ya mita tatu za unene wa barafu, huku nchini Uswisi theluji yote iliyeyuka kwenye msimu wa kiangazi, jambo linalotajwa kuwa mara ya kwanza katika historia tangu mwanzo wa karne iliyopo, barafu na theluji inasambaratika.

**PIGO RASMI LILIVYO**

Anafafanua kuwa, kuyeyuka kwa barafu duniani kote kunasababisha viwango vya kina cha bahari kupanda, jambo ambalo halikuwepo zaidi ya miaka 30 iliyopita.

Ni hali inayodhihirika siku chache zilizopita visiwani Zanzibar, ambapo maji ya bahari yalivamia makazi ya watu na kusababisha taharuki.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Dk. Selemani Jafo, akaagiza halmashauri zote kuhakikisha zinafikia malengo ya kupanda miti ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kiwango cha ongezeko la joto la bahari pia kimekuwa cha juu sana katika miongo miwili iliyopita, mawimbi ya joto baharini yanazidi kuongezeka, na viwango vya ongezeko la joto vinatarajiwa kuendelea katika siku zijazo," inasema ripoti ya kimataifa.

Vilevile utafiti huo unataarifu kuna athari za ukame na mvua nyingi, mfano katika mataifa ya Kenya, Somalia, na Ethiopia, sasa zikikabiliwa na upungufu wa mazao na uhaba wa chakula, kiwango cha mvua kikichangia.

Wizara ya Utalii ya Kenya, imeomba usaidizi wa kupatikana maji, nyasi na chumvi kuwasaidia wanyama waishi katika maeneo yaliyoathiriwa zaidi na ukame.

Waziri wa Utalii na Wanyamapori Kenya, Penina Malonza, anasema kuwa nchi hiyo imepoteza tembo 205 mwaka huu kutokana na ukame mkubwa zaidi, katika taifa hilo.

Waziri Penina, anasema maelfu ya wanyamapori wala mimea wamekufa mbugani na kwenye hifadhi za nchi, kutokana na ukosefu wa maji na malisho, akiainisha takwimu; nyumbu 500, pundamilia 400, twiga na nyati jumla yao 50.

Pia, inaelezwa zaidi ya theluthi moja ya eneo la Pakistan, sasa limekumbwa na mafuriko kati ya mwezi Julai na Agosti, hata imevunja rekodi ya mvua, wakazi wake milioni nane kuyahama makazi.

Ukanda wa Kusini Afrika nako kunatajwa kukumbwa na mfululizo wa vimbunga kwa miezi miwili mwanzoni mwa mwaka uliopo, huku Madagascar ikipata mvua kubwa na mafuriko.

Mnamo mwezi Septemba, Kimbunga Ian kilisababisha uharibifu mkubwa na kupoteza maisha ya watu Cuba na Kusini Magharibi mwa jimbo la Florida, Marekani.

WMO inasema sehemu kubwa za Ulaya ziligubikwa na vipindi vya kila mara vya joto kali, mfano nchini Uingereza, kuna rekodi mpya ya kitaifa mnamo Julai 19, joto lilifikia zaidi ya nyuzi 40 kwa mara ya kwanza.

Wakati dunia ikikabiliwa na majanga ya mabadiliko ya tabianchi na hali mbaya ya hewa duniani kote, Guterres amezindua mpango kazi katika mkutano wa COP27 ili kufikia lengo la tahadhari ya mapema kwa wote katika miaka mitano ijayo.

Mkuu huyo wa UN anaeleza kuwa mifumo ya tahadhari ya mapema ni muhimu ili kulinda watu na jamii kila mahali.

"Lazima tuchukue hatua dhidi ya ishara ya zahma kwa sayari yetu, kwa hatua kabambe na hatua za kuaminika za mabadiliko ya tabianchi. COP27 lazima iwe ndio mahali pakufanya hivyo na lazima iwe wakati wa sasa," anasema.

Mwisho



Miongoni mwa tembo waliokufa katika moja ya hifadhi nchini Kenya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Hali halisi ya athari ya ukame nchini Ethiopia.

MAZINGIRA

## KABRASHA LA COP 27

# Ajenda iliyohitimishia mada Jumapili na angalizo la wanazuoni Watanzania

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa Misri.**




Viongozi kutoka nchi wanachama katika Mkutano wa 27 wa Mabadiliko ya Tabia nchi , uliofanyika Sharm El Sheikh. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA**

BAADA ya mvutano wa takribani wiki mbili, kuanzia Novemba 6 hadi Novemba 20, Jumapili iliyopita, Mkutano wa 27 wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27) ukafungwa, jijini Sharm El Sheik, nchini Misri.

Hapo kuna makubaliano ya kupitishwa ajenda mbalimbali, ikiwamo ya kuwapo mfuko wa kusaidia majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabia nchi (Loss and damage) ili zilipe fidia kwa nchi zinazoendelea .

Ajenda nyingine zilizojadiliwa na kufikiwa muafaka ni ulazima wa kuzuia joto lisifike nyuzijoto 1.5 na ulazima wa nchi zinazeoendelea kutoa ahadi za pesa za kuchangia mfuko wa kuzisaidia nchi zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile kujenga visima vya kuhifadhi maji ya mvua, ili yatumike wakati wa ukame.

Ingawa uamuzi wa kutelekezamfuko huo utafanyika katika mkutano ujao, yaani COP 28, lakini kupitishwa kwake ni ushindi kwa nchi zinazoendelea kwa sababu ni moja ya ajenda sita walizozipigania usiku na mchana, ili zipitishwe ukizingatiwa kuwa ndio waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabianchi, huku mchango wao katika uzalishaji wa hewa ukaa ni asilimia 14 tu.

Kwa Tanzania, kupitishwa ajenda hiyo ni ishara ya mwanga wa matumaini wa kurudisha uhalishia wa mazingira yaliyokuwa hatarini kutoweka, kufuatia baadhi ya maeneo yameshaanza kuonja joto ya jiwe ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hapo kuna inayohusu maji ya bahari kuvamia makazi ya watu na kuwaacha wakiwa hawana sehemu za kuishi, pia kuvamia maji ya kunywa na kupikia Zanzibar.

Wakati hayo yakiendelea Zanzibar, Tanzania Bara nako hali ni tete, ukame umetawala na kusababisha maji kukauka kuingia kwenye mgawo wa maji na umeme, wanyama wanakufa kwa kukosa malisho, wengine wanadhoofika na kushuka thamani sokoni na kumwacha mfugaji katika lindi la umasikini.

**MSOMI WA UDSM**

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, anasema, kupitishwa ajenda hiyo, kunaonyesha kazi kubwa iliyofanywa na nchi zinazoendelea kuisukuma ajenda hiyo, lakini mbele kuna kazi kubwa waliyo nayo kuhakikisha inaelekezwaji.

Prof. Yanda, anasema nchi hizo zinatakiwa kujifunza kupitia mifuko kadhaa iliyoanzishwa katika Makubaliano ya Paris, ikiwamo kuzisaidia nchi masikini kuhimili athari za mabadiliko tabianchi (adaptation fund), ambayo utekelezwaji wake bado unasuasua, kwa kutokuwapo rasilimali.

"Ni vizuri kuwa ajenda hii imepitishwa, lakini haimaanishi kuwa kazi imemalizika, kuwa na mfuko ni jambo moja, kuwa na pesa ni jambo jingine, tuna mifuko mingi iliyoanzishwa chini ya makupaliano ya Paris.

"Karibu mifuko yote inapitia changamoto ya kutokuwa na rasilimali za kutosha, tunapokea ahadi nyingi lakini hazitekelezwi," anafafanua Prof Yanda, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa (IPCC ).

Anazishauri nchi zinazoendelea zitumie nguvu ile ile iliyoiumia, kuhakikisha ajenda iliyopitishwa kusimamia upatikanaji pesa hizo, ili uwafikie waathirika kwa wakati kwa sababu taarifa zinaonyesha kuwa ndani ya muda mfupi majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi yameongezeka maradufu, hivyo kuna idadi kubwa ya watu wamepoteza rasilimali zao na kurudi nyuma kiuchumi kufuatia athari hizo.



Prof Pius Yanda

"Swali la kujiuliza ni tunahitaji kiasi gani ili kufidia hasara zilizotokana na majanga ya athari za mabadiliko ya tabianchi, pia tunaweza kupata rasilimali kiasi gani, lakini ni njia gani zitatumika kuhakikisha kuwa hivi vitu vinapatikana, kwa sababu bado tuna jinamizi ya mifuko iliyopo ikiwamo.

" Nakukumbuka kwenye majadiliano yaliyofanyika mwezi Juni nchini Ujerumani, ilikuwa mfuko huu uwe ni rahisi kufikia watu , mara tu mtu anapoathirika alipwe fidia yake, " anafafanua.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika, (SACAU) Dk Sinare, anasema kama mfuko huo utafanya kazi inavyotarajiwa basi utakwenda kuboresha maisha ya watu, ikiwamo wakulima ambao wameathirika kiuchumi, kutokana na shughuli za kilimo kuzorota kwa takribani miaka mitatu mfululizo.

Aidha, anashauri utekelezaji wake uwe na usawa ukiangazia zaidi wanawake ambao ndio wazalishaji wakubwa wa chakula nchini na wahudumiaji wakubwa wa familia hivyo kujikuta wakiathiriwa zaidi na mabadiliko hayo ikiwamo kutembea umbali mrefu kutafuta maji kutokana na ukame, kuingia misituni kutafuta kuni za kupikia na kujikuta mikononi mwa sheria.

"Fedha hizo ziende kuwalipa fidia wakulima ambao karibu asilimia 75 ni wanawake, wengi wao wanakosa hata pesa ya kununua mbegu, kwa sababu hawajapata mavuno ya kutosheleza kuuza kwa muda mrefu.

"Wanachovuna wanaweka ndani kihudumie familia, lakini wengine wameuza hata hayo mashamba na kubaki wakiomba kwa ndugu, unaweza kuona namna walivyoathirika kisaikolojia," anasema.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Hamisi Hamza Hamisi, anaiambia Nipashe katika mkutano huo kuwa, ujio wa fedha hizo zitasaidia kuondoa msongo wa mawazo wa wakazi wa Zanzibar unaotokana na kuathiriwa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

"Fedha hizo tukizipata, badala ya kujenga madaraja tutarejesha uhalisia na kuwanusuru wananchi kuchanganyikiwa kutokana na kufikiwa na maji yasiyosalama.

"Pemba kule maji ya bahari yanaingia mitaani, kama unavyofahamu kuna baadhi ya kilimo hakistawi katika maji ya bahari, " anasema Hamisi.

**MWANANCHI**

Mzee Selemani, mkazi wa kijiji cha Mdimni, wilayani Mkuranga, anaeleza mataraji yake ni kwamba fedha ziwafikie hata wakaliwa fidia za nyumba walizopoteza, baada ya kuvamiwa na maji ya bahari na kuwasababisha kwenda kuishi nyumba za kupanga, hali inayowaongezea mzigo wa maisha.

"Unavyotuona hapa tuna miaka miwili tunaishi nyumba za kupanga, maeneo tuliojenga jumba yamevamiwa na maji ya chumvi na sasa kumekuwa fukwe," anadems Selemani na kuendelea:

"Maisha ni magumu, kwa sababu tumeingia mzigo wa kulipa kodi wakati tayari tulipambana kujenga nyumba ili kuachana na adha hii, lakini hata hiyo shughuli ya uvuvi ineyumba kwa sababu samaki wote wamekimbilia kwenye kina kirefu."

MAZINGIRA

KABRASHA LA COP27

# Kutoka kitendawili cha tabianchi hadi penye mwelekeo wa safari kuu mpya

**Na Nimi Mweta**



Wajumbe wa mkutano wa Umoja wa Mataifa wa COP27, wakiwa mkutanoni.

MKUTANO wa dunia wa mabadiliko ya tabianchi umemalizika Misri, kwenye jiji la starehe la Sharm El Sheikh, ambao baadhi ya maofisa wa Umoja wa Mataifa walidiriki kuutambulisha awali kama 'COP ya Afrika.'

Ni mkutano wa 27 katika mfululizo wa mikutano ya kimataifa ya kila mwaka ya mabadiliko ya tabianchi na inavyooelekea mkutano huu umekuwa na mafanikio tata, kuliko awali.

Labda kwa vile mazingira ya kimataifa nayo ni magumu zaidi, Afrika imevuna angalau, ila ilifanikiwa kupata saini za nchi tajiri zaidi kuhusu malengo muhimu.

Labda, viongozi waliohudhuria walikuwa wanajua kuwa suala hilo litakuwa ndiyo la mwisho la kufikia tamati ya mkutano huo, yaani kuwepo kwa mfuko wa dunia wa kufidia majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Yako matukio makubwa ya mabadiliko hasa kwa dhoruba kutoka baharini na kukaribia kuweka sehemu kubwa ya nchi, maeneo ya tambarare, chini ya usawa wa bahari. Vimbunga vya aina mpya ambavyo havikuwepo awali sasa vineonekana, kwingineko ni moto na joto.

Inahitajika uhakiki wa kina kujua ni kitu gani kinafuata kwani hitaji la mfuko wa dola bilioni 100 kufidia au kusaidia kutatua uharibifu unaotokana na mabadiliko ya tabianchi si jambo jipya.

Upo mfumo unaofanana kiasi fulani na hitaji la mfuko huo wa Dola za Marekani bilioni 100, ambazo ni ule wa 'biashara ya hewa haribifu' ambako nchi tajiri zinazozalisha hewa haribifu zinalipa fedha kwa nchi maskini zaidi (hazina viwanda vingi, hutoa hewa haribifu kidogo sana) ili kulinda misitu.

Hiyo Inaitwa 'carbon credits,' mapato kutokana na kunyonya hewa haribifu kutoka angani, kutokana na uwepo wa misitu mikubwa kadhaa.

Kuwepo mfuko wa kufidia uharibifu ni dhana ambayo imekuwa siyo rahisi kutetea, kwa sababu uharibifu huo umezikubwa nchi takriban kote kwani vimbunga hutokea kila mahali, havichagui nchi tajiri au maskini.

Hoja hiyo insingekuwa rahisi kumezwa na nchi maskini, kwa sababu uharibifu unatokana na hewa chafuzi kutoka nchi tajiri, hivyo kutokuukubali mfuko huo, ni sawa na kukana uhusika huo.

Pia, ni sawa na kusema hakuna haja ya ushirikiano wa dhati kuhusu suala hilo, na kila nchi 'ipambane na hali yake' kwa masuala ya mazingira. Ingekuwa balaa.

Tatizo mojawapo muhimu ambao lingetokana na kuweka msimamo wa aina hiyo ni kuwa nchi tajiri, pia zinataka nchi maskini zaidi kuchukua hatua za aina moja au nyingine katika masuala ya mazingira, na hata ya kijamii au kisiasa ili kutuliza uhamiaji kinyume cha sheria.

Wengi kati ya wanaotaka au wanaofurika kuhamia Ulaya na Marekani kwa upande wa pili wa Bahari ya Atlantiki hasa ni 'wahama tabianchi,' wanaokimbia ukame na kukosa kazi katika nchi nyingi. Ukame na kukosa kazi husababisha shinikizo la ubongo, kujitosa kuhamia mbali.

Ila zipo sababu maridhawa katika ngazi ya mtu binafsi kumfikisha kuchukua uamuzi wa kujitosa katika safari hatari za kuvuka bahari, ila tatizo hilo kwa kumla limeanza kuziathiri nchi za Magharibi kwa jumla.

Vyama vya sasa kali za kizalendo vinavyoingia madarakani 'kuokoa' nchi hizo kutokana na janga la uhamiaji ambao chimbuko lake mara nyingi ni vita vya kutaka demokrasia (katika mazingira ya kutoelewana kidhehebu) visivyoisha Mashariki ya Kati.

Ila ndani ya mzozo huo kiwingu cha kubarikika uchumi, ambako kunaharibu matumaini ya watu na kuchochea uhamiaji kama suluhisho.

**NENO LAKE SAMIA**

Akihutubia mkutano huo katika hotuba za kwanza ambako kila nchi ilitoa tathmini yake mbele ya wajumbe wote, Rais Samia Suluhu Hassan, akaelekeza hisia zake katika kuundwa kwa mfuko huo.

Ziko nchi kadhaa tajiri ambazo tayari zilikuwa zimepinga mpango huo, kwa maana kuwa kila nchi ina aina moja au nyingine ya majanga ya tabianchi, kwa hiyo mahitaji ya aina hiyo inabidi yaoanishwe na 'madirisha' ya mikopo ya dharura ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, kama ilivyokuwa wakati wa janga la Uviko-19.

Hakukuundwa mfuko maalum wa dunia nzima, ila bodi ya wakurugenzi wa mashirika hayo, ilibuni njia za kutoa mikopo isiyo na riba kwa nchi nyingi kukabiliana na athari za janga hilo.




Wanaharakati nao wakiwa mstari wa mbele kufikisha salamu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Ila wazo hilo likakubaliwa kwa sababu, hapakuwapo na kitu kingine cha kuunganisha nchi zilizohudhuria kwa tamko la kuhitimisha mkutano linaloweza kuchangia hisia ya afueni nchi nyingi duniani.

Ambacho hasa kingeendana na mkutano huo na hapakuwa na mazingira ya kufikia maamuzi ya pamoja ni kuweka mkakati wa kuondoa kabisa matumizi ya makaa ya mawe, wazo lililoungwa mkono mkutano wa mwaka jana Glasgow, Scotland kabla ya vita vya Russia nchini Ukraine.

Kuanzia pale biashara ya gesi asilia kati ya Russia na nchi za magharibi ilipovurugika, zimebidi zianze tena kutumia makaa ya mawe kwa wingi, kiasi ambacho Tanzania imeanza mipango sio haba ya kuuza makaa ya mawe nchi za nje.

Ni jambo lililokuwa nadra kutajwa kabla na hata mipango ya kujenga mtambo kuzalisha umeme wa megawati 600 kwa kutumia raslimali hiyo ulikwama kwa zaidi ya miaka 20, kuanzia pale gesi asilimia ilipogunduliwa kueleleka mwaka 2000.

Sasa mauzo ya gesi yanatazamiwa kupanda na hata makaa ya mawe yanapata soko Ulaya, kwani 'pakacha likivuja nafuu ya mchukuzi.' Mkutano uliopita hilo lingezua mzozo, sasa hakuna jinsi!

AFYA

# Anayetaka kuwa baba baada ujana, hii hapa hatari anayomwachia mtoto



Mume na mke 'mama kijacho' wa nchini Afrika Kusini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA utaalamu wa afya, inaelezwa pale wanaume wanapoamua kuwa wazazi baada ya miaka 35 ambao tayari kishavuka ujana, wanakabiliwa na uwezekano wa hatari ya kupata watoto wanaozaliwa kabla ya muda wao wa kuzaliwa au wenye hali ya usonji.

Pia kila mwaka unaokwenda, mbegu za uzazi za kiume unatajwa kwamba unapopungua kwa kiasi kikubwa kwa wingi na ubora wake, jambo linaloweza kuhatarisha uwezo wao wa kuendeleza kizazi.

Haya yamebainishwa na tafiti kadhaa zilizofanywa katika miaka ya hivi karibuni, ukiwamo utafiti uliofanywa na Kitivo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Stanford University, nchini Marekani, ambacho kimetathmini taarifa za wazi zaidi ya milioni 40.

Kuhusu uzazi na taarifa kuhusiana na hali hiyo, habari njema pia ni kwamba kuna mapendekezo ya vipimo na tiba, ambavyo inaweza kufuatilia kwa karibu na kupunguza hatari kwa mtoto mchanga ya 'kijacho.'

Dk. Karla Zacharias, mtaalamu aliyebobea katika masuala ya uzazi wa binadamu na mjumbe timu teule ya kutafiti tiba, anaeleza kwamba kila mara hupokea wanaume katika ofisi yake ambao wangependa kuwa na watoto.

"Ninawapokea wagonjwa wenye miaka 50 na 'ushee' na 60 na 'ushee' ambao wanawaoa wanawake vijana, ambao wanataka kupata ujauzito, anasema.

Swali ambalo huwa wanauliza kwa wanaowatibu ni kwamba "ni zipi hatari za baba mwenye umri mkubwa?" Anasema, kwa ujumla mfumo wa uzazi wa mwanaume hutenda tofauti na ule wa wanawake.

Huku wanawake wakiwa na ukomo wa idadi ya seli za uzazi, kwa wanaume utengenezwaji wa mbegu za uzazi ambao huanza katika kipindi cha kubalehe huendelea katika kipindi chote cha maisha yao.

Anasema hapo ndipo penye jambo muhimu linalojitokeza, ingawa uzalishaji wa mbegu za uzazi haukomi, ubora wa mchakato huu hauwi sawa baada ya umri fulani.

Kadri miaka inavyokwenda, anasema ni jambo halisi kwamba seli hizo hutengenezwa kwa kiwango kidogo zaidi na huwa na kasoro zaidi.

Anasema matokeo ya kasoro hizo zinaweza kuzuia utungwaji mimba na baadhi ya tafiti zinaonyesha kuwa hata wakati wanapofanikiwa kuwa na uwezo wa kutungisha mimba, mtoto mchanga anakuwa katika hatari kupata matatizo ya kila mara kiafya kuanzia, kasoro na mfumo wa kupumua hadi usonji.

**KINABABA MFUATILIE**

Mbegu za kiume huendelea kutengenezwa pasipo kukoma kuanzia kipindi cha balehe na utafiti uliofanywa mwaka 2018 na Chuo Kikuu cha Stanford cha Tiba, ulibaini kwa ujumla, kadri mwanaume anavyoendelea kuwa na umri mkubwa, ndivyo ndivyo mtoto anavyokuwa na uwezekano wa harari ya kuzaliwa akiwa na kasoro za kiafya.

Wanaume wenye watoto baada ya umri wa miaka 35, wana uwezekano wa juu zaidi wa watoto wao kuzaliwa wakiwa na uzito wa chini wa mwili kuwa na kifafa, au kuhitaji kuongezewa hewa ya kupumua muda mfupi baada ya kuzaliwa.

Anaeleza kuwa wenye umri wa zaidi ya miaka 45 wana uwezekano kwa asilimia zaidi kupata watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya muda wao kufika na wale wenye zaidi ya umri miaka 50, wana uwezekano wa asilimia 28 zaidi, watoto wao wanazaliwa kuhitaji kuwekwa katika Kitengo cha Uangalizi Maalum kwa muda.

Katika chapisho hilo, Profesa Michael Eisenberg, wa Masuala ya Uzazi na Mkuu wa Utafiti huo, anabainisha kwamba idadi hiyo haipaswi kutafsiriwa kama kitu cha kutisha.

Anaelimisha jamii kwamba, matokeo ya utafiti huo yanapaswa kuzisaidia familia kupanga vyema na kufuatilia afya yao ya uzazi kadri inavyopaswa.

Katika hitimisho la utafiti huo, kunabainishwa kuwa, kwa kila miaka 10 ya ongezeko la umri wa baba, kuna nafasi asilimia 21ya fursa ya ziada, kwamba mtoto ataugua kutokana na hitilafu, zinazohusiana na ugumu wa kuwasiliana, mwingiliano ya kijamii na kitabia.

2.

**SABABU NINI?**

Kupungua ubora wa mbegu za uzazi za kiume, bado idadi ya seli za uzazi na uimara wake una nafasi katika nguvu za kutungisha mimba kupunguza hatari za kiafya za mtoto, anaeleza Dk. Alfredo Canalini, Rais wa Chama cha Madaktari wa Uzazi cha Brazil.

"Baioloji ya mfumo wa uzazi wa kike, unategemea na mtu binafsi wa kiwango cha juu na mwanaume anahitaji ushauri wa daktari kuelewa ni nini kinachoendelea na kipi kinapaswa kufanyika," anasema.

Anawaambia wanaume wanaotaka kuwa baba wazee wanapaswa kupima uzito wa kumkuza mtoto na shauri huo ni sharti kumhusisha daktari wa kawaida au daktari wa uzazi.

Pia anawashauri kuwa ni tathmini inayoweza kufanywa mara moja kila mwaka wakati panapokuwapo dalili, kama vile kukasirika kusiko kawaida, ugumu katika kupata ari ya kujamiiana au kupatwa na ari hiyo kwa kipindi kifupi, pamoja na kushindwa kutungisha mimba.

- ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***



Mwanamke mmoja mzee mwenye miaka 68 nchini Nigeria amejifungua watoto pacha na kuwaacha wengi na mshangao. Bibi huyo alijifungua katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Lagos.

FUATILIA MKASA WA MAZINGIRA...

# Kenya yaruhusu mibuyu kukatwa iuzwe nje, kisha yacharuka kuzuia

**NAIROBI, KENYA**

WANAMAZINGIRA wana wasiwasi kuhusu athari mbaya za kukata miti ya mbuyu. Inaelezwa, tangu jadi, mti wa mbuyu umekuwa ukitumika kama sehemu ya kuendeleza maombi na tambiko kwa jamii tofauti katika maeneo ya Pwani ya Kenya.

Hata hivyo, siku za hivi karibuni mjadala umeibuka baada ya kubainika kuwa miti hiyo imekuwa ikikatwa au kung'olewa na kuuzwa nje ya nchi, katika hali ya kutatanisha, ambayo imewatia wasiwasi wanamazingira nchini.

Inadaiwa, katika uamuzi huo hakuna mashauriano wala uchunguzi uliofanywa kutathmini athari za ukataji miti hiyo kwa mazingira yao yanayowahusu.

Kutokana na malalamiko hayo, serikali ya Kenya imefuta leseni iliyotolewa kwa kampuni ya kigeni ya kung'oa na kuuza nje miti ya mbuyu, kutoka maeneo ya pwani, ambako miti hiyo imestawi.

Waziri wa Mazingira, Soipan Tuya, anasema kampuni ya Georgia ilinunua miti minane mikubwa kutoka kwa wakulima wa ndani, ikapatiwa idhini ya kuing'oa.

Kwa mujibu wa waziri huyo, miti mibuyu ina uwezo wa kuishi hadi miaka 2,500 na hivyo uamuzi wa kuruhusu ing'olewe haukuzingatia vigezo vinavyohitajika.

Inaelezwa, Idara ya Misitu nchini Kenya (KFS) ilitoa kibali cha kung'olewa kwa miti, kutoka hiyo kufuatia idhini ya Mamlaka ya Kitaifa ya Kulinda Mazingira, mnamo Oktoba 2, mwaka huu.



Mti wa mbuyu ulioko nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO.**

Baadhi ya wakulima katika eneo la Kilifi mkoani Pwani ya Kenya, waliripotiwa kutaka kusafisha ardhi yao ili kupanda mahindi na wengine wakiripotiwa kuonyesha nia ya kufanya biashara, baada ya mamlaka husika kutoa cheti cha kuendesha mpango huo.

Waliuza miti iliyokua katika ardhi yao ya kibinafsi kwa kati ya Dola za Marekani 800 (zaidi ya Sh.milioni 1.8) na Dola 2,400 (zaidi ya Sh. miliOni 5.6).

Haijulikani miti hiyo ilikuwa na umri gani, lakini picha zinazoshirikiwa mtandaoni zinaonyesha miti iliyong'olewa yenye vigogo na matawi makubwa ya miti.

Mamlaka ya kitaifa ya Kulinda Mazingira (NEMA) baadaye ikawasilisha kesi mahakamani kupinga mchakato huo, baada ya kugundua miti hiyo ilikuwa ya kuuzwa nje ya nchi.

Mratibu wa Mradi wa Kuhifadhi eneo la Pwani, Francis Kagema ,ambaye pia ni mmoja wa wahifadhi wanaopinga kung'olewa au kukatwa kwa miti hiyo, akanukuliwa akisema:

"Huu ni unyakuzi kwa sababu hiyo ni rasilimali yetu ya kibaolojia. Mtu anang'oa na kuipeleka nchi nyingine. Hatujui ni nani aliyeruhusu hilo na mchakato uliohusika kwa sababu hapakuwa na mashauriano,"

Kagema akatoa wito kwa NEMA na Huduma ya Ukaguzi wa Afya ya Mimea (Kephis) kufafanua jinsi wageni hao waliruhusiwa kuingilia rasilimali asili ya Kenya.

"Tunahitaji kujua kilichotokea kwa sababu huwezi kwenda Marekani, kung'oa mti na kuja nao Kenya. Nani atakuruhusu kufanya hivyo?"aliongeza kusema

### HATUA YA KISERIKALI

Katika taarifa ya kufuta leseni ya kampuni hiyo ya kigeni, Wizara ya Kilimo ilisema kwamba, mchakato huo unahitajika kufanywa kwa njia ya uwazi na mpango wa kugawana faida na jamii, pia uwekwe wazi.

Kwa sasa wizara hiyo imeagiza Mamlaka ya Uchukuzi na Misitu kufuta kibali cha kilichoruhusu usafirishaji miti hiyo kutoka sehemu iliyokatwa, pamoja na usafirishaji wake nje ya nchi, huku ikisubiri kutathminiwa upya kwa mkataba huo.

"Tumekubaliana kwamba miti ya mibuyu isisafirishwe nje ya nchi hadi makubaliano kati ya wahusika yaratibiwe ipasavyo," Waziri wa Mazingira na Misitu, Tuya anasema.

*Kwa mujibu wa BBC.*


---

Dondoo: Kulia
1. Msaidizi wa Mungu
6. kinga
7. eleza
8. magoli
10.bara la pili kwa ukubwa
13.filimbi
14.jina la kale Afrika mashariki
15.sujudia mtu kwa kuinamisha kichwa 17.kinywani
20.wingi wa mlei
21.epusha mtu na janga
22.huzaa ndizi

Chini:
1. Mtu asiyekuwa na dini
2. Monrovia ni mji wake mkuu
3. chukua bila ruhusa
4. usawa juu ya ardhi
5. Mji mkuu wa Tanzania
8. mimea
9. shina la kuti 11. tenda
12.mtu asiyesikia maagizo
16.tendo la kumega
18.jimbo
19.oana kwa mke na mume

## CHEMSHABONGO NA -00 22 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

UHALIFU
MAKINI
ABELI
LILIGA
IGIZA
MZAZI
ARAKA
IRANI
AZIMIO
CHAKI
MHAYA
AMINI
TAMAA
KANYA

HADI
IASI
HABA
AGA
GAMU
AKUA
AUA
AMU
ONJA
DAU
KOMAA




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | U | S | A | | B | E | B | W | A |
| U | S | A | W | A | | | I | | J |
| T | I | M | A | M | U | | A | L | A |
| u | K | A | L | I | | | S | | B |
| | U | D | I | N | I | | H | A | U |
| | | I | | I | S | H | A | | |
| | B | | I | S | H | A | R | A | |
| M | A | R | A | H | A | B | A | | M |
| | B | U | S | A | R | A | | | R |
| K | A | D | I | | A | R | A | K | A |
| | | I | | | | I | | | O |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | A | L | A | K | I | | | B |
| A | M | A | L | I | | K | A | A |
| M | I | L | A | N | G | O | | N |
| A | N | A | S | A | | M | | D |
| K | A | M | I | S | H | E | N | I |
| O | | I | R | A | | S | A | A |
| | A | S | I | | A | H | A | |
| U | | H | | U | T | A | M | U |
| S | H | A | I | R | I | | | M |
| O | | | | U | A | N | G | A |



# Ushirikiano Mbeya, Zurich waleta manufaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

USHIRIKIANO kati ya Jiji la Mbeya na Jiji la Zurich la nchini Uswisi, umeanza kuleta manufaa kwa jamii baada ya kuanzisha mradi wa pamoja wa kuimarisha mifumo ya chakula ili kukabiliana na tatizo la udumavu.

Mradi huo ulizinduliwa juzi jijini hapo kwenye mkutano maalumu ambao uliwashirikisha watendaji wa majiji yote mawili, maofisa lishe wa jiji la Mbeya na wa shirika lisilokuwa la kiserikali la HELVETAS ambalo liliwezesha kuwapo kwa ushirikiano huo.

Naibu Meya wa Jiji la Mbeya, Kefas Mwasote, alisema mradi huo unalenga kuimarisha hali za wananchi katika upatikanaji wa lishe bora kwa wananchi kuanzia uzalishaji mpaka ulaji.

Alisema mradi huo unalenga kuhakikisha wananchi wanapata chakula chenye mchanganyiko unaotakiwa ili kuhakikisha wanaondokana na matatizo yatokanayo na lishe duni.

Kwa mujibu wa Mwasote, mbali na majiji hayo kushirikiana katika lishe, pia yanashirikiana katika masuala ya utawala hasa watendaji kubadilishana uzoefu wa kazi.

"Tunawashukuru wenzetu wa Zurich kwa kukubali kushirikiana na sisi kwenye mambo mbalimbali lakini kwa uzito, hili la chakula tunaamini litatusaidia kupunguza tatizo la udumavu kwa watu wetu," alisema Mwasote.

Alisema watahakikisha wanaweka mifumo mizuri ya uongozi ndani ya jiji hilo ili kuhakikisha ushirikiano unaoendelea baina ya majiji hayo mawili unaendelea kwa faida ya wananchi.

Mratibu wa Mradi kutoka HELVETAS, Agnes Mahembe, alisema mradi huo wa ushirikiano katika masuala ya lishe kwa majiji hayo ambao unajulikana kama 'Inclusive Cities For Nutrition' (IC4N) una thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.9. Alisema afua mbalimbali zitakuwa zinatekelezwa kwa wananchi wa Jiji la Mbeya na kwamba mradi huo unatekelezwa mjini kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi kwa sasa wanaishi mjini.

Mahembe alisema HELVETAS kupitia programu yake ya Kilimo Bora kwa Wanawake na Vijana (KIBOWAVI), inatekeleza miradi mbalimbali katika Jiji la Mbeya ikiwamo uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

"Tumeanzisha huu mradi ili kuwa na mwendelezo mzuri wa kazi ambazo tumekuwa tukizifanya. Tumejenga kiwanda cha kusindika mazao hapa, hivyo tutakitumia kiwanda hiki kwenye mwendelezo wa kuboresha lishe," alisema.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, ambaye alishiriki kwenye uzinduzi huo, alisema mradi huo utasaidia kukabiliana na matatizo ya lishe katika jiji hilo kwa sababu unalenga kubadili mifumo ya maisha ya watu ikiwamo mifumo ya ulaji.

Alisema katika mradi huo pia wananchi watafundishwa namna sahihi ya uandaaji wa chakula kuanzia kwenye uzalishaji mpaka kwenye ulaji ili wawe na afya njema.

Alisema utafiti uliofanyika mwaka 2018 ulionyesha kuwa kiwango cha udumavu kwa wananchi mkoani Mbeya ni asilimia 33.8 jambo ambalo alisema si hali nzuri na linahitaji miradi mingi ya aina hiyo kwenye kukabiliana nalo. Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, aliushukuru uongozi wa jiji la Zurich na HELVETA kwa kukubali kushirikiana nao kwenye jambo hilo kwa maelezo kuwa wananchi watasaidiwa.




Mkurugenzi wa Shirika la HELVETAS Tanzania, Felix Bachmann, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa kuimarisha mifumo ya chakula kwa wananchi wa Jiji la Mbeya, unaotekelezwa kwa ushirikiano na Jiji la Zurich la nchini Uswis, jijini humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 'Dharura Fasta' kurahisisha maisha kwa wananchi Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa halmashauri 10 za mikoa ya Mbeya na Songwe, wameunganishwa na huduma ya 'Dharura Fasta' inayotekelezwa na Shirika la Kusimamia Huduma za Afya na Bima (HIMSO) kwa lengo la kuwasaidia kupata huduma za usafiri wakati wa dharura za kiafya.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Fadhili Mtanga, aliyasema hayo juzi jijini hapo wakati wa kikao baina ya waandishi wa habari na menejimenti ya HIMSO kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya miaka 10 tangu walipoanza kutoa huduma.

Alisema huduma hiyo inatekelezwa katika halmashauri zote za mkoa wa Songwe na tano za mkoa wa Mbeya hasa katika maeneo ya vijijini ambako huduma za usafiri hupatikana kwa shida inapotokea dharura. Mtanga alisema shirika hilo linawaunganisha wananchi hao na huduma za usafiri wa vyombo ambavyo vya watu binafsi na vinavyonunuliwa na shirika hilo ili kuwasaidia kufika haraka hospitalini wanapokuwa wanatakiwa kufika kwenye vituo vya afya.

Alisema wanalenga zaidi maeneo hayo ya vijijini kwa sababu ndiko kwenye shida kubwa ya afya kwa wananchi hasa kwa wajawazito ambao alisema huwa wanafariki dunia ama kupata matatizo ya uzazi kwa kukosa huduma za usafiri wa dharura. "Tumehamasisha wananchi katika vijiji vyote vya maeneo tunayotekeleza mradi huu, yako maeneo ambayo yapo mbali na huduma za afya na hivyo huwa yanatakiwa kupata huduma kama hizi," alisema Mtanga.

Mwenyekiti wa Bodi ya HIMSO, Charles Mbwanji, alisema shirika hilo lilianzishwa mwaka 2012 kwa lengo la kuboresha afya za wananchi na kwamba awali lilikuwa linafanya kazi katika wilaya ya Mbozi pekee kabla mkoa wa Mbeya haujagawanywa.

Alisema baadaye walianza kupanua mipaka na kuingia katika halmashauri zingine za mkoa wa Songwe na hatimaye katika mkoa wa Mbeya ambako wameanza katika Halmashauri zote za pembezoni isipokuwa Kyela.

Kwa mujibu wa Mbwanji Alisema mbali na shirika hilo kusafirisha wagonjwa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, pia linasafirisha miili ya marehemu kutoka hospitalini mpaka nyumbani inapotokea amefariki dunia. "Mpango huu ni endelevu na unajiendesha wenyewe, tunafanya kazi kwa kushirikiana na watoa huduma wa afya ngazi ya jamii ambapo wanaunda kamati maalumu za usimamizi ngazi ya vijiji zijulikanazo kwa jina la 'CHUA,'" alisema Mbwanji.

## Atembeza bakuli ujenzi ofisi chama

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ALIYEKUWA Diwani wa Ndato katika Halmashauri ya Rungwe mkoani Mbeya kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Paulos Zambi, amewaomba wadau wa maendeleo kuchangia ujenzi wa ofisi ya chama hicho unaoendelea katika kata hiyo ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

Ombi hilo alilitoa juzi wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi huo huku akisema wanahitaji kupata Sh. milioni 17 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo na kwamba ofisi hiyo imejengwa na wanachama wa kata hiyo kwa nguvu zao.

Alisema wamekuwa wakichangishana kwa nyakati tofauti na kwamba mradi ulikwama miaka miwili iliyopita baada ya yeye mwenyewe kama mhamasishaji kuswekwa rumande kwa sababu ambazo hakuziweka wazi.

"Wananchi wa eneo hili wamekuwa wakiuza mazao yao na mifugo kwa ajili ya kuchangia mradi huu, kwa hiyo hapa tulipofikia tunahitaji nguvu za ziada ili tukamilishe, tunawaomba wadau mbalimbali watuunge mkono," alisema Zambi.

Naye aliyekuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Rungwe kupitia CHADEMA, John Mwambigija, alisema ofisi za chama ni muhimu kujengwa kwa kuwa zinasaidia kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema Kata ya Ndato imeonyesha mfano mzuri kwenye ujenzi wa ofisi za chama kwa kuwa ni miongoni mwa kata ambazo wanachama wa chama hicho wanajitolea kwenye shughuli za chama.

Mwambigija alisema kwa sasa katika Jimbo la Rungwe kuna kata nyingi lakini ambazo zinaongozwa na madiwani wa chama hicho ni kata mbili pekee ambazo ni Kiwira na Swaya.



# Arusha kidedea usafi mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imeutaja mkoa wa Arusha kuwa kinara kwenye mashindano ya afya na usafi wa mazingira nchini kwa mwaka 2022 huku Morogoro ikifanya vibaya zaidi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Seif Shekalaghe, aliyasema hayo jijini hapo hivi karibuni kwenye kilele cha Wiki ya Usafi kitaifa na maadhimisho ya Siku ya Matumizi ya Choo Duniani.

"Ni matarajio ya wizara washindi wote wataendeleza hali ya usafi ambayo tuliiona katika kipindi cha miezi minne iliyopita na kwamba upande mwingine wale ambao hawakufanya vizuri wanayo nafasi ya kuboresha mapungufu yaliyobainishwa kwenye taarifa ya mashindano ambayo itatolewa na wizara hivi karibuni," alisema.

**Halmashauri za Wilaya Njombe imepata asilimia 97.8 huku Itigi ikipata asilimia 35.3.**

Alisema wasibweteke katika suala la usafi na kuwahimiza kuinua kiwango cha usafi katika maeneo yao kwa kuwa ndio msingi wa kuanzishwa kwa mashindano hayo.

"Kundi la Halmashauri za Majiji, Mshindi wa Tatu: Halmashauri ya Jiji la Tanga (80%), Mshindi wa Pili: Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (81%). Mshindi wa Kwanza: Halmashauri ya Jiji la Arusha (85%) na nafasi ya mwisho katika kundi hili imeshikwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambayo imepata asilimia 56," alisema.

Kuhusu la Halmashauri za Manispaa alitaja Shinyanga imeongoza kwa asilimia 87 huku nafasi ya mwisho ikishikwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliyopata asilimia 44.

"Kundi la Halmashauri za Miji ni Babati imepata asilimia 77 huku nafasi ya mwisho imeshikwa na Halmashauri ya Mji wa Ifakara iliyopata asilimia 25,"alisema.

Kadhalika, alisema kwa Halmashauri za Wilaya Njombe imepata asilimia 97.8 huku Itigi ikipata asilimia 35.3.

Akizungumzia kundi la vijiji alitaja kijiji kinara cha Image, Kata ya Kidegembye Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kupata asilimia 98 huku Kijiji cha Kiwege Wilaya ya Morogoro kikishika nafasi ya mwisho kwa kupata asilimia 27.

"Kundi la Shule za Msingi vijijini ya kwanza ni Kimashuku wilayani Hai imepata asilimia 96.5 huku nafasi ya mwisho imeshikwa na Shule ya Msingi Njage, Kata ya Mchome, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, Morogoro kwa kupata asilimia 17.5. Kundi la Shule za Sekondari za bweni ni shule ya wasichana ya Nyankumbu imepata asilimia 98 huku Shule ya Sekondari Sumbawanga ikishika nafasi ya mwisho kwa kupata asilimia 36," alisema.



Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Gilberty Moga, akizungumza wakati akifungua semina ya fedha, utawala bora na uwajibikaji kwa mamlaka za serikali za mitaa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watumishi kikwazo ukusanyaji mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Umma imesema watendaji wa serikali wasio waaminifu katika ukusanyaji mapato ni kikwazo katika kufikia malengo.

Pia imewakumbusha waajiri kuzingatia taratibu kanuni na sheria pindi mtumishi anapofanya kosa ili kuacha kufanya maamuzi kinyume na miongozo ya utumishi wa umma.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Hamisa Kalombola, alitoa kauli hiyo jana katika ziara yake aliyoifanya wilayani Bahi.

Jaji Kalombola alisema mtumishi wa umma ni lazima aweke mbele maslahi ya nchi ili fedha wanazokusanya ziwe kwa matumizi binafsi bali nchi nzima.

"Tumekuwa tukipambana na hali hiyo kwani kuna mashine ambazo zinatumika sasa kumekuwa na kasoro tumekuja kuzigundua."

"Unakuta wamefikishwa kwenye mamlaka ya nidhamu kutokana na kasoro ambazo zingeweza kuzuilika na hii inatokana na makusanyo yanakusanywa. Halafu fedha zinabakia kwa mkusanyaji wengine siku tatu mpaka nne kama binadamu wanajikuta wanaingia katika matatizo," alisema.

Alisema lengo la ziara hiyo wilayani Bahi ni kuwasisitizia watumishi matumizi mabaya ya fedha za serikali yanaweza kuwapeleka katika shida.

"Tumekuja kusisitiza kuhimiza cha msingi ni kuwa mwaminifu na huu ni wito kwa ajili ya wakusanya mapato wote Tanzania nzima," alisema.

Kadhalika, alizikumbusha halmashauri kuzingatia sheria, taratibu na kanuni pale ambapo mtumishi anabainika kufanya kosa.

"Nasisitiza taasisi na halmashauri wanapomshughulikia mtumishi inatakiwa wafuate taratibu na kanuni. Na inatakiwa ifanywe hivyo hata sisi tusibaki kuwa na majalada mengi ambayo yalikuwa hayana haja ya kufika kwetu.

"Waajiri wazingatie hizo taratibu kanuni na sheria na watumishi wafanye kazi sio kwa mazoea wafanye kwa kufuata taratibu na kanuni," alisema Jaji Kalombola.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Athumani Masasi, alisema waendelea na ukusanyaji wa mapato na kazi yao kubwa ni kuhakikisha wanadhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato.

"Kwa mfano ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine unahitaji uaminifu na uadilifu mtu anaweza asikate kama ambavyo amepaswa kukata.

"Na akakosa uaminifu kazi yetu kubwa tunafanya ukaguzi mara tunapokutana na watu wa namna hiyo hana risiti sahihi sisi tunapiga faini lakini huyu ambaye hakukata risiti nae tunaweka utaratibu wa kuwachukulia hatua," alisema.

Kamishna wa Tume hiyo, Balozi Adadi Rajabu, alisema kumekuwa na rufani nyingi ambazo watumishi wamefukuzwa kutokana na ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa mashine za POS.

# Serikali na wadau kushirikiana malezi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kusimamia suala la malezi ya mtoto kwa kuhakikisha wanafikia hatua ya ukuaji timilifu.

Akizungumza jana kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwenye uzinduzi wa mradi wa malezi awamu ya tatu kupitia Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi na Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto uliofanyika jijini hapa, Mariam Nkumba, alisema lengo la mradi wa malezi awamu ya tatu ni kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kupitia vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema Ofisi ya Rais –TAMISEMI itaendelea kusimamia suala la usimamizi wa malezi ya mtoto kwa kuhakikisha wanaimarisha utoaji wa huduma za elimu na afya msingi kwa kuweka miundombinu rafiki na inayotosheleza kwa wananchi.

Kuhusu upatikanaji wa takwimu sahihi katika usimamizi wa watoto, alisema TAMISEMI itaendelea kuweka takwimu na taarifa sahihi za utekelezaji wa mradi kufikia lengo na kuwajengea uwezo watumishi kwenye fani za afya, ustawi wa jamii pamoja na kutoa mafunzo kwa kamati zinazoshughulika na huduma za malezi.

Awali, akimwakilisha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Nandera Mhando, alisema uwepo na uhusiano mzuri kati ya serikali na wadau kutachangia kwenye jitihada za kutoa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto na kuhakikisha wanakuwa kwenye mweleko sahihi wa kufikia ukuaji timilifu.

# SMZ yajizatiti kurejesha minazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kuimarisha kilimo cha nazi na kurudisha katika enzi zake za miaka ya 1960 huku ikipiga marufuku ukataji wa minazi kwa matumizi mingine yakiwamo mbao.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakar Hamad Bakar, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Bakar alitaka kujua mikakati ya wizara katika kuimarisha zao hilo nchini.

Khamis alisema katika mwaka 2019 wizara ilitayarisha Sera ya Taifa ya Minazi ya mwaka 2020 na sehemu ya kanuni zake ni uimarishaji wa zao hilo ili kurudisha hadhi ya zamani.

Alisema wizara imeweka mikakati katika kipindi cha mwaka 2020- 2025 kuotesha minazi 500,000 kwa mwaka kwa wakulima na wananchi wa kawaida.

Alisema hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ambayo imejikita katika kuimarisha mazao maarufu ya asili kwa ajili ya mageuzi ya kibiashara.

Pia alisema utafiti wa mwisho wa sensa ya miti ya Zanzibar uliofanyika mwaka 2013, ulionyesha imeonyesha kuwapo kwa minazi milioni 3.5 kulinganisha na minazi milioni 5.2 iliyokuwapo mwaka 1992.

Alisema wizara kupitia Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu Na. 10 ya mwaka 1996, imetoa ruhusa ya kukata miti hiyo kwa kibali maalumu ikiwamo miti ambayo iko katika tishio na kusababisha madhara kwa binadamu.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu kuona kwamba tunarudisha zao la asili la minazi na kuligeuza la kibiashara kwa ajili ya kutoa kipato kikubwa kwa wananchi wetu," alisema.

Khamis alisema wamejipanga kuimarisha vitalu vya miche ya minazi vinavyomilikiwa na serikali pamoja na watu binafsi ili kuona uzalishaji unakwenda katika malengo yaliyokusudiwa.

Alisema wakulima binafsi watapewa elimu ambayo itawawezesha kuendesha vitalu hivyo kwa mafanikio makubwa ili kufikia malengo ya kuzalisha miche ya minazi ya aina mbalimbali.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi wa Shirikisho la Somali nchini Tanzania, Zahra Ali Hassan, alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

# Waziri achagiza elimu kwa maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema ili kupiga hatua katika maendeleo ya kiuchumi lazima kwenda sambamba na mabadiliko ya kielimu yanayoendelea duniani kote.

Amesema teknolojia imekuwa ikibadilika kwa kasi kubwa, hivyo uendeshaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali za kijamii nao umebadilika sana.

Waziri Hamza aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakili, Kikwajuni Zanzibar, wakati akifunga mafunzo ya udhibiti wa uhamaji na mabadiliko ya kiuchumi, changamoto na fursa kwa watendaji wa Idara ya Uhamiaji na taasisi zingine zinazoshughulikia wahamaji.

Uhusiano na ushirikiano baina ya nchi na nchi, alisema vimekuwa vikibadilika kwa kasi, hivyo warsha hiyo ina umuhimu mkubwa katika kuwapatia washiriki mabadiliko yanayoendelea kote duniani na nchini.

Alisema kuna haja ya kuangalia maeneo ambayo hayafanyiki vizuri ili kuimarisha utoaji wa huduma za uhamiaji Tanzania na kuna wakati kumekuwa kukijitokeza changamoto baina ya taasisi za Muungano na zisizo za Muungano.

Kutokana na hali hiyo, alisema lazima kuwe na mtaala maalum wa kuwafundisha viongozi wa ngazi mbalimbali ndani ya Idara ya Uhamiaji kwa kuzingitia mahitaji halisi ya uongozi kwa kila ngazi pamoja na changamoto zinazojitokea bila kuathiri mafunzo mengine ya kuwajengea askari na maofisa uwezo na weledi katika maeneo ya uhamiaji.

Alisema kwa kufanya hivyo, Idara ya Uhamiaji itakuwa na utaratibu wa kuandaa viongozi makini wa sasa na wa baadaye, hivyo kuwa na mpango bora wa kurithishana madaraka.

Pia alisema ziko changamoto ndani ya nje ya Idara ya Uhamiaji ambazo wanakabiliana nazo, hivyo hawana budi kujenga mfumo thabiti wa uongozi unaowajibika ipasavyo katika ngazi mbalimbali.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwapo na kilio kikubwa cha upungufu wa askari, vitenda kazi ndani ya idara hiyo. Kutokana na kilio hicho, kuna umuhimu wa kuomba nafasi za ajira kwa idara hiyo ili kufikia malengo.

Alisema licha ya upungufu uliopo wa askari aliwataka kuendelea kuwatumia kwa ufanisi askari walioko ili idara hiyo kuchangia ipasavyo katika kuimarisha usalama wa nchi pamoja na mipaka ya nchi.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema mafunzo hayo yaliyoendeshwa na Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Kilimanjaro, yanahusu uongozi wa kiuhamiaji mabadiliko ya kiuchumi, changamoto na fursa.

Alisema idara ya uhamiaji inakazi kubwa ya kudhibiti na kuwezesha uingiaji na ukaaji wa wageni na kuhakikisha huduma wanazotoa ni bora ili kukuza biashara ya utalii.

Katika kuimarisha huduma zao kupitia mafunzo hayo, alisema wamepata mafanikio makubwa kuimarisha huduma zao na kuongeza wageni nchini kwa kutoa huduma bora.

# Mke wa Rais ataka nguvu ya pamoja kutokomeza maradhi

**Na Rahma Suiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, amesema maambukizi ya virusi vya Ukimwi, homa ya ini na kaswende kutoka kwa wazazi kwenda mtoto, ni tishio nchini na kwamba nguvu ya pamoja inahitajika kuyatokomeza.

Mama Mariam aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa mpango mkakati wa kitaifa wa kutokomeza maradhi hayo uliofanyika katika hoteli ya Verde, Zanzibar.

Alisema takwimu kuhusu maambukizi zinathibitisha kwamba bado maradhi hayo ni tishio nchini juu ya kujenga mustakabali bora wa afya ya jamii. Kwa mujibu wa kiongozi huyo, maradhi hayo yanamgusa mtoto moja kwa moja kupitia kwa mama mwenye maambukizi wakati wa ujauzito, kujifungua na wakati wa kunyonyesha. Alisema maradhi hayo yameathiri dunia ikiwamo Zanzibar na kupunguza nguvu kazi ya taifa kwa kudhoofisha afya za vijana ambao ndio rasilimali ya ujenzi wa nchi.


"Lakini maradhi haya yanaweza kuwa mzigo katika juhudi za kudhibiti matumizi ya huduma za matibabu ambayo ni ghali sana," alisema.

Pia alisema watoto wanaozaliwa na maambukizi ya VVU, wana uwezekano mkubwa wa kufariki dunia kulinganisha na wanaozaliwa bila maambukizi hayo. "Lakini wana uwezekano wa kulazwa hospitalini mara kwa mara na wengi wao hufariki dunia kabla ya kufika hata kufika umri wa miaka miwili," alisema.

Kadhalika, alisema watoto wanaozaliwa na maambukizi ya homa ya ini 'B', wako katika uwezekano mkubwa wa kupata usugu wa maradhi hayo ambayo husababisha athari kwa ini ikiwamo kusinyaa na uwezekano wa kupata saratani ya ini.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema serikali imejipanga kuhakikisha maambukizi ya maradhi hayo matatu yanakuwa asilimia sifuri na hilo linawezekana.

Alisema mafanikio yamepatikana kupunguza kasi ya maambukizi mapya. Hata hivyo, alisema bado wananchi wanaambukizwa na kusambaza kwa kasi maradhi hayo.





# Jaji Kiongozi atoa somo kwa mawakili, wanasheria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewataka mawakili na wanasheria kuwashauri wateja wao kufanya usuluhishi wa migogoro yao kwa kupatana na si kila kitu kupelekwa mahakamani.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupunguza mrundikano wa mashauri.

Jaji Siyani ambaye ni Kamishna wa Tume ya Utumishi ya Mahakama, aliagiza hayo juzi kwenye mkutano wa tume hiyo na wadau wa mahakama mkoani Shinyanga, uliofanyika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga.

Alisema nchi zilizoendelea usuluhishi wa migogoro unamalizwa kwa asilimia 90 na siyo kila kitu kinapelekwa mahakamani ili kupunguza mrundikano wa mashauri.

**Mrundikano wa mashauri uliopo mahakamani hadi sasa kuanzia mahakama za mwanzo, wilaya, mkoa hadi mahakama kuu ni mashauri 3,419.**

"Mrundikano wa mashauri uliopo mahakamani hadi sasa kuanzia mahakama za mwanzo, wilaya, mkoa hadi mahakama kuu ni mashauri 3,419," alisema Siyani.

Aidha, aliwataka pia waandishi wa habari kuandika habari za kuelimisha jamii na faida ya umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, kuwa licha ya kupunguza marundikano wa mashauri mahakama.

Naye Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama alisema wamefanya ziara ya kukutana na wadau wa mahakama mkoani Shinyanga ili kujadili uboreshaji wa utoaji haki kwa wananchi pamoja na kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani.

Alisema katika uboreshaji wa utoaji huduma kwa wananchi, Novemba 25 mwaka huu, wamepanga kuzindua mahakama za wilaya 18 na katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, watazindua mahakama mbili katika Wilaya ya Itilima na Busega mkoani Simiyu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, Athumani Matuma, alisema ziara hiyo ya Tume ya Utumishi wa Mahakama itaboresha utendaji kazi wa mahakama pamoja na utoaji haki kwa wananchi na kwa wakati.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza wakati akifungua jukwaa la nane la maendeleo endelevu lenye dhima ya usimamizi madhubuti wa fukwe jijini Mwanza jana. **PICHA: OMR**

# Mpango asisitiza utunzaji mazingira

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amewataka wadau mbalimbali kutunza mazingira ya fukwe nchini kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aliyasema hayo jana jijini hapo alipofungua kongamano lililohusisha wadau mbalimbali ambalo lililenga kujadili masuala yanayohusu utunzaji wa mazingira ya fukwe.

Kongamano hilo ambalo liliandaliwa na Taasisi ya Uongozi lilikutanisha wadau mbalimbali ambao wanahusika na utunzaji wa mazingira ya fukwe.

Alisema utunzaji wa fukwe ni muhimu kwa kuwa unalinda ikolojia pamoja na kukuza utalii katika maeneo yaliyotunzwa.

Naye Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema lengo la serikali ni kuzigeuza fukwe kuwa sehemu za utalii.

Alisema Ilani ya Chama Cha Mpainduzi (CCM), ya mwaka 2020 inaelekeza serikali kuongeza watalii pamoja na mapato yatokanayo na utalii hapa nchini.

Aliongeza kuwa katika hilo, wizara yake imepiga hatua na kwamba suala la utunzaji wa mazingira ya fukwe ni miongoni mwa vipaumbele vyao katika kukuza utalii.

Baadhi ya wadau katika kongamano hilo, walisema miji mingi inatenga chini ya asilimia moja kwa ajili ya maeneo ya wazi ambayo yanatumiwa kupumzikia.

Walitoa mfano kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao walisema una maeneo machache kwa ajili ya kupumzikia watu mbalimbali.

Wadau hao walisema kupungua kwa maeneo ya wazi kwa ajili ya kupumzikia kunaathiri watoto na vijana kwa kuwa wanashindwa kupata sehemu za michezo.

# Magheto yadaiwa kichocheo mimba za utotoni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NYUMBA za kupanga maarufu kama 'magheto' kwa wanafunzi katika kata ya Lunguya Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, imetajwa kuwa kichocheo cha matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa kike hali inayosababisha kuwapo kwa mimba na ndoa za utotoni.

Hayo yalibainishwa jana na wanafunzi wa shule ya sekondari Lunguya wakati wa mdahalo wa namna ya kuzuia ukatili wa kijinsia shuleni na ndani ya jamii zao uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Korea Kusini (KOICA).

Mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule hiyo, alisema wanafunzi wa kike wanaoishi kwenye nyumba za kupanga wanakuwa na uhuru hivyo ni rahisi kuingia kwenye vishawishi vya mahusiano ya mapenzi na wanaume na kusababisha kupata mimba na kuolewa wakiwa bado wadogo.

Alisema baadhi yao wamekuwa na tabia ya kuwashawishi wanafunzi wa kike kuwa na mahusiano na wanaume wa mitaani na kujikuta wapo kwenye mapenzi na kupoteza ndoto zao huku akiomba serikali kuwachukulia hatua wanaotembea na wanafunzi.

"Sisi wenyewe tumekuwa chanzo cha ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wenzetu wa kike, tunapokea fedha kutoka kwa wanaume wa mitaani na kuwashawishi kuingia kwenye mahusiano halafu wanapopata mimba tunaanza kuwacheka huku sisi ndio chanzo," alisema John.

Mwanafunzi mwingine, Msanja Samweli, alisema wanaowapatia mimba wanafunzi wa kike wanafahamika ikiwamo waendesha bodaboda, wachimbaji wadogo wa madini lakini wanaogopa kusema kwa kuhofia kufanyiziwa matukio maovu na wahusika na kuimba serikali kwa hili kuwa wakatili ili kumnusuru mtoto wake na masomo yake.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Lunguya, Lucas Gombe, alisema wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwaka huu waliokuwa 117 na kwamba walianza wakiwa 245.

Mwenyekiti Msaidizi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Lunguya, Irene Nyanza, aliwataka wanafunzi hao wa kiume waliopewa elimu ya ukatili wa kijinsia wanapoona viashiria vya ukatili watoe taarifa kwenye kituo hicho na mamlaka nyingine kwa msaada kwani wapo kwa ajili yao.

Kadhalika, mratibu wa shughuli zinazofanywa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) mkoani Shinyanga, John Shija alisema, wanafunzi wa kiume wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuwalinda watoto wa kike na kuwasihi kutoyafumbia matukio na kutoa taarifa zinazomlinda mtoto wake.

Ofisa kiongozi wa mradi kutoka TGNP, Joyce Mkina, alisema lengo la mdahalo huo ni kuongeza ushiriki wa vijana na wavulana katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

## Uingereza kupeleka ndege Ukraine

**LONDON,** UINGEREZA

Uingereza kwa mara ya kwanza inatuma ndege aina ya helikopta nchini Ukraine, kwa ajili ya kusaidia jeshi la nchi kuwadhibiti wavamizi.

Waziri wa Ulinzi, Ben Wallace, alisema helikopta tatu za zamani za Sea King zitatolewa na ya kwanza tayari imewasili nchini humo.

Katika wiki sita zilizopita, wafanyakazi wa Ukraine walipata mafunzo nchini Uingereza kuzirusha na kuzikarabati ndege hizo.

Wallace alisema Uingereza pia itatuma risasi 10,000 za ziada.

Alitoa tangazo hilo kutoka mjini Oslo, ambapo anakutana na washirika kujadili msaada unaoendelea wa kijeshi kwa Ukraine.

Waziri huyo wa ulinzi alisema kuwa shehena hiyo ya risasi zitasaidia wanajeshi wa Ukraine kulinda eneo lililokombolewa hivi karibuni.

Ndege hiyo ya helikopta, Sea King hapo awali ilitumiwa na Jeshi la Anga na Jeshi la Wanamaji la Uingereza, na ndege ya mwisho ilistaafishwa na Jeshi la Wanamaji mwaka 2018.

Nchi chache zimetuma ndege za rubani nchini Ukraine tangu kuanza kwa mzozo huo, na maombi ya serikali yake kwa mataifa ya Magharibi kutuma ndege za kivita hadi sasa hayajajibiwa.

Mwishoni mwa wiki, Waziri Mkuu Rishi Sunak alitumia ziara yake nchini Ukraine kutangaza awamu mpya ya msaada wa kiulinzi wa pauni milioni 50 ambao ulijumuisha bunduki 125 za kukinga ndege na vifaa vya kukabiliana na ndege zisizo na rubani zinazotolewa na Iran.

Katika hatua nyingine, Wabunge wa Umoja wa Ulaya wanatarajiwa kuipa Russia hadhi ya taifa linalodhamini ugaidi kutokana na matendo ya nchi hiyo katika vita vyake dhidi ya Ukraine.

Itakuwa mara ya kwanza kwa Umoja wa Ulaya kwa ujumla wake kuchukuwa hatua kama hiyo, lakini haijulikani itakuwa na maana gani.

Kulingana na waraka ulioandaliwa na idara ya utafiti ya Bunge la Ulaya, Russia inafanya mashambulizi yake kuwalenga raia na miundombinu ya kiraia, ikiwemo hospitali, shule na vituo vya afya.

**BBC**

# Marais wakutana kuwajadili M23

**LUANDA,** ANGOLA

MKUTANO wa kutafuta amani mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) umefanyika nchini Angola na kuwakutanisha viongozi wa nchi tano.

Mkutano huo umefanyika katika mji mkuu wa Angola, Luanda katika juhudi za kutafuta ufumbuzi wa ghasia na kukomesha harakati za waasi wa M23.

Tangazo la ofisi ya Rais wa Angola Joao Lourenco, lilisema viongozi walioalikwa ni Felix Tshisekedi wa DRC, Paul Kagame wa Rwanda, pamoja na mpatanishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta.

Pia mkutano huyo utajumuisha mwenyekiti wa sasa wa jumuiya hiyo, Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye. Aidha, Ikulu ya Burundi imethibitisha kushiriki kwa Rais Ndayishimiye katika mazungumzo hayo.

Katika mkutano na waandishi wa habari jana jioni, msemaji wa Ikulu ya Kinshasa, Patrick Muyaya alisema serikali ya nchi hiyo haitakubali kuzungumza na kundi la waasi la M23, hadi pale litakapokuwa limeondoka kikamilifu katika maeneo yote iliyoyakamata kwa mtutu wa bunduki

Katika hatua nyingine, Msemaji wa jeshi la DRC amesema kuwa ndege ya kijeshi ya Ufaransa iliyoanguka mjini Kisangani siku ya Ijumaa ilipata ajali kutokana na hitilafu ya kiufundi. Katika mazungumzo na waandishi wa habari yaliyopeperushwa na televisheni ya serikali ya DRC, Msemaji huyo Patrick Muyaya, ndege hiyo ilikuwa njiani kuelekea katika kisiwa cha Reunion, ikalazimika kupitia Bujumbura Burundi, na kuelekea katika mji mkuu wa Chad wa Ndjamena.

Tangu mwishoni mwa juma taarifa ya ndege hiyo ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii, huku wengi wa wakisema ndege hiyo ya kijeshi ilikuwa ikipeleka silaha kwa wapiganaji wa kundi la M23.

Baadhi waliishutumu Ufaransa kwa kuunga mkono kundi la M23 ambalo limekwisha yadhibiti maeneo mengi ya jimbo la Kivu Kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.

Ufaransa haijatoa kauli yoyote kuhusiana na ndege hiyo.

Muyaya alisema ndege hiyo ilitua Kisangani kutokana na tatizo la kiufundi.

"Kwani moja ya injini zake ingeweza kuungua ." alisema

Aliongeza kuwa uwanja wa ndege uliokuwa karibu kutua ni uwanja wa ndege wa Bangboka uliopo Kisangani.

Ndege hiyo ilikuwa na jumla ya abiria 9, na picha zao zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

**DW**



Mwanakijiji akiangalia nyumba zilizoharibika kufuatia tetemeko la ardhi la kipimo cha 5.6 ambalo limeua watu 162, huku mamia wakijeruhiwa na wengine kutoweka katika eneo la Cianjur nchini Indonesia jana. **PICHA: AFP**

# Marekani yataka majeshi kuondolewa Tigray

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken amezungumza na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed kuhusu utekelezaji wa mkataba wa kusitisha mapigano kati ya wanajeshi wa serikali na vikosi vya Tigray kaskazini mwa nchi hiyo.

"Waziri Mkuu wa Ethiopia na mimi tulijadili hatua ya dharura ya kutekeleza makubaliano ya kusitisha uhasama na kupata amani ya kudumu kaskazini mwa Ethiopia," alisema Blinken kupitia ukurasa wake wa Twitter.

Katika wito wake, Blinken alisisitiza kuhusu umuhimu wa kutekeleza mara moja mpango huo. Mpango huo ni pamoja na kuondoa majeshi yote ya kigeni na kupokonywa silaha kwa wakati mmoja kwa vikosi vya Tigray.

Abiy tayari alisisitiza kujitolea kwa serikali yake katika mapatano ya amani.

Waziri huyo alisema Marekani imejitolea kuunga mkono mchakato unaoongozwa na Umoja wa Afrika ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na uhakiki wa makubaliano ya amani.

Blinken alitambua juhudi zinazoendelea za serikali ya Ethiopia kufanyia kazi usambazaji wa misaada ya kibinadamu na kurejesha huduma za kimsingi katika jimbo la Tigray na maeneo jirani ya Afar na Amhara.

Vikosi vya eneo la Amhara na Afar, pamoja na wanajeshi wa Eritrea, wamekuwa wakipigana pamoja na vikosi vya serikali dhidi ya wapiganaji wa Tigray.

Novemba 2 serikali ya Ethiopia na wapiganaji wa Tigray walikubaliana kusitisha mapigano, katika hatua ambayo haikutarajiwa.

Mzozo huo umesababisha vifo vya maelfu ya watu huku wengine wakikabiliwa na tishio la baa la njaa

**BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 856 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late LEONARD HAMIS MUHONAME**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**JOYCE LEONARD MUHONAME**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22nd day of December, 2022.

Dated at **DAR ES SALAAM** this **22** day of November, 2022.

Senior Resident Magistrate

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**COSMA DONATI KWEKA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 881 AZH Toyota Hiace.** Chasses Namba **JTFSX23P6016927,** Engine Namba **2R219670856** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**Polisi Taafifa : KIL/MOS/RB/393470/2022**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**Datius Burchard,** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S 1689-0087** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Peace Secondary School mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/MAP/RB/443660/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**GOODWHEELS (T) COMPANY LTD** Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC. 758 DBA** yenye Chassis No. **LW8HDNZ46MW043282,** Engine No. **WH170MMB210756475,** Model No, **WH250ZH-2B** aina ya **WANHOO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya polisi.
**KAH/RB/1809/2022.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ANASTAZIA M. ONARY** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.5282-0527** iliyotolewa na **JULIUS KAMBARAGE NYERERE SEKONDARI – TARIME** mwaka 2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: MWA/MAG/RB/419557/2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA TEMEKE**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 349 YA 2022**
**MNYONGWA EZRA BARAMPAMA...............MDAI**
**DHIDI YA**
**HASHIM MOHAMED HAMSINI.........1. MDAIWA**
**FRANCIS JOSEPH MSEKWA.........2. MDAIWA**
**YUSUFU HASSAN.........3. MDAIWA**
**ZAKIA MAKONO...............4. MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**HASHIM MOHAMED HAMSINI, FRANCIS JOSEPH MSEKWA, YUSUFU HASSAN NA ZAKIA MAKONO – POPOTE MLIPO.**

**MNYONGWA EZRA BARAMPAMA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Temeke (Usalama). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 12/12/2022 saa 3:00 Asubuhi. Mnatakiwa mfike nyinyi au Wakili wenu pasipo kukosa.

AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo terehe 21 mwezi 11 mwaka 2022 mbele ya Mheshimiwa.

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UHUMA FINANCIAL SERVICES - DODOMA TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 23/12/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA CROWN YENYE NAMBA ZA USAJILI T 140 DLV MALI YA ATUPELE MWAISUMO MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE DODOMA. PIA TUTAUZA ENEO LA SHAMBA LILILOPO MUNGANO MALI YA JACQLINE NDAKIDENI BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MIKOPO WALIYOKOPA UHUMA FINANCIAL SERVICES, MNADA UTAFANYIKA MAHALI AMBAPO SHAMBA LIPO

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

## BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

**WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.**

## NOTISI YA SIKU (14) NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **BILO STAR DEBT COLLECTOR COMPANY LIMITE**D kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **STANBIC BANK TANZANIA LIMITED** tunapenda kukutaarifu ndugu **FRANK TRADING COMPANY LTD** unatakiwa kulipa deni unalodaiwa na mteja wetu. Kwamba unatakiwa kulipa deni hilo ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Pia tumeelekezwa kuwa ukishindwa kulipa deni hilo ndani ya siku (14) tutauza kwa mnada wa hadhara mali zako zilizowekwa dhamana ambazo ni kama zifuatazo:-

| JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA AINA YA DHAMANA (MAGARI) | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| FRANK TRADING COMPANY LTD | • SHACMAN T 147 DXD<br>• SHACMAN T 145 DXD<br>• SHACMAN T 474 DTP<br>• SHACMAN T 472 DTP<br>• SHACMAN T143 DXD<br>• SHACMAN T142 DXD<br>• HOWO T 723 DTC<br>• HOWO T 718 DTC | Ghala ya BILO STAR lililopo Mbezi Beach Dar es Salaam | Mnada utafanyika tarehe 08/12/2022 kuanzia saa tano asubuhi na kuendelea |

1171162902

**MASHARTI YA MNADA**

Mnunuzi atakayefanikiwa kununua magari husika atalazimika kulipa 25% papohapo na kiasi kilichobaki 75% atatakiwa kulipa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe yam nada. Akishindwa kulipa 25% aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.

**KWA MAELEZO ZAIDI**
**Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi Beach au wasiliana nasi kwa simu namba 0719206984, 0716943424,0713552685 email: bilostarcompany@gmail.com, S.L.P 16095 DAR ES SALAAM.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Harmonize kutumbuiza Sol Fest

MSANII Harmonize kutoka lebo ya Konde Music Worldwide amethibitisha atakuwa mmoja wa wasanii watakaotumbuiza katika tamasha kubwa la Kundi la Sauti Sol almaarufu Sol Fest litakalofanyika Desemba 17, mwaka huu nchini Kenya.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Harmonize alisema ni sharti ahudhurie kwani ameshapata mwaliko rasmi na kipindi hicho atakuwa Kenya baada ya kutumbuiza katika Tamasha la Eldoret.

"Niaje watu wangu wa 254 Kenya huyu ni Konde Boy kutoka Konde Music Worldwide na ninawathibitishia nitakuwapo katika Tamasha la Sol Fest mnamo Desemba 17," aliandika," Harmonize.

Sol Fest ni tamasha la kimuziki linaloandaliwa kila mwaka na kikundi cha wanamuziki cha Sauti Sol kama moja la kusherehekea mafanikio yao kimuziki kwa mwaka mzima na pia kutangaza maazimio yao katika mwaka unaofuata.





# MOBETTO: SINA KINYONGO NA WEMA

Na Mwandishi Wetu

MWANAMITINDO na msanii wa Bongofleva, Hamisa Mobetto, ameweka wazi hana kinyongo chochote na msanii mwenzake, Wema Sepetu.

Wawili hao ndio mastaa wa kike wa Tanzania wanaofuatiliwa zaidi kwenye mitandao ya kijamii na kwa muda mrefu mashabiki wao wamekuwa wakiwashindanisha na hivyo kufanya ionekana kama wanazozana.

Mobetto hata hivyo amebainisha ana uhusiano mzuri na mwigizaji huyo na kuficha huwa wanawasiliana mara kwa mara.


"Hatuna utofauti. Huwa tunaongea kabisa wakati mwingi," alisema.

Wasanii, Mobetto na Wema pia waliwahi kuwa wapenzi wa bosi wa WCB, Diamond Platnumz kwa nyakati tofauti.

Mobetto pia alikanusha madai ya kushindana na mwigizaji huyo kwenye wafuasi wa mitandao ya kijamii. Alisema hajishughulishi sana na mitandao hiyo na yuko pale kwa ajili ya kutengeneza fedha tu.

"Ingekuwa sitengenezi fedha, basi nisingekuwa na akaunti. Ndio maana watu wanalalalamika kwa ukurasa wangu umejaa matangazo, lakini ndio maana niko hapo. Nahitaji kutengeneza pesa hapo," alisema.

Pia aliweka wazi hajawahi kununua wafuasi wa Instagram.



# Zuchu: Diamond shujaa wangu

BAADA ya shoo yake ya Ijumaa kutofanya vizuri, kule Houston, Marekani kwa kukosa watu, Zuchu amesema Diamond ndiye shujaa wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Zuchu alieleza namna alivyomwaga machozi baada ya shoo yake kukosa watu.

Lakini kama wanavyosema Mungu humpa mtu muda anaoutaka, Zuchu hakujua kama jioni yake angeenda kubeba tuzo ya AFRMMA.

Chozi lake liligeuka baraka baada ya kubeba tuzo hiyo na usiku wa tuzo hizo alieleza namna alivyoumia baada ya shoo yake kubuma.

Zuchu aliongeza Diamond ni shujaa wake na anampenda sana.

## HABARI MICHEZO



Msanii wa Bongo Fleva na Balozi wa Parimatch Tanzania, Marioo (katikati), akisikiliza uzinduzi wa kampeni ya Chomoka na Ndinga la Kombe la Dunia iliyotambulishwa jijini, Dar es Salaam. Wengine kuanzia kulia ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Erick Gerald, Mkaguzi Mkuu wa Michezo ya Kubahatisha nchini, Emmanuel Ndaki , meneja wake msanii huyo, Abbah na Ofisa Habari wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PARIMATCH YALETA CHOMOKA NA NDINGA KOMBE LA DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU utamu wa michuano ya Kombe la Dunia inayoendelea nchini Qatar, Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya Parimatch Tanzania imewapa wateja na wadau wake nafasi ya kubeti mchongo wa kujishindia gari mpya na ya kisasa, simu janja pamoja na bodaboda kutoka katika kampeni yao ya Chomoka na Ndinga.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Habari wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed, wakati alipokuwa akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo na kusema promosheni hiyo ni mahususi kwa wateja wao wote wenye akaunti na hata wateja wapya watakaojiunga katika kipindi hichi cha Kombe la Dunia.

"Katika kipindi cha kuanzia Novemba 22 hadi 26, mwaka huu, mteja wa Parimatch akifanya bashiri kwenye mchezo wowote basi ataingia moja kwa moja katika droo ya kuwania gari aina ya Urban Cruiser yenye O kilometa kutoka katika showroom ya Toyota Tanzania, bodaboda aina ya Hero Hunter 125cc na smartphone aina ya Samsung Galaxy A03 Core (Simu janja)," alisema Mohamed.

**Aliongeza kila siku watakuwa wanatoa simu mbili na washindi watatangazwa kupitia kurasa zao za kijamii na zawadi ya bodaboda itatolewa kwa wiki mara moja, siku ya Ijumaa, kupitia droo itakayoruka kituo cha ITV, wiki husika.**

Zawadi ya gari itatolewa mwisho wa mashindano haya Desemba 27, mwaka huu ambapo droo kubwa ya kutafuta mshindi wa gari itafanyika siku hiyo.

Pamoja na hayo, Mohamed alifafanua katika promosheni hiyo sehemu ya michezo ya TVBET, Live Casino, Casino New na michezo ya Virtual haitaruhusiwa kushiriki katika promosheni hiyo.

Kampuni ya Parimatch imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya asilimia 100 mpaka Sh. milioni moja kwa wateja wapya wanaojiunga nao na imekuwapo nchini tangu mwaka 2019, ikitoa huduma zinazojumuisha malipo ya haraka, odds kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, Kasino na Michezo ya virtual.

Mbali na soka, Parimatch pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, kikapu, kriketi, baseball na michezo mingine ya Live na pre-match.

## Azam yaigeukia Coastal Union

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuendeleza kasi ya ushindi, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kally Ongala, amesema sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja Azam Complex, Dar es Salaam.

Kally aliliambia gazeti hili, lengo la timu hiyo ni kupambana kushinda kila mechi na kamwe haitazami matokeo ya wapinzani wao, wakiwamo Simba na Yanga.

Kocha huyo alisema mechi zote wanazocheza ni ngumu kwa sababu kila timu imejipanga kusaka matokeo bora, hivyo kwao wanaheshimu wapinzani wote wanaokutana nao kwenye ligi hiyo.

"Malengo yetu ni kutwaa ubingwa, ili tufikie ni lazima tushinde kila mechi iliyopo mbele yetu, hatuwezi kufikia malengo hayo bila ya wachezaji wetu kupambana katika kila mchezo," alisema Kally.

Aliongeza wanahitaji kuvuna pointi tatu katika kila mechi na hawafanyi hivyo kwa kushindana

## Ligi ya Kabaddi kuanza Des.

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya Taifa ya mchezo wa Kabaddi inatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 19 hadi 24, mwaka huu hapa jijini, Dar es Salaam imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Chama cha Kabaddi Tanzania, Abdallah Nyoni, alisema lengo la kuanzisha ligi hiyo ni kupata wachezaji watakaounda kikosi cha taifa.

Nyoni alisema maandalizi kuelekea ligi hiyo yako katika hatua za mwisho na chama kinawaomba wadau wajitokeze kushirikiana nao ili kufanikisha wanafikia malengo.

Alisema kikosi cha taifa kitakachopatikana kitaingia kambini Januari Mosi, mwakani na kinatarajia pia kwenda kuweka kambi yake India kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya dunia.

## *Mkwasa alia na mastraika Ruvu*



**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwassa, amesema tatizo linaloiangusha timu yake kwa sasa ni washambuliaji kukosa utulivu na umakini wa kutumia vyema nafasi wanazotengeneza katika michezo mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea hapa nchini.

Ruvu Shooting hivi karibuni ilipoteza michezo miwili mfululizo, ikifungwa bao 1-0 na Azam FC na baadaye kukubali kichapo cha magoli 4-0 kutoka kwa Simba, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakiwa wenyeji.

Mkwasa alisema hawakufanya vizuri katika michezo minne mfululizo huku mechi mbili wakipoteza kwa nyota wake kurudia makosa yale yale.

"Tunaendelea kufanyia kazi madhaifu yetu na nina imani tutakuja kukaa vizuri licha ya kuwepo kwa changamoto ya wachezaji wangu wengi wa kikosi cha kwanza kwenda kozi, " alisema Mkwassa.

Aliongeza kwa sasa wamerejea tena katika mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Singida Big Stars kwenye mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO NJIA PANDA
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo yupo njia panda kuhusu uhamisho wa kwenda Newcastle United au Al- Nassr ya Saudi Arabia kufuatia nyota huyo mwenye umri wa miaka 37 kuondoka Manchester United kwa makubaliano na klabu hiyo. ***(Marca)***

### UNITED YAOKOA MAMILIONI
KLABU ya Manchester United imeokoa mishahara ya takriban pauni milioni 15.5 baada ya kufikia makubaliano na Cristiano Ronaldo kumaliza mkataba wake kabla ya kumalizika majira ya joto. ***(Times)***

### CHELSEA YAMTAKA RONALDO
CHELSEA inatarajiwa kuanza mazungumzo juu ya Cristiano Ronaldo huku mmiliki mwenza, Todd Boehly akiona mvuto wa kumsajili Mreno huyo kwa uhamisho wa bure, ingawa kocha, Graham Potter hajashawishika. ***(CBS, via Sun)***

### CHELSEA, NEWCASTLE KIMYA
KLABU ya Chelsea na Newcastle zinadaiwa kujitenga na mpango wa kumnunua Cristiano Ronaldo, huku Inter Miami wakidaiwa kuangalia kwingine. ***(Telegraph)***

### DANILO ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Palmeiras Mbrazil Danilo mwenye umri wa miaka 21 katika dirisha la Januari. ***(Sun)***

### THURAM ANUKIA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United ipo tayari kuilipa Borussia Monchengladbach pauni milioni 10 ifikapo Januari ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa Marcus Thuram mwenye miaka 25, ambaye mkataba wake unaisha msimu ujao. ***(Football Insider)***

### GUARDIOLA SAFI CITY
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekubali kuongeza mkataba wa miaka miwili kubakia klabuni hapo ambao utamalizika ifikapo 2025. ***(The Athletic)***

### DEPAY HAJUI HATIMA YAKE
MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28, amesema hana uhakika kuhusu mustakabali wake Barcelona, baada ya kuibua shabaha ya klabu ya zamani ya Manchester United katika dirisha la usajili la majira ya joto.***(Mail)***

### TCHOUAMEN: NILITAKIWA LIVER
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22, amesema Liverpool walimtaka kwa mara ya kwanza lakini alikuwa na nia ya kuhamia Real Madrid kutoka Monaco msimu huu wa joto mara tu timu hiyo ya Hispania ilipomnunua. ***(Le Parisien, via 90 Min)***

### DE JONG ALITAJWA BARCA
MSHAURI mmoja wa Barcelona amejibu pendekezo la mchezaji anayelengwa na Manchester United, Frenkie de Jong kwamba bodi ya klabu hiyo ilifichua maelezo ya mkataba wa kiungo huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, msimu uliopita wa joto. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GIROUD AFIKIA REKODI YA HENRY UFARANSA

●●●Afikisha mabao 51, lakini akiwa kwenye tano bora ya...

**DOHA, Qatar**

OLIVIER Giroud ameifikia rekodi ya Thierry Henry kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote wa Ufaransa baada ya kufunga mara mbili katika ushindi wa magoli 2-1 ambao Ufaransa waliupata dhidi ya Australia kwenye Kombe la Dunia juzi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alifunga bao lake la 50 na 51 kwa Les Bleus hao walipofungua kampeni yao ya hatua ya makundi ya Kombe la Dunia 2022 kwa ushindi huo.

Giroud alifunga bao la pili la Ufaransa baada ya Adrien Rabiot kumnyang'anya Nathaniel Atkinson mpira na kumpasia mshambuliaji huyo wa AC Milan.

Baada ya kukosa mkwaju wa ajabu wa juu katika kipindi cha pili, Giroud alisawazisha rekodi ya Henry kwa mpira wa kichwa kutoka kwa krosi ya Kylian Mbappe.

Mabao mawili ya Giroud ya kufunga rekodi yalikuja kwenye mechi yake ya 115 akiwa na Ufaransa, ambayo sasa anashikilia nafasi ya tano kwenye orodha hiyo ya wachezaji waliocheza mechi nyingi.

Anahitaji mechi nane zaidi ili kuingia kwenye nafasi tatu za juu, huku Henry akiwa wa tatu katika msimamo huo akiwa na mechi 123.

Laurent Blanc alimchezesha Giroud mechi yake ya kwanza ya Ufaransa mwaka 2011 alipokuwa akichezea Montpellier ya Ligue 1.

Mtindo wake wa uchezaji wa kujitolea ulikuwa muhimu kwa ushindi wa Ufaransa wa Kombe la Dunia 2018, huku akiwa na uhusiano bora wa ndani na washambuliaji wenzake Mbappe na Antoine Griezmann.

Giroud alitazamiwa kuanza kampeni za 2022 kwenye benchi kabla ya Karim Benzema kujiondoa katika dimba hilo kutokana na jeraha.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,053,2
MECHI KALI
PORTUGAL
VERSUS
GHANA
1 | 1.37
X | 4.58
2 | 8.37
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI: HAKUNA VISINGIZIO KUFUNGWA NA SAUDI ARABIA



**DOHA,Qatar**

LIONEL Messi amesema Argentina "haina visingizio" baada ya kufungwa mabao 2-1 na Saudi Arabia katika mechi ya ufunguzi wa Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lusail, juzi.

Argentina walielekea katika dimba hilo wakiwa miongoni mwa wanaopewa nafasi kubwa ya kushinda taji lao la tatu, na mkwaju wa penalti wa Messi uliiweka La Albiceleste mbele hadi mapumziko huku wakionekana kukaribia ushindi wa kwanza katika Kundi C.

Hata hivyo, mabao mawili katika muda wa dakika tano kutoka kwa Saleh Al Shehri na Salem Al Dawsari yalipindua kabisa maandishi, na upande wa Messi ukahukumiwa kwa moja ya majanga makubwa katika historia ya Kombe la Dunia.

Messi alikiri yeye na wachezaji wenzake lazima wasitafute kuhalalisha upotezaji huo wa kushangaza, ingawa alitumai ingeleta kundi karibu zaidi.

"Hakuna visingizio," Messi aliwaambia waandishi wa habari katika mkutano wake baada ya mechi.

"Ni pigo gumu sana kwa kila mtu, hatukutarajia kuanza hivi.

"Tunaenda kuwa wamoja kuliko wakati mwingine wowote. Kundi hili liko imara na wameonyesha.

"Hii ni hali ambayo hatukuwa nayo kwa muda mrefu, sasa inabidi tuonyeshe hili ni kundi la kweli.

"Mambo hutokea kwa sababu. Tunapaswa kujiandaa kwa kile kinachokuja, lazima tushinde na inategemea sisi."

# Rasmi Ronaldo anaondoka United

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo (37), anatarajiwa kuondoka Manchester United mara moja.

Uamuzi huo unafuatia mahojiano yenye utata ambapo aliikosoa klabu hiyo na kusema "hana heshima" kwa kocha, Erik ten Hag.

Pande zote mbili zilisema kuondoka kwa Ronaldo "ni uamuzi uliokubaliwa kwa pamoja".

"Klabu inamshukuru kwa mchango wake mkubwa katika misimu miwili ndani ya Old Trafford," ilisema taarifa ya Manchester United.

Walimtakia "yeye na familia yake heri kwa siku zijazo" na wakaongeza "kila mtu katika Manchester United anabakia kulenga kuendeleza maendeleo ya timu chini ya Erik ten Hag na kufanya kazi pamoja kuleta mafanikio uwanjani".

Ronaldo yuko pamoja na Ureno kwenye fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar na anatazamiwa kuwa nahodha wao katika mchezo wao wa ufunguzi wa Kundi H utakaochezwa leo dhidi ya Ghana.

"Kufuatia mazungumzo na Manchester United tumekubaliana kwa pamoja kumaliza mkataba wetu mapema," ilisema taarifa ya fowadi huyo.

"Ninaipenda Manchester United na ninawapenda mashabiki, hilo halitabadilika kamwe. Hata hivyo, ninahisi kama wakati mwafaka kwangu kutafuta changamoto mpya.

"Naitakia timu kila mafanikio kwa kipindi kilichosalia cha msimu huu na kwa siku zijazo."



232,366/-

# WANAOKIUKA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI KUSHUGHULIKIWA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kutekeleza majukumu yake ya kusimamia masuala ya hakimiliki na hakishiriki hapa nchini, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania hivi karibuni imetangaza kuendesha kampeni maalum ya kubaini na kuwachukulia hatua wale wote wanaovunja Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7 ya mwaka 1999.

Katika taarifa kwa umma iliyotolewa na ofisi hiyo kwenye vyombo mbalimbali vya habari, ofisi hiyo imetoa onyo kali kwa watu wote wanaokiuka Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 kwa kutumia kazi zinazolindwa na sheria hiyo bila kufuata utaratibu na kujiingizia kipato.

Taarifa hiyo imebainisha kazi hizo zinazolindwa na sheria hiyo ni pamoja na maudhui yote ya vipindi/matangazo ya vyombo vya habari yenye mikataba ya hakimiliki, kazi za muziki, filamu ambazo hufanyiwa udurufu bila kibali cha mmiliki pamoja na kazi zote za ubunifu, ambazo zimekuwa zikisambazwa bila kufuata utaratibu wa kuwa na mkataba au kibali cha mmiliki husika na kujiingizia kipato au kuwa na leseni kutoka Ofisi ya Hakimiliki Tanzania huku mmiliki wa kazi akiwa hanufaiki na kazi hiyo.

"Ofisi ya hakimiliki inatoa onyo kali kwa watu wote wanaofanya vitendo vinavyovunja sheria husika kuacha mara moja," imesisitiza taarifa hiyo.

Aidha Ofisi ya Hakimiliki imetoa rai kwa wamiliki wote wa hoteli, mabasi, kumbi za starehe, kumbi za sherehe, televisheni na redio wanaotumia kazi za muziki na filamu katika biashara zao au maeneo yao wanatakiwa kuhakikisha wanalipia matumizi ya kazi hizo kwani kutolipia matumizi ya kazi hizo ni kosa kisheria.

Kwa mujibu wa sheria hiyo kutumia kazi yoyote inayolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki na kujiingizia kipato bila kibali cha mmiliki ni kosa la uharamia na adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano au faini isiyopungua milioni ishirini au vyote kwa pamoja.

Ofisi hiyo imesisitiza kuwa inafuatilia kwa karibu malalamiko ya wizi wa maudhui unaodaiwa kufanywa na baadhi ya warusha matangazo kwa kurusha matangazo ambayo hawana haki nayo bila kibali kutoka kwa wamiliki wa matangazo hayo.

Pia imetangaza kuwa itaendesha kampeni mahsusi nchi nzima ili kuwabaini wale wote wanaovunja Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki na kwa yeyote atakayebainika kuvunja sheria hiyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Ofisi ya Hakimiliki haitasita kuchukua hatua kali kwa wale wote wanaokiuka Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999 kwa namna yoyote ile," ilisisitiza taarifa hiyo.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ally Mayai (mwenye miwani waliokaa), akiwa na viongozi na baadhi ya wachezaji wa Taasisi ya Fountain Gate iliyoko jijini, Dodoma alipotembelea kituo hicho. **PICHA: MTANDAO**

# Nabi afunguka Yanga ni moto

INATOKA UK. 32

ulikuwa mgumu kwa sababu ya ushindani waliopata kutoka kwa wapinzani pamoja na changamoto ya uwanja ambao ulikuwa na majani mengi.

"Naogoza katika ufungaji. Kikubwa tunaendelea kupambana kutafuta matokeo mazuri kwa ajili ya kuwafurahisha mashabiki na wanachama, tunaendelea na Unbeaten yetu katika michezo ijayo," alisema Mayele.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Melis Medo, alisema kilichosababisha timu yake ikapoteza mchezo huo ni wachezaji kuingiwa na hofu lakini wakishindwa kufuata maelekezo ambayo aliwapa kabla ya mchezo huo.

Medo alisema walianza vizuri lakini baada ya wapinzani wao Yanga kuwazoea, mchezo uliwabadilikia na kutoa nafasi kwa wageni kuwashambulia na kupata bao kabla ya mapumziko.

# SIMBA YAVUTWA

INATOKA UK. 32

bahati mbaya kwa Mbeya City.

Dakika moja baadaye Manula alilazimika kutoka langoni kuokoa hatari ya George Sangija ambaye alikuwa amewazidi mbio mabeki wa Simba.

Straika kwenye mabao saba mpaka sasa Sixtus Sabilo nusura aipatie timu yake bao, alipowahadaa mabeki wa Simba, akabaki na kipa Manula, lakini aliukanyaga mpira alipokuwa kwenye harakati za kufunga akaanguka na Tanzania One huyo akauwahi mpira.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/11/22 | 18:00 | Walsall FC vs Carlisle United | 2.28 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/11/22 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Chesterfield FC | 2.44 | 3.35 | 2.75 |
| 03. 26/11/22 | 18:00 | Shrewsbury Town vs Peterborough United | 3.10 | 3.25 | 2.27 |
| 04. 26/11/22 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 05. 26/11/22 | 20:00 | Dagenham and Redbridge FC vs Gillingham FC | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 26/11/22 | 20:00 | SC Pisa vs Ternana Calcio | 2.21 | 3.30 | 3.20 |
| 07. 26/11/22 | 20:30 | Albacete Balompie vs Racing Santander | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 08. 27/11/22 | 13:30 | Ankara Keciorengucu vs Samsunspor | 2.48 | 3.35 | 2.75 |
| 09. 27/11/22 | 13:30 | Pendikspor vs Eyupspor | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 10. 27/11/22 | 16:00 | Burgos CF vs Real Zaragoza | 2.48 | 2.90 | 3.10 |
| 11. 27/11/22 | 16:00 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 12. 27/11/22 | 17:00 | Como 1907 vs SSC Bari | 2.85 | 3.20 | 2.46 |
| 13. 27/11/22 | 17:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Ascoli Calcio 1898 | 2.40 | 3.15 | 3.00 |
| 14. 27/11/22 | 18:00 | CD Leganes vs Granada CF | 2.55 | 3.00 | 2.90 |
| 15. 27/11/22 | 20:00 | Palermo FC vs Venezia FC | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 16 27/11/22 | 20:00 | FC Cartagena vs SD Eibar | 2.38 | 3.10 | 3.05 |
| 17. 27/11/22 | 22:00 | Spain vs Germany | 2.50 | 3.25 | 2.75 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 24/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1000 | Switzerland vs Cameroon | 1.73 | 3.46 | 4.91 |
| 14:00 | 3528 | Kenkre FC vs Churchill Brothers | 5.04 | 3.73 | 1.58 |
| 14:00 | 3578 | KF Onix Banje vs KF Ballkani | 10.67 | 6.21 | 1.18 |
| 15:30 | 5307 | Lion City Sailors vs Borussia Dortmund | 23.48 | 9.78 | 1.05 |
| 15:40 | 2034 | Sohar Club vs AL Musanaa | 2.19 | 2.79 | 3.52 |
| 16:00 | 1553 | Uruguay vs South Korea | 1.74 | 3.41 | 4.91 |
| 16:00 | 4083 | Wolkite City FC vs Hadiya Hosahina FC | 3.98 | 2.91 | 1.98 |
| 16:05 | 5894 | AL Etihad vs Al Seeb | 5.83 | 3.21 | 1.62 |
| 17:00 | 5312 | Delhi Dynamos FC vs Chennaiyin FC | 1.82 | 3.65 | 3.60 |
| 17:30 | 4003 | Primeiro De Agosto vs Sporting de Benguela | 1.13 | 6.79 | 15.53 |
| 17:30 | 4852 | Sagrada Esperanca vs Recreativo DO Libolo | 1.49 | 3.69 | 6.41 |
| 17:45 | 2356 | Oman Club vs Al Suwaiq | 3.32 | 2.68 | 2.35 |
| 18:00 | 2412 | Aali vs Malkiya Club | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 18:00 | 2869 | Etehad Alreef vs Al-Tadamun Buri | 2.53 | 2.91 | 2.77 |
| 18:00 | 3185 | Bouri vs Najma Manama | 4.66 | 3.49 | 1.67 |
| 18:30 | 2640 | Societe Omnisport vs Stella Club dâ€™Adjame | 2.40 | 2.73 | 3.17 |
| 19:00 | 3024 | Portugal vs Ghana | 1.37 | 4.58 | 8.37 |
| 19:00 | 3422 | Welayta Dicha FC vs Arba Minch Kenema | 2.20 | 2.81 | 3.44 |
| 19:00 | 5940 | Rayon Sports FC vs AS Kigali | 2.50 | 2.79 | 2.94 |
| 20:30 | 1433 | Spartak Trnava vs Zemplin Michalovce | 1.36 | 4.37 | 7.38 |
| 20:30 | 2196 | Slovan Bratislava vs Zlate Moravce | 1.20 | 5.84 | 10.71 |
| 20:30 | 5620 | Dunajska Streda vs Ruzomberok | 1.78 | 3.41 | 4.09 |
| 20:45 | 5088 | Barcelona W vs Bayern Munich W | 1.24 | 5.84 | 7.98 |
| 21:00 | 1862 | ASEC Mimosas vs Racing Club Dabidjan | 1.41 | 3.90 | 7.40 |
| 22:00 | 2050 | Brazil vs Serbia | 1.48 | 4.30 | 6.20 |
| 22:00 | 4914 | Reading W vs Liverpool W | 2.82 | 3.51 | 2.17 |
| 22:30 | 5472 | UE Engordany vs Inter Club De Escaldes | 6.80 | 4.37 | 1.38 |
| 23:00 | 2505 | SL Benfica W vs Rosengard W | 2.02 | 3.60 | 3.07 |
| 23:00 | 2997 | Juventus Women vs Arsenal W | 4.19 | 3.65 | 1.70 |
| 23:45 | 1947 | Tondela vs SCU Torreense | 2.02 | 3.17 | 3.46 |

## IJUMAA- 25/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4462 | Wales vs Iran | 2.05 | 3.15 | 3.79 |
| 14:00 | 3927 | Buriram Utd vs Ratchaburi | 1.29 | 4.87 | 8.18 |
| 15:00 | 4170 | Chonburi vs Port FC | 2.22 | 3.40 | 2.81 |
| 16:00 | 4534 | Qatar vs Senegal | 5.62 | 3.66 | 1.62 |
| 19:00 | 4252 | Netherlands vs Ecuador | 1.78 | 3.50 | 4.50 |
| 20:00 | 4706 | Denizlispor vs Bodrumspor | 4.38 | 3.70 | 1.66 |
| 21:30 | 1126 | FC Martigues vs Orleans | 1.99 | 3.20 | 3.70 |
| 21:30 | 1510 | Red Star vs Nancy | 2.04 | 3.27 | 3.47 |
| 21:30 | 1782 | Saint Brieuc vs Cholet | 2.17 | 3.25 | 3.16 |
| 21:30 | 1908 | Avranches vs Dunkerque | 3.16 | 3.21 | 2.18 |
| 21:30 | 1954 | Paris 13 Atletico vs Concarneau | 3.65 | 3.21 | 2.00 |
| 21:30 | 4460 | Villefranche Sur Saone vs FC Versailles 78 | 2.33 | 3.15 | 2.96 |
| 21:30 | 5516 | Sedan vs Bastia Borgo | 1.78 | 3.41 | 4.35 |
| 21:30 | 5854 | Le Puy vs Bourg Peronnas | 3.71 | 3.26 | 1.97 |
| 22:00 | 5603 | England vs USA | 1.62 | 3.90 | 5.14 |
| 22:15 | 2819 | FC Schaffhausen vs AC Bellinzona | 2.02 | 3.59 | 3.06 |
| 22:45 | 1336 | Larne vs Coleraine FC | 1.51 | 4.00 | 5.27 |
| 23:00 | 4268 | Huesca vs Sporting Gijon | 2.40 | 2.97 | 3.06 |
| 23:45 | 1678 | Porto vs Mafra | 1.10 | 8.62 | 21.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Novemba 24, 2022
Nipashe



UKURASA 29

## Giroud afikia rekodi ya Henry Ufaransa




Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri (kushoto), akipambana kumtoka mchezaji wa Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya CCM Sokoine jijini, Mbeya jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAVUTWA SHARUBU MBEYA

## ●●●Ni baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 ugenini na kuendelea kuiacha...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika 12 kabla ya mechi kumalizika na Tariq Seif wa Mbeya City liliifanya Simba kushindwa kuiengua Yanga kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kutoa sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya jana.

Lilikuwa ni kosa la Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' kumwacha, Awadh Juma kwenye wingi ya kulia akidhania mpira utatoka, lakini mwenzake aliukimbia kwa juhudi zote na kuukuta ukakaribia katika mstari kabla ya kupiga krosi iliyomkuta mfungaji akiwa mbele ya mabeki watatu wa Simba, akaupiga na kutinga wavuni moja kwa moja huku Aishi Manula akishindwa kuufuata.

Bao hilo lilikuwa la kusawazisha baada ya kiungo, Mzamiru Yassin kufunga goli kwa upande wa Simba dakika ya 14 ya mchezo.

Sare hiyo imeifanya Simba kusalia kwenye nafasi ya tatu iliyokuwa ikifikisha pointi 28, na kuziacha Yanga inayoongoza ikifuatiwa na Azam, kila moja ikiwa na pointi 29.

Ni matokeo ambayo pia yameifanya Mbeya City kwenda hadi kwenye nafasi ya sita ya msimamo ikiwa na ponti 19 lakini ikicheza mechi 13.

Kwenye mechi hiyo timu zote zaligawana vipindi, Simba ikitawala kipindi cha kwanza, lakini ikishindwa kufanya chochote kipindi cha pili ambacho Mbeya City ilionekana kutawala dimba la kati na kuwaponza kabisa viungo wa wapinzani wao.

Simba ilionekana kuathiriwa na kukosa kiungo mkabaji madhubuti pamoja na straika mwenye uwezo wa kukaa na mipira mbele, kwani mpira yote mirefu iliyokuwa ikipigwa au krosi ilikuwa ikiokolewa kirahisi na mabeki wa Mbeya City ambao wao walikuwa wakiwadondoshea viungo wao wa kati waliokuwa wanakosa upinzani, hivyo kuigawa kwa mawinga na mastarika wao kirahisi.

Juhudi za Mzamiru kutaka kufunga bao kwenye mechi hiyo zilianza kuonekana dakika ya pili tu ya mchezo alipofanya shambulio kwa kupiga shuti kali lililomshinda kipa wa Mbeya City, Lameck Kayonga, wakati kila mtu akitegemea mpira utakwama wavuni ulitoka nje kidogo ya lango mashabiki wasiamini macho yao.

Hiyo iliyotaka na mpira wa kona fupi kutoka kwa Clatous Chama, ambaye badala ya kuupiga langoni, alimpeleka mchezaji huyo aliyekuwa nje kidogo ya lango.

Dakika sita baadaye nahodha, John Bocco akiwa katikati ya mabeki wa Mbeya City, aligeuka ghafla na kuachia shuti kali ambalo nalo lilitoka sentimeta chache langoni mwa timu hiyo inayomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ndipo Mzamiru aliposawazisha makosa yake kwa kupachika bao kwa mguu wa kushoto akimalizia kazi kubwa iliyofanya na Chama.

Baada ya hapo Mbeya City walionekana kufunguka na kuanza kufanya mashambulizi ya mara kwa mara katika lango la Simba.

Ilikuwa ni dakika ya 29, krosi ya Awadh nusura ilete madhara kwenye lango la Simba, ambapo, Hassan Nassor aliporuka 'tik-tak', lakini aliukosa mpira huo ikawa ni

INAENDELEA UK. 31

# Nabi afunguka Yanga ni moto

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema siri ya kuendelea kupata ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ubora wa kikosi chake lakini pia wachezaji kutambua wajibu wao.

Kauli hiyo imekuja kufuatia ushindi wa mabao 2-0 walioupata Yanga ilipokuwa ugenini kwenye Uwanja wa Liti, Singida dhidi ya Dodoma Jiji, matokeo ambayo yamewafanya wafikishe pointi 29, wakishuka dimbani mara 11.

Nabi aliliambia gazeti hili waliingia katika mchezo huo wakijua wanakwenda kukutana na timu inayotumia nguvu nyingi lakini ubora na uzoefu wa wachezaji wake ndio ulisababisha kuondoka na pointi zote tatu muhimu.

"Niwapongeze wachezaji wangu ingawa tumecheza katika mazingira magumu lakini wamepambana na kupata ushindi, pointi tatu ndiyo ilikuwa kitu muhimu tunachokihitaji, haikuwa rahisi kutokana na uwanja kutokuwa rafiki sana," alisema Nabi.

Kocha huyo ameendelea kulalamikia ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara sio rafiki na inawaweka katika wakati mgumu wachezaji wake kutokana na kukosa muda wakutosha wa kupumzika kutokana na kucheza mechi mfululizo.

Alisema hata matukio ya kuumia kwa wachezaji wake wawili nahodha, Bakari Mwamnyeto na Feisal Salum 'Fei Toto' kumetokana na kukosa muda wa kutosha wa kupumzika jambo ambalo linaweza kuwaathiri na kushindwa kufanya vizuri kwenye mechi zijazo.

"Hali ya majeruhi inatufanya tunawakosa baadhi ya wachezaji wetu muhimu, jambo kubwa tutaendelea kupambana kuhakikisha tunapata ushindi katika kila mechi kwa sababu tunahitaji kufikia malengo," Nabi alisema.

Naye mshambuliaji na kinara wa mabao wa Yanga, Fiston Mayele, alisema mabao aliyofunga katika mechi hiyo ya juzi dhidi ya Dodoma Jiji FC ameendelea kutoa zawadi kwa familia yake hasa kwa mke wake aliyejifunga hivi karibuni.

Mayele alisema mchezo huo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >